Kiswahili

Njia ya Mungu ya Uponyaji



Na A.L. na Joyce Gill

Njia ya Mungu ya Uponyaji

Chake
A.L. na Joyce Gill

Gill Ministries
www.gillministries.com

Vitabu katika Mwongozo Huu

Mamlaka ya Mwamini
Jinsi ya kukoma kushindwa na Kuanza Kushinda

Ushindi wa Kanisa
Kupitia Kitabu Cha Matendo

Karama za Huduma
Mtume, Nabii, Mwinjilisti,
Mchungaji, Mwalimu

Uinjilisti wa Mwujiza
Mpango wa Mungu Kufikia Ulimwengu

Sura ya Kuumbwa Upya
Kutambua Wewe ni Nani Katika Kristo

Mbinu za Kuishi
Kutoka Agano la Kale

Sifa na Kuabudu
Kufanyika Waabudu wa Mungu

Maombi
Kuileta Mbingu Duniani

Kuishi kusio kwa Kawaida
Kupita Karama za Roho Mtakatifu

About the Authors

A.L. na Joyce Gill ni wanenaji wanaojulikana kimataifa, waanzilishi na walimu wa Biblia. Huduma ya utume ya usafiri wa A.L. umempeleka katika nchi zaidi ya sitini, akihubiri kwa umati unaozidi elfu mia moja ya watu na pia kupitia redio na runinga kwa mamilioni.

Vitabu vyao na nakala inayouza sana imeuzwa zaidi ya milioni saba. Maandishi yao, ambayo yametafsiriwa katika lugha nyingi, inatumika katika shule za Biblia na katika semina duniani.

Kweli zenye nguvu zibadilishayo maisha za Neno la Mungu zinalipuka katika maisha ya wengine kupitia huduma za mahubiri, mafundisho, uandishi, video na kanda za kusikiza.

Utukufu wa ajabu wa uwepo wa Mungu unaonekana katika semina za sifa na kuabudu wakati waamini wanagundua jinsi ya kufanyika ibada ya uhusiano wa karibu na Mungu. Wengi wamegundua mbinu mpya ya ushindi na ujasiri kupitia mafundisho yao juu ya mamlaka ya mwamini.

Wamefundisha waamini wengi kuchukua hatua katika huduma zao walizopewa na Mungu kwa nguvu za uponyaji wa Mungu kupitia mikono yao. Wengi wamejifunza kuwa kawaida katika nguvu za juu wakihudumu katika vipawa vyote tisa vya Roho Mtakatifu katika maisha huduma zao kila siku.

Wote A.L. na Joyce wana shahada katika mafunzo ya Thiolojia. A.L. pia na shahada ya udaktari katika philosophia kutoka Chuo Kikuu cha Kikristo cha Vision. Huduma yao imeegemea kwa uthabiti juu ya Neno la Mungu, katikati mwa Yesu, yenye nguvu katika imani na kufundishwa katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Huduma yao huonyesha upendo wake Baba. Mahubiri yao na mafundisho huambatana na upako wa nguvu za juu,, ishara, miujiza, na uponyaji katika miujiza huku wengi wakipigwa katika nguvu za Mungu.

Ishara za uvuvio unaojumlisha mawimbi ya kicheko kitakatifu, kilio mbele za Bwana na kuonekana utukufu wa ajabu wa Mungu unaonekana na wengi wanaohudhuria mikutano zao.

Neno kwa Walimu na Wanafunzi

Mafundisho haya yenye nguvu juu ya uponyaji yanaweka msingi dhabiti wa Neno ambalo huachilia imani kwa wanafunzi ili kupokea uponyaji wao, kuenda katika afya, na kwa ujasiri kuhudumu uponyaji kwa wengine. Wengi wataponywa wakati ufunuo huu utafanyika hai rohoni mwao.

Katika kitabu cha Mariko, maneno ya maagizo ya mwisho ya Yesu kabla hajaondoka duniani yalikuwa, "wataweka mikono yao juu ya wangonjwa nao watapona." Kitabu hiki kinatoa maagizo ya wazi jinsi ya kuhudumia uponyaji kwa wagonjwa.

Kabla ya kufundisha somo hili, tazama au sikiliza video na kanda katika mwongozo huu, na pia soma vitabu vilivyoorodheshwa kama pendekezo. Kadri unavyokolea katika ukweli wa Neno la Mungu kuhusu uponyaji, ndivyo kweli hizi zitaingia moyoni mwako. Nakala hii basi itatoa muhtasari wa kutumia unapotoa kweli hizi kwa wengine.

Mifano ya binafsi ni bora na lazima kwa mafundisho bora. Waandishi hawajatumia katima nakala hii ili mwalimu aweze kutoa mifano yake binafsi yenye ustadi, au kwa wengine ambayo wanfunzi watakubaliana nayo.

Na ikumbukwe kila mara kuwa ni Roho Mtakatifu ndiye mwalimu wetu, na kuwa tunapojifunza, au kufundisha, kila mara tutiwe nguvu na kuongozwa na Roho Mtakatifu.

Mafundisho haya ni bora kwa binafsi au kikundi, shule za Biblia, Shule ya Jumapili na makundi ya nyumbani. Ni muhimu kuwa mwalimu na mwanafunzi wawe na nakala ya kitabu hiki wakati wa masomo.

Andika ndani, tia mistari, tafakari na kutoa maoni katika kitabu hiki. Tumeacha nafasi kwa ajili yako. Mtindo uliotumika ni kwa ajili ya marejeo ya haraka ili kurudia na kusaidia katika kupata mada. Kimeandikwa bora ili kila mtu, baada ya kusoma kitabu hiki, waweze kuwafundisha wengine.

Paulo aliandika kwa Timotheo,

Na mambo uliyosikia kutoka kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo mwakabidhi watu waaminifu watakaowafundisha wengine pia. 2 Timotheo 2:2b

Masomo haya yameundwa kama ili kuhusika katika mafunzo ya Biblia katika Mpango wa Kuendeleza Huduma ambayo imetayarishwa kwa ajili ya mipango ya kujifunza. Wazo hili limetayarishwa kwa ajili ya kujumlisha maishani, huduma, na mafundisho ya baadaye kwa wanafunzi. Wanafunzi wa awali, kwa kutumia nakala hii, wanaweza kufundisha kosi hii wengine.

Orodha ya Yaliyomo

Somo la Kwanza

Mtazamo wa Mungu Kuhusu Magonjwa na Maradhi……7

Somo la Pili

Uponyaji katika Ukombozi Wetu…….17

Somo la Tatu

Yesu – Mfano Wetu 28

Somo la Nne

Roho Mtakatifu na Nguvu Zake.....38

Somo la Tano

Uponyaji kwa Kuwekelea Mikono.....49

Somo la Sita

Maneno Tunayonena.....59

Somo la Saba

Uponyaji Kupitia Vitendo na Maombi.....69

Somo la Nane

Uponyaji Kutoka Ndani Nje 79

Somo la Tisa

Roho Mtakatifu na Vipawa Vyake.....89

Somo la Kumi

Kupokea na Kuifadhi Uponyaji Wako.....100

Somo la Kwanza

Mtazamo wa Mungu Kuhusu Magonjwa na Maradhi

Utangulizi

➢ *Mtazamo wa Mungu*

Wakati mwingine unaposoma somo, ni bora kulichunguza kwa mtazamo wa Mungu. Je, Mungu anahisi vipi kuhusu magonjwa na maradhi?

Katika somo hili, tutaona kuwa uponyaji na afya vilikuwa mpango wa Mungu katika Bblia nzima na vinaendelea hadi kuwa mpango wa Mungu maishani mwetu na huduma.

Uponyaji ni mojawapo ya ahadi za Mungu. Ukiamini na kufwata, ahadi yoyote inaachilia nguvu ya Mungu maidhani mwetu. Tunaitaji ahadi Zake, kuziamini na kuzifwata.

Mithali 4:20,22 Mwanangu, yasikie maneno yangu; tega sikio lako kwa misemo yangu. Kwa kuwa haya ni uhai kwa wale watakaoyapata, ni afya milini mwao.

➢ *Chanzo cha Magonjwa*

Tukiamini kuwa magonjwa yanaweza kutoka kwa Mungu, hatutaweza kumwamini kwa uponyaji wetu. Kwa sababu hii, tunaitaji kuelewa chanzo cha magonjwa.

UMUHIMU WA UPONYAJI

Muhimu kwa Mungu

Ili kumjua Mungu kabisa, ni lazima tumjue Yeye kama Mponyaji.

Kutoka 15:26b Mimi ndimi BWANA nikuponyaye.

Ikiwa hatumjui Bwana kama Mponyaji, tunakosa mtazamo bora wa uhusiano wetu Naye. Uponyaji ulikuwa muhimu kwa Mungu – Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

➢ *Baba*

Roho Mtakatifu alimvuvia Yohana kuandika na kutueleza kuwa uponyaji ni mapenzi ya Baba.

3 John 2 Wapendwa, ntamani juu ya yote kuwa mtaendelea na kuwa na afya njema, na pia nafsi zenu zitanawiri.

Ni bora kuelewa kuwa uponyaji kila mara ni mapenzi ya Mungu.

Imeandikwa pia kuwa Yesu alisema,
Yohana 6:38 Kwa kuwa nimekuja chini kutoka mbinguni, sio kufanya mapenzi yangu, bali mapenzi ya yule aliyenituma.

➢ *Mwana*

Tunapomfuata Yesu katika Injili, tunaona alihudumu uponyaji katika hali nyingi tofauti. Huruma zake kwa wagonjwa ulikuwa wazi. Uponyaji ilikuwa sehemu kubwa ya huduma Yake.

Mariko 1:40,41 Kisha mtu mwenye ukoma akaja kwake, akinyenyekea, akipiga magoti na kumwambia, "Ikiwa ungependa, unaweza kunifanya safi."

Na Yesu, kwa huruma, akanyosha mkono wake na kumguza, na akamwambia, "Ningependa; na uwe safi."

Uponyaji ilikuwa muhimu kwa Yesu kwa sababu alikuja kufanya mapenzi ya Baba Yake.

Waebrania 10:7 Kisha akasema, 'Tazama, nimekuja-katika nakala ya kitabu imeandikwa juu yangu-kutenda mapenzi Yako, ewe Mungu.'

Wakati Yesu aliwaponya watu, alikuwa akitenda mapenzi ya Baba.

Matayo 9:35 Na Yesu akaenda mijini na vijijini, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri injili ya ufalme, na kuwaponya wagonjwa na wenye maradhi kati yao.

➢ *Roho Mtakatifu*

Uponyaji ni muhimu kwa Roho Mtakatifu na sehemu ya kusudi la upako Wake. Katika Luka, tunasoma jinsi Roho Mtakatifu alimpaka Yesu ili kuwaponya waliovunjika mioyo.

Luka 4:18 "Roho wa Mungu yu juu yangu, kwa kuwa amenipaka kuihubiri injili kwa maskini. Amenituma kuponya waliovunjika mioyo, kuhubiri ukombozi kwa waliofungwa na kuondoa upofu kwa vipofu, kuwafungua wanaoteseka."

Alimpaka Yesu aponye waliopagawa na ibilisi.

Matendo 10:38 ... jinsi Mungu alimpaka mafuta Yesu wa Nazareti kwa nguvu za Roho Mtakatifu, aliyeenda kila mahali akifanya mema na kuponya wote walioteswa na ibilisi, kwa kuwa Mungu alikuwa Naye.

Kukubaliana na Neno la Mungu

Uponyaji ni muhimu kwa sababu ni njia ya Bwana ya kuthibitisha Neno Lake kwa dunia iliyopotea na inayoaga.

Mariko 16:20 Nao wakaenda kila mahali wakihubiri, Bwana akitenda nao na kuhakikisha neno kwa kuambatanisha ishara kati yao. Amina.

Dunia ya leo inaitaji Yesu. Mungu ametuamuru kuenenda kila mahali tukionyesha ishara na kuthihirisha Neno Lake. Kutoa pepo na kuwaponya wagonjwa itasaidia kufungua macho ili waone ukweli wa injili.

Je, Yesu aliteseka bure?

Tusipohudumu uponyaji kwa wagonjwa, basi baadhi ya mapigo ya Yesu mwilini Mwake yalikuwa ya bure.

Isaya 53:5 Alijeruhiwa kwa ajili ya dhambi zetu, akateswa kwa makosa yetu; kichapo kwa ajili ya amani yetu kilikuwa juu Yake, na kwa mapigo yake tumeponywa.

Tunapopuuza kile Neno la Mungu linasema kuhusu uponyaji, tunapuuza neema ya Mungu. Tufanya mapigo – Yesu alipata kuwa yasiyo na maana.

Wagalatia 2:21 Siweki kando neema ya Mungu; kwa kuwa ikiwa haki inatokana na sharia, basi Kristo alikufa bure.

Kuokoa Maisha?

Uponyaji unaweza kuokoa maisha yako, maisha ya watu wa jamii yako, na marafiki. Nabii Hosea aliandika,

Hosea 4:6a Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa.

Uponyaji kwa mwili na nafsi ni msaada Mungu alifanya kwetu. Sisi, kama Daudi, tusiishi sana na kiafya kama mashahidi wa Yesu.

Zaburi 18:17 Sitakufa, bali nitaishi, na kutangaza matendo ya BWANA.

Ufunuo juu ya uponyaji wa Mungu umewaweka wengi kwa kufa mapema.

Yakobo 5:14,15 Je, kuna yeyote miongoni mwenu aliye mgonjwa? Basi awaite wazee wa kanisa wamwombee na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana.

Kule kuomba kwa imani kutamwokoa huyo mgonjwa, naye Bwana atamwinua, na kama ametenda dhambi atasamehewa.

Sehemu ya Agizo Kuu

➢ *Amri kwa Wanafunzi*

Uponyaji ulikuwa sehemu muhimu ya mafundisho na huduma ya wanafunzi wa Yesu na wafuasi wao. Kama vile Yesu alienda akiwaponya waginjwa, aliwaamuru wanafunzi kumi na wawili kufanya hivyo.

Matayo 10:1,7,8 Na alipowaita wale wanafunzi kumi na wawili Kwake, akawapa nguvu juu ya pepo wachafu, kuwakemea, na kuponya magonjwa na maradhi yote.

Na mnapoenda, hubiri, mkisema, 'ufalme wa Mungu uko juu yenu.' Ponya wagonjwa, wasafishe wenye ukoma, fufua wafu, kutoa pepo. Bure mmepewa, bure mpeane

Yesu alisema yeyote anamwaminie atatenda kazi hiyo alitenda Yeye. Uponyaji ni lazima uwe muhimu kwetu ikiwa tutafanya kile Yesu alifanya.

Yohana 14:12 Amini, nawaambia, yeye aniaminiye, matendo ninayotenda naye atafanya; na matendo zaidi ya haya atafanya, kwa sababu naenda kwa Baya Yangu.

Yesu alisema tutahudumu na kufanya miujiza kama vile Yeye alifanya.

➢ *Amri Kwetu*

Kuweka mikono kwa wagonjwa na kuhudumu uponyaji ni sehemu ya Agizo Kuu Yesu alitoa kwa waamini wote,

Yohana 14:15 Ikiwa mwanipenda, fuateni amri zangu.

Yesu alitoa amri hiyo ya mwisho:
Mariko 16:15-18 Naye akawambia, "Enendeni ulimwenguni kote na kutangaza injili kwa kila kiumbe. Yeyote aaminiye na kubatizwa ataokolewa; lakini yeyote anayekataa kuamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini: Katika jina Langu watakemea pepo; watanena katika ndimi tofauti; watachukua nyoka mkononi; na wakinywa sumu, haitawadhuru; watawekelea mikono wagonjwa, nao wataponywa."

Maneno ya mwisho ya Yesu kwa waamini haikuwa mapendekezo. Ilikuwa amri! Kuponya wagonjwa ni muhimu ikiwa tutakuwa watiifu.

CHANZO CHA MAGONJWA

➥ **Je, ugonjwa unatoka kwa Mungu au Shetani?**

Tukiwa na tashwishi kuhusu mambo haya akilini mwetu, tutakuwa na njia mbili akilini, imani ndogo ya uponyaji, tutaishi maisha ya kushindwa. Ili tugundue kwa kweli jinsi ya kushughulikia tatizo la magonjwa, ni sharti tuwe na ufahamu dhabiti kuhusu mwanzo, chanzo, na kusudi.

Ukweli Huleta Uhuru

Tunapogundua ukweli kuhusu chanzo cha magonjwa, maradhi na maumivu, tutawekwa huru ili kupokea na kutoa uponyaji. Ukweli na unapatikana katika utu wa Yesu.

Yohana 14:6 Yesu akamwambia, "Mimi ndimi njia, kweli, na uzima. Hakuna yoyote ajaye kwa Baba ila kwangu Mimi."

Ukweli ulionekana kwa maneno na matendo ya Yesu.

Yesu alisema,
Yohana 8:32 Na mtajua ukweli, nao ukweli utawaweka huru.

Maswali Kuhusu Magonjwa

Kugundua ukweli juu ya chanzo na kusudi la magonjwa, tutaanza kwa kutafuta majibu kwa maswali yaulizwayo sana.

➢ *Je, ni Mapenzi ya Mungu?*

➥ **Je, ni Mapenzi ya Mungu kuwaponya wagonjwa?**

Kizuizi kikubwa zaidi kwa uponyaji ni kutokuwa na hakika juu ya mapenzi ya Mungu kuwaponya wote. Shetani huja dhidi yetu na kuweka maneno yenye utata ndani ya akili zetu, na tusipokuwa waangalifu, tunaweka wasiwasi hiyo katika matendo.

Tunaona haya kayika maneno ya maombi ya kiasili kama vile, "Bwana, kama ni mapenzi yako, tunauliza uponyaji wako ..."

Maombi kama haya huleta kukosa uhakika kama ni mapenzi ya Mungu kwa wote kupata uponyaji. Bila hakika katika roho zetu kuwa ni mapenzi ya Mungu kuponya, ni vigumu kuomba maombi ya imani kwetu na kwa wengine.

Tunaona shaka hii katika mtu mwenye ukoma aliposema, "kiwa unapenda."

Mariko 1:39-41 Naye akawa anahubiri katika masinagogi kote Galilaya, akikemea pepo.

Kisha mtu mwenye ukoma akaja kwake, akinyenyekea, akipiga magoti na kumwambia, "Ikiwa ungependa, unaweza kunifanya safi."

Na Yesu, kwa huruma, akanyosha mkono wake na kumguza, na akamwambia, "Ningependa; na uwe safi."

Yesu alikata ile "kama" kwa kusema, "ningependa" yote Yesu alifanya ilikuwa ufunuo wa mapenzi ya Baba kwa watu Wake.

➥ **Je, ni mapenzi ya Mungu niwe mgonjwa?**

Ni mapenzi ya Mungu juu ya yote kuwa tuishi katika afya nzuri kila siku.

3 Yohana 2 Wapendwa, omba kuwa mfaulu katika mambo yote na muwe na afya, kama vile nafsi zenu hufaulu.

Kama Yesu angeponya wagonjwa, basi ni mapenzi ya Baba kuponya. Kwa sababu ni mapenzi ya Baba kuponya wagonjwa, basi ni mapenzi ya Baba kukuponya!

Kwa Mema yetu?

➥ **Je, magonjwa ni njia moja Mungu hutumia kufanya mambo kwa wema wetu?**

Wengi wamefundisha kuwa magonjwa baadhi ya "mambo yote" Paulo alisema kuwa kufanya pamoja ni kwa ajili ya mazuri yetu.

Warumi 8:28 Na tunajua kuwa mambo yote hufanyika bora kwa wale wampendao Mungu, kwa wale walioitwa kulingana na kusudi Lake.

Katika Habari Njema inasema kwa wazi kuwa,

Tunajua kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi kwa mema ya wale wampendao Yeye, walioitwa katika kusudi Lake.

Ni kutilia mkazo"katika" mambo yote Mungu anafanya kwa mazuri yetu. Si kuwa mambo yote yanafanya kazi kwa mazuri yetu. Bali, "katika yote" au "katika magonjwa," kazi ya Mungu ya uponyaji itakuwa mazuri yatakayotokea.

➢ *Kuteswa kwa Ajili Yake?*

➥ **Je, magonjwa ni mojawapo ya njia tunateswa kwa ajili Yake?**

Wafilipi 1:29 Kwa kuwa, kwenu imetolewa kwa niaba ya Kristo, sio tu kwa kumwamini Yeye, bali pia kuteswa kwa ajili Yake.

Ili kuchunga ufafanuzi wa kinyume, ni bora kuangalia kifungu, hali, ya mada. Katika hali hii, Paulo yuko gerezani akiandika juu ya kufungwa na kuteswa kwa ajili ya injili.

Wafilipi 1:12-14 Lakini nataka mjue kuwa, ndugu zangu, mambo yaliyotendeka kwangu yamegeuka ya kuendeleza injili, na kuwa imefanyika ushahidi kwa walinzi wote katika jumba la kifalme, na kwa wengine, kuwa minyororo yangu iko ndani ya Kristo; na wapendwa wote katika Bwana, kwa kupata ujasiri katika minyororo yangu, nikawa na ujasiri zaidi kunena neno bila uoga.

Ni wazi kutokana na kifungu cha maandiko haya kuwa mateso Paulo anataja hapa haikuwa magonjwa au maradhi. Ilikuwa mateso ya kufungwa kwa ajili ya Injili.

➢ *Kwa Wanafunzi?*

➥ **Je, Mungu huweka magonjwa kwa watu ili kuwakosoa, kuadhibu, au kuwafunza subira?**

Shetani, sio Mungu, ndiye huleta magonjwa na maradhi.

Ayubu 2:7 Kisha Shetani akatoka kwenye uwepo wa BWANA, na kumpiga Ayubu kwa vidonda vibaya kutoka nyayo za miguu yake hadi kichwani.

Hatungemtazamia baba mwenye upendo, kujali kuweka saratani juu ya watoto wake ili kuwapa adhabu. Je,

tunawezaje kuweka picha hii kwa Baba wa mbinguni kuweka magonjwa na maradhi kwa wana Wake?

Yohana 10:10 Mwizi haji ila kuiba, na kuua, na kuharibu. Nimekuja ili wawe na uzima, wawe nao tele.

Yesu alisema ni Shetani ndiye huja kuua, kuiba na kuiba afya yetu, na kutuharibu na magonjwa na maradhi.

Lakini Yesu alikuja kutupatia uhai tele, uhai bila magonjwa, maradhi na maumivu. Alikuja kurejesha kwetu yote Aliyoumba mwanadamu awe nayo alipomuumba Adamu na Eva katika mfano Wake.

➢ *Je, vipi Juu ya Mwiba wa Paulo?*

➥ **Je, Biblia inasema kuwa mwiba wa Paulo ulikuwa ugonjwa?**

Kwa kutokuelewa Maandiko, wengine wamefundisha kuwa mwiba wa mtume Paulo ilikuwa ugonjwa wa macho. Lakini, Paulo aliandika kuwa mwiba wako ulikuwa pepo aliyetumwa na Shetani kumtesa na kuleta usumbuvu.

2 Wakorintho 12:7 Na wala nisiinuliwe kuliko kiasi kwa ajili ya ufunuo tele, mwiba niliowekewa mwilini mwangu, mtumwa wa Shetani kunitesa, nisije nikainuliwa kupita kiasi.

Hakuna mahali ambapo Biblia inasema mwiba wa Paulo ulikuwa ugonjwa wa kimwili.

➢ *Inaweza Kuleta Mauti?*

➥ **Mungu akiwa tayari kutuchukua nyumbani ni lazima tuwe wagonjwa ili tufe?**

Ni mapenzi ya Mungu kuwa tuishi katika afya nzuri kila siku, kwa nini iwe sawa kwake kuwa tuwe wagonjwa na kufa?

Musa ni mfano mzuri! Alikuwa miaka mia ishirini alipoitwa na Mungu nyumbani. Afya yake ilikuwa nzuri angeweza kuukwea mlima kukutana na Mungu. Hakupoteza macho yake na alikuwa na nguvu zake.

Kumbukumbu 34:7 Musa alikuwa miaka mia ishirini alipokufa. Macho yake yalikuwa sawa wala nguvu zake kumwishia.

Mtu mzima anapokuwa mgonjwa, ni mapenzi ya Mungu kuwa apate uponyaji. Wakati wa Mungu ufikapo, roho zao hutoka na mioyo huacha kupiga.

➢ *Je, Mungu husababisha itendeke?*

➥ **Je, Mungu "huacha" magonjwa au kifo cha mapema kije kwa watu Wake?**

Wengi humlaumu Mungu magonjwa au kifo kinapokuja, wakisema "Mbona Mungu alikubali haya yafanyike?"

Adamu na Eva walipewa nguvu na mamlaka juu ya yote yanafanyikapo hapa duniani walipoumbwa katima mfano wa Mungu.

Mwanzo 1:26a Kisha Mungu akasema, "Hebu na tuumbe mwanadamu kwa mfano wetu, kulingana na sura Yetu; hebu na wawe na utawala."

Nguvu au mamlaka yaliyopotea wakati Adamu na Eva kutenda dhambi, ilirejeshwa na Yesu.

Matayo 16:19 Nami nitawapa funguo za ufalme wa mbinguni, na chochote mtakachofunga duniani kitafungwa mbinguni, na chochote mtafungua duniani kitafunguliwa mbinguni.

Magonjwa huja katika nguvu za Shetani, lakini Yesu alisema kuwa waamini leo wanazo nguvu (au mamlaka) juu ya nguvu za adui.

Luka 10:19 "Tazama, nawapa mamlaka kuwakanyaga nyoka na nge, na juu ya mamlaka ya adui, na hakuna kitakachowadhuru."

Kwa kukosa kutumia mamlaka ya Mungu hapa duniani, sisi, si Mungu, tunamwachilia shetani kuleta magonjwa, maradhi na mauti kwetu na wapendwa wetu.

Chanzo cha Magonjwa

Magonjwa yote na maradhi yanatoka kwa Shetani na si Mungu. Wengi ni wagonjwa kwa sababu wametoa roho zao kwa kupagawa katika dhambi, kutokutii, au kwa kudharau kanuni za afya nzuri na lishe.

Waefeso 4:27 Wala kutoa nafasi kwa ibilisi

Kwa kutumia uwezo wetu uliorejeshwa, tunaweza kumkemea ibilisi, roho za kupagawa, au magonjwa na yatatoroka kutoka kwetu.

Yakobo 4:7b ... Mkinge Shetani naye atatoroka.

Waamini wana uwezo kukemea roho wa kupagawa, na kuponya maradhi na magonjwa ya aina yote.

Matayo 10:1 Na alipowaita wale wanafunzi kumi na wawili Kwake, akawapa nguvu juu ya pepo wachafu, kuwakemea, na kuponya magonjwa na maradhi yote.

Kile tu ibilisi anaweza kufanya maishani mwetu leo ni kile tumemruhusu afanye. Shali lisiwe, "kwa nini Mungu anakubali haya yafanyike?" bali liwe, "kwa nini tunaachilia haya yafanyike?"

Kumbuka: Ili kuelewa swali hili, soma kitabu, Mamlaka ya Mwamini na A.L. Gill na kitabu chake, Kuytengwa ili Kutawala.

SHETANI HUTUMIA MAGONJWA KAMA SILAHA YA KUTUSHINDA

Kuanguka kwa Shetani

Shetani na malaika wake walirushwa chini duniani baada ya kuasi mbinguni. Tunasoma maelezo,

Ufunuo 12:7-10 Na kukawa vita mbinguni: Mikaili na malaika wake wakapigana na joka; na joka na malaika zake wakapigana lakini hawakufaulu, wala hapakuwa na nafasi mbinguni tena.

Kwa hivyo yule joka mkuu akatupwa nje, nyoka wa zamani, aliyeitwa Ibilisi na shetani, anayehadaa ulimwengu wote; alitupwa duniani, na malaika zake walitupwa pamoja naye.

Kisha nikasikia sauti kubwa ikisema kutoka mbinguni, "Sasa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu, na nguvu ya Kristo imewadia, kwa kuwa msaliti wa wapendwa, aliyewasaliti mbele za Mungu kila siku, ametupwa chini."

Mwanadamu kwa Mfano wa Mungu

Mungu alimwumba mwanadamu kwa mfano Wake kwa ile nyota Setani alirushwa baada ya kuasi. Aliwaumba wawe na utawala juu ya ardhi ambayo Shetani alitawala hadi nyakati hizo.

Mwanzo 1:26,28 Kisha Mungu akasema, "Natuumbe mwanadamu kwa mfano wetu; na watawale juu ya samaki majini, ndege angani, na juu ya ng'ombe, juu ya nchi yote na juu ya kila kiumbe atambaaye ardhini."

Kisha Mungu akawabariki, na Mungu akawambia, "zaeni na kuzidisha; jaza ulimwengu na kutawala; tawala juu ya samaki wa majini na ndege wa angani, juu ya viumbe walio hai na wanaotembea juu ya nchi."

➥ **Mwanadamu aliumbwa ili:**

- ➢ Kuonekana kama Mungu
- ➢ Kutembea kama Mungu
- ➢ Kunena kama Mungu
- ➢ Na kuwa na utawala hapa duniani!

Shetani ana chuki Nawe

Shetani alirushwa hapa duniani toka mbinguni, akiwa na chuki dhidi ya Mungu, yule aliyetaka kuwa kama Mungu, lazima alikasirika akimtazama Mungu akiwaumba wanadamu kwa mfano wake. Kisha Mungu akawapa mamlaka juu ya kila kitu alichotawala!

Kila mara Shetani anapomwona mume au mke, lazima anakumbushwa juu ya Mungu – sababu ya hasira yake kuu. Anapowaona wanadamu wakionekana na kutenda kama

Mungu, chuki inapanda. Kuonyesha chuki hiyo ni kuiba, kuua na kuharibu.

Mtume Yohana aliandika,
Yohana 10:10a Mwizi haji ila kuiba, kuua, na kuharibu.

Satan knows that we are God's representatives on earth. We are the body of Christ, and his greatest desire is to defeat us.

➢ *Mwanadamu kama chambo cha Shetani*

Hasara, mauti, na uharibifu kila mara ni kazi ya Shetani. Kwa miaka elfu nne baada ya kuanguka kwa Adamu na Eva, mwanadamu aliishi chini ya utumwa, kufungwa, na kuteswa.

- ➢ Wanadamu walioumbwa kutembea katika mamlaka, walemaa na kuwa vipofu, wakiketi kando ya njia, wakiomba
- ➢ Mwanamke aliyeumbwa kutembea wima, alilemaa na kuinama kwa maumivu na mashaka.
- ➢ Waume kwa wake waliumbwa kuwa kama Mungu (kwa mfano Wake), sasa nyuzo zao zikaliwa na ukoma.

➥ **Yesu alikuja kumweka manadamu huru kutoka utumwani, kufungwa na kuteswa katika maradhi, magonjwa na maumivu.**

Mungu anataka tuwekwe huru kutokana na mateso ya Shetani. Anataka tuachiliwe kutoka ngome ya dhambi. Mungu anataka tuwe bora!

Chanzo cha magonjwa na maradhi ni Shetani – sio Mungu!

MASWALI YA KUSAIDIA KUJIFUNZA

1. Je, kwa nini ni muhimu kwa Mungu kuwa upokee uponyaji wako na kuhudumia wengine uponyaji?

2. Je, Mungu, kama Baba anayekupenda, anaweza kuweka magonjwa juu yako kama mwana Wake? Eleza ukitumia Maandiko.

3. kama ungekuwa Shetani na ungetaka kuonyesha hasira yako kwa Mungu kwa kuwapinga wanadamu, taja vitu vitatu ungefanya.

4. Yesu alikuja kutuweka huru. Je, unaweza kutoa sababu kuonyesha kwa nini uendelee kuishi na magonjwa mwilini mwako?

Somo la Pili

Uponyaji katika Ukombozi wetu

Hakuna ukweli ambao Shetani amejaribu kuwaficha Wakristo zaidi ya kuwa Yesu alileta uponyaji wetu katika kuteswa kwake, mauti na ufufuo! Tunaelewa kuwa ametuletea wokovu wetu, lakini hudhani uponyaji ni kitendo kigeni kwa wachache – au ililetwa kwa kizazi maalum.

Tumekubali ukweli kuwa "aliteswa kwa ajili ya dhambi zetu" lakini tumepuuza kweli kuwa "kwa mapigo Yake tumeponywa." Hata kama maneno haya yanapatikana msitari mmoja.

Isaya 53:5 Alijeruhiwa kwa ajili ya dhambi zetu, akateswa kwa makosa yetu; kichapo kwa ajili ya amani yetu kilikuwa juu Yake, na kwa mapigo yake tumeponywa.

Mungu anayo agano nasi na hii inajumlisha uponyaji!

MAAGANO NA MUNGU

Maomo ya kutumia ishara katima Neno la Mungu, inatuma mtazamo wa ndani katika mpango wa Mungu. Katika Agano la Kale tunaona Mtu na kazi ya Yesu Kristo kama ilivyotimika katika Agano Jipya. Ukombozi kutoka Misri na wana wa Israeli wakivuka Bahari ya Shama ni mfano wetu kukombolewa kutoka ngome ya dhambi.

Agano

➥ **Agano ni ahadi kubwa ya kujitolea na makubaliano ya kushikanisha kati ya makundi mawili, watu, au katika masomo haya kati ya Mungu na watu Wake.**

Punde tu Israeli alipovuka Bahari ya Shama, Mungu alifanya agano la uponyaji na kujitokeza Mwenyewe kama Mponyaji.

Kutoka 15:26 Na kusema, Ikiwa utaisikia sauti ya BWANA Mungu wako na utende haki machoni mwako, uzisikie amri zake na kuyafuata maagizo Yake, sitaweka ugonjwa wowote juu yako ambao nimeleta juu ya Wamisri. Kwa kuwa Mimi ndimi BWANA nikuponyaye."

Kiebrania, jina, Yehova-Rafa, ilitumika maana yake Mimi ndimi Bwana mponyaji wako, au mimi ni Bwana nikuponyaye.

Majina ya Agono ya Mungu

Yehova ni jina la Mungu la ukombozi na lina maana: Yule Aishiye na anayejitokeza Mwenyewe.

Yehova anayo majina saba ya ukombozi ambayo yanamwuonyesha yeye kama anayekutana na mahitaji ya Agano kwa watu wake.

➢ *Yehova-Shammah*

➥ **Bwana yu pale.**

Ezekieli 48:35b ... na jina la mji kutoka siku hiyo litakuwa: BWANA Yu Pale.

➢ *Yehova-Shalom*

➥ **Bwana ni Amani.**

Waamuzi 6:23,24a Kisha BWANA akamwambia, "Amani iwe kwenu; usiogope, hutakufa."

Kwa hiyo Gidion akamjengea BWANA madhabahu pale, na kupaita Bwana Shalomu (Amani).

➢ *Yehova-Raah*

➥ **Bwana ni Mchungaji Wangu.**

Zaburi 23:1 Bwana ni mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu.

➢ *Yehova-Jaira*

➥ **Bwana Ataleta.**

Mwanzo 22:13,14 Kisha Ibrahimu akainua macho yake na kutazama, na haponyuma yake palikuwa na kondoo amenaswa kati ya kichaka kwa pembe zake. Ibrahimu akamchukua kondoo, na kumtoa kama dhabihu wa kuchoma badala ya mwanawe. kisha Ibrahimu akaita mahali pale, Bwana-ataleta; kama ilivyo hata sasa, "Katika mlima wa BWANA itapatikana."

➢ *Yehova-Nissi*

➥ **Bwana ni Mlinzi wetu, Mshindi au Nahodha.**

Kutoka 17:12,13,15 Lakini mikono ya Musa ikawa mizito; nao wakalichukuwa jiwe na kuweka chini yake, naye akalikalia. Nao Haruni na Huri wakamsaidia mikono yake, mmoja kila upande; na mikono yake ikawa imara hadi kutua jua. Kwa hiyo Yoshua akawashinda Wamaleki na watu wake kwa ya upanga.

Naye Musa akajenga dhabihu na kuita jina, Bwana-ni-Bendera-Yangu

➢ *Yehova-Tsidkenu*

➥ **Bwana Haki Yetu.**

Yeremia 23:6 Katika siku Zake, Yuda ataokolewa, naye Israeli atakaa salama; hili ndilo jina Lake ambalo ataitwa: BWANA HAKI YETU

➢ *Yehova-Rapha*

➥ **Mimi Ndimi Bwana Mponyaji wako, au Mimi ndimi Bwana Akuponyaye.**

Kutoka 15:26b Maana Mimi ni BWANA Akuponyaye.

Hakuna mahali popote katika Neno ambapo tunaona Mungu akikana agano hili. Hakuna mahali ambapo tunaona amefanyika "Nilikuwa Bwana Mponyaji Wako" au Nilikuwa Bwana niliyewaponya." Hakuna mahali ambapo Mungu anasema, "Mimi ndimi Mungu wako anayekuletea magonjwa."

Mungu habadiliki. Yeye ni yule jana, leo na milele, na bado Yeye ni Mponyaji wetu!

Ahadi ya Agano ya Uponyaji

Yehovah-Rapha ni ufunuo wa ahadi ya agano ya Mungu kuleta uponyaji kwa watu Wake.

Kulingana na Daudi, ufunuo wa Mungu kama Yehova-Rapha ilikubalika na kuaminika na Waisraeli, na watu wote wakafurahia afya.

Zaburi 105:37b Hapakuwa na mtu yeyote mnyonge kati ya makabila yao.

Israeli ilipotenda dhambi na afya yao kudhoofika, walitubu, dhabihu ya Walawi ilifanywa, na Mungu aliendelea kuwa Yehova-Rapha kwa wote. Leo, tunapohubiri Injili ya kukombolewa na kurejeshwa katika Yesu Kristo, tunayo ahadi hiyo kwa wagonjwa.

TAARIFA YA ISAYA – MKOMBOZI MPONYAJI

Kwa mamia ya miaka, wasomi wa Kiebrania wasioamini walijaribu kueleza kuwa Isaya hamsini na tatu haikuwa sehemu ya Maandiko ya Wayahudi ya asili. Lakini wakati nakala hizi zilipatikanat Quram mwaka 1947, kitabu cha Isaya ndicho kilipatikana kamilifu mwanzo hadi mwisho. Ilikuwa na unabii kamili wa Yesu katika sura ya hamsini na tatu.

Je, Nani Ataamini?

Isaya aliandika,
Isaya 53:1a ... Na ni nani aliyeamini taarifa yetu?

"Nani aliyeamini taarifa yetu" tunapojifunza taarifa hii, tunao uamuzi. Tunaweza kuamini taarifa hii, au tuwe na tashwishi juu ya taarifa na kuwa bila matokeo bora.

Je, Mungu ni mwenye Nguvu kiasi gani?

Isaya 53:1b ... na ni kwa nani mkono wa BWANA umeonekana?

Wanaoamini ripoti watakuwa wale mkono wa BWANA utawaonekania. Mkono wa BWANA maana yake nguvu Zake kuu.

Tujiulize swali, "Je, Mungu wangu ana nguvu kiasi gani?"

Isaya alitueleza nguvu za Mungu.

Isaya 45:12 Nimeumba dunia, na kumwumba mwanadamu. Nilikuwa mimi mikono yangu iliyonyoshwa toka mbinguni, na jeshi lote nimeliamuru.

Baadaye, Isaya aliandika kuhusu mkono na sikio la Mungu.

Isaya 59:1 Tazama, mkono wa Bwana si mfupi, kwamba usiokoe; na sikio Lake si nzito lisisikie.

Mungu ni mwenye nguvu! Kwa mikono yake Alinyosha na kuivuta mbingu. Yesu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, alinyosha mkono Wake na kuwaponya wagonjwa. Mkono Wake umedhihirishwa na si mfupi kuwa usiweze kuokoa na kuponya leo.

Ufunuo

Wanaoamini watapokea ufunuo kamili wa taarifa hii. Watagundua kuwa msaada wa Mungu kwa uponyaji ni sehemu ya kazi ya ukombozi wa Yesu kwa ajili yao, kama msaada wa wokovu.

Ufahamu huu wa ndani unatokana na ufunuo usio wa kawaida – kutambua kwa ghafla ukweli wa Mungu ndani ya roho zetu. Ufunuo hauji kwa nguvu za kuwaza kimaarifa. Ngundua neno "kufunuliwa"

Isaya 53:1b ... ni kwa nani mkono wa BWANA umefunuliwa?

"Logos" ni neno la Kigriki maana yak e Neno la Mungu lililoandikwa. Mungu aletapo ufunuo wa sehemu ya Neno Lake kwetu, inafanyika rema. "Rhema" ni neno la Kigriki maana yake Neno la kibinafsi la Mungu, au ufunuo, kunenwa katika nafsi zetu na Roho Mtakatifu.

Mara nyingi tunaposoma na kutafakari juu ya Neno la Mungu, "nuru itawaka," ghafla tutapata ufahamu wa kweli. Tunaweza kupiga ukulele "Ajabu! Mungu ameweka msitari mpya katika Biblia yangu! Hili ni jibu nimekuwa nikitafuta. Sijaliona hivi awali!"

Mungu amedhihirisha ukweli fulani rohoni mwetu. Logos imefanyika rhema kibinafsi kwetu. Wakati huo, imani inaingia katika roho zetu, na imani hiyo inaturuhusu kupokea uponyaji Yesu ametoa kwetu.

Warumi 10:17 Kwa hivyo Imani huja kwa kusikia, na kusikia Neno (rhema) la Mungu.

Kuirejelea ripoti ya Isaya,
Isaya 53:3-7 Amedharauliwa na kukataliwa na watu, mtu wa mateso mengi. Nasi tukafanya, jinsi ilivyokuwa, nyuso zetu kutoka Kwake; alionyeshwa madharau, na wala hatukumheshimu.

Hakika Amefanya

Kwa kweli alibeba mateso yetu; nasi tulimheshimu Yeye, aliyepigwa na Mungu, na kuteswa. Lakini alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu, alipigwa kwa ajili ya dhambi zetu; mapigo juu yake ilikuwa yetu, na kwa mapigo Yake tumeponywa.

Msitari wan ne unaanza na neno "hakika" je, hakika ina maana gani? Katika kamusi:

- ➢ Na hakikisho au ujasiri,
- ➢ Bila kusita sita,
- ➢ Bila tashwishi,
- ➢ Bila swali,
- ➢ Kwa hakika,
- ➢ Hutumika kutilia mkazo kuamini.

Kuteseka kwa Ajili ya Yesu

Biblia inatueleza ufahamu kamili wa kifungu hiki.

Isaya 53:4,5 Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu, amepigwa sana naye na kuteswa. Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona.

Isaya aliandika, "Hakika, amebeba magonjwa yetu, unyonge, na mahangaiko, na kuchukua mateso na maumivu yetu." Mistari hii michache inatuletea ujasiri na na hakikisho. Kama vile Yesu alichukua dhambi zetu ili tusibebe sisi, alichukua pia magonjwa, maradhi na mateso ili tusibebe tena kamwe.

Je, ripoti ya Isaya ni ipi? Yesu aliteseka kwa nini?

- ➢ Huzuni zetu – magonjwa, unyonge, mahangaiko
- ➢ Mateso yetu – maumivu
- ➢ Dhambi zetu
- ➢ Dhambi zetu na hukumu
- ➢ Amani na wema wetu
- ➢ Uponyaji na kufanywa wazima

Tunaweza kusema, kwa ujasiri, "Hakina, kwa mapigo aliyopata mwilini mwake, tumepona!"

Kwa hakika jinsi tunajua amezichukua dhambi zetu ili tusibebe sisi tena, tunaweza kujua pia kuwa ametuondolea magonjwa yetu na maumivu.

Yesu Badala Yetu

Katika kazi ya ukombozi ya Yesu kwa niaba yetu, Yeye alifanyika kwa niaba yetu. Alichukua nafasi yetu. Kama mbadala, Yeye hakuchukua tu dhambi zetu, pia alichukua mshahara wa dhambi.

I Petro 2:24 Ambaye mwenyewe alizibeba dhambi zetu mwilini mwake juu ya mti, ili sisi, baada ya kufa kwa dhambi, tuweze kuishi kwa haki – kwa mapigo yake tumeponywa.

Kabla Yesu kutundikwa msalabani, alipigwa.

Matayo 27:26b ... na alipompiga Yesu, alimtoa ili asulubiwe.

Kwa maumivu na kipigo alichopata mwili wake ulikatika kutoka mgongoni, akafanyika kwa niaba yetu. Alichukua maumivu ya magonjwa na maradhi.

Kazi yake ya ukombozi kwa niaba yetu haikulipia tu adhabu ya dhambi zetu, bali pia ilituweka huru kwa kubeba mshahara wa dhambi.

Uponyaji – Sehemu ya Ukombozi

➥ **Ufunuo kamili wa Ukombozi unatoa:**

- ➢ Wokovu wa milele katika Yesu kama mwokozi wetu.
- ➢ Uponyaji wa mili yetu kwa imani katika Yesu kama mponyaji weu.

Ni muhimu kwa Wakristo kujua kuwa uponyaji ni sehemu ya ukombozi wa Mungu kwa wanadamu walioasi. Wakati Yesu alikuja duniani na kulipa gharama ya dhambi zetu, pia alilipa gharama ya uponyaji. Ni mpango wa Mungu wanadamu wafurahie afya kamili – kimawazo, kimwili, na hisia.

Ili tuweze kupata manufaa ya msaada huu, ni bora tuzitambue na kupokea kwa imani katika Neno la Mungu.

IMANI DHIDI YA HISIA

Kuzitegemea Hisia

Mojawapo ya pingamizi katika kupokea uponyaji ni kutegemea hisia. Ingawa inaachilia imani yetu tunapoona mtu akiponywa, msingi wa imani ya kuponywa sharti uwe Neno la Mungu!

Kurejea Isaya,
Isaya 53:1b Je, nani amesadiki taarifa yetu?

Ni swali tunaitajika kujibu sisi wenyewe. Je, ninaamini Neno la Mungu?

➥ **Ninao uamuzi kufanya.**

- ➢ Je, nitaamini ripoti ya daktari? Je, nitaamini ripoti ya Mungu?
- ➢ Je, nitaamini tamaduni zangu? Je, nitaamini kile Mungu amenena na kunifunulia katika roho yangu?

Tunapopokea neno la rhema kutoka kwa Mungu, imani huingia katika roho zetu. Kinyume na ripoti ya daktari, tamaduni, au ustadi wa awali, imani imekuja na imani huamini ripoti ya Mungu.

Katika Maelezo yafuatayo, utaona tofauti kati ya imani katika hisia na imani katika Neno la Mungu.

Uponyaji Kupitia Imani

Uponyaji ni kwa imani. Tunaponywa tunapojifunza, kuamini, naps through faith. We are healed as we learn, believe, and then act on the Word of God.

Paulo aliandika,
Warumi 3:3,4a Basi itakuwaje wengine wakikosa kuamini? Je, kutokuamini kwao kutafanya uaminifu wa Mungu uwe bila mafanikio? Hakika hapana! Kweli, na Mungu awe wa kweli mwanadamu mwongo.

Mungu ni mwaminifu. Yeye yu tayari kutimiza ahadi yake ya uponyaji. Kile tunaitajika kufanya ili kupokea uponyaji ni kuamini!

- ➢ "Kwa majeraha Yake tumepona!"
- ➢ "kwa majeraha Yake tumeponywa!"

➢ *Nimeokoka kwa sababu Mungu anasema hivyo!*

"Wakati mwingine sijisikii nimeokoka – lakini najua hivyo kwa sababu ninaamini ujumbe wa Mungu."

1 Yohana 5:13a Mambo haya nimewaandakia ninyi mnaoamini katika jina la Mwana wa Mungu, ili mjue kuwa mnao uzima wa milele.

➢ *Nimeponywa kwa maan Mungu amesema hivyo!*

"Wakati mwingine sijisikii nimeponywa – lakini najua hivyo kwa maana naamini ujumbe wa mungu."

Isaya 53:5 Alijeruhiwa kwa ajili ya dhambi zetu, akateswa kwa makosa yetu; kichapo kwa ajili ya amani yetu kilikuwa juu Yake, na kwa mapigo yake tumeponywa.

Ni lazima tupokee kile ambacho kwa haki ni chetu, bila kujali hisia au kuona kwetu. Tusiruhusu shaka za wengine kuiba uponyaji wetu.

Wengine huuliza,

➢ "Kwa nini, ikiwa ni mapenzi ya Mungu kuwa wote wapone, si basi wote wameponywa?"

Pia tunaweza kuuliza,

➢ "Kwa nini, ikiwa ni mapenzi ya Mungu wote waokolewe, basi si wote wameokolewa?"

Jibu kwa maswali haya mawili ni,

➢ Ni lazima waamini.

Tunapokea wokovu kwa imani katika Neno la Mungu. Pia tunapokea uponyaji kwa imani katika Neno la Mungu.

MITUME WALIAMINI – SEHEMU YA UPONYAJI YA UKOMBOZI

Ni wazi kutokana na vitendo kuwa mitume waliamini kuwa uponyaji ulikuwa sehemu ya ukombozi wao walipowaponya wagonjwa na kuandika taarifa ya kusisimua.

Matayo Aliamini

Matayo aliamini ripoti ya Mungu jinsi ilivyotabiriwa na Isaya.

Matayo 8:16,17 Jioni ilipofika, walimletea watu wengi wenye pepo. Naye akawakemea pepo kwa neno, na kuponya wote waliokuwa wagonjwa, ili yatimizwe aliyonena Isaya akisema, "Yeye mwenyewe aliyachukua maradhi yetu na kubeba magonjwa yetu."

Isaya 53:4 inaweza tu kutimizwa katika kazi ya Yesu akiwaponya wote, na "wote" inajumlisha kila mmoja wetu leo.

Petro Aliamini

Petro alimwamini ripoti ya Mungu kama alivyotabiri Isaya.

I Petro 2:24 Ambaye mwenyewe alizibeba dhambi zetu mwilini mwake juu ya mti, ili sisi, baada ya kufa kwa dhambi, tuweze kuishi kwa haki – kwa mapigo yake tumeponywa.

Petro aliamini ripoti ya Mungu alipomponya mtu wa kwanza kufuatia kuondoka kwa Yesu hapa duniani.

Matendo 3:6,7 Kisha Petro akasema, "Fedha na dhahabu sina, lakini kile nilicho nacho nakupa: katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti, inuka na utembee."

Kama mtu kilema, nasi pia sharti tuamini Neno la Mungu ni kweli.

Neno la Mungu

➢ *Ni Hakika sana*

Petro hakuamini tu ujumbe wa Mungu, alijua kuwa Neno la Mungu ni hakika sana kuliko chochote angeona au kutaja.

2 Petro 1:19a Nasi tunalo Neno la kinabii la hakikisho ...

➢ *Linadumu milele*

Petro alijua kuwa Neno la Mungu linadumu. Ni hai na lafaa maishani mwetu sasa.

1 Petro 1:23 kwa kuwa tumezaliwa mara ya pili, sio kwa mbegu ya ufisadi bali isiyo ya ufisadi, katika neno la Mungu ambalo linaishi na kukaa ndani yetu milele.

Ninaamini

Ni wazi kwetu tunapoona katika Neno:

- ➢ Ikiwa tutaponywa kulingana na 1 Petro 2:24,
- ➢ Ikiwa tutaponywa kulingana na Isaya 53:5,
- ➢ Basi nimeponywa!

Kilicho cha muhimu ni kuamini ripoti Yake Mungu! Hata kama tamaduni zangu, viongozi wa kidini, mtazamo wangu, au ninavyohisi ni tofauti!

- ➢ Ni lazima nipokee uponyaji wangu kwa imani.
- ➢ Ni lazima nianze kunena na kutenda imani yangu!
- ➢ Wakati imani yangu inajengeka, nitaachilia imani hiyo, kwa ujasiri nianze kutenda imani yangu, na nipokee uponyaji wangu.
- ➢ Kama yule kilema, dalili zangu zitatoweka, aidha polepole au ghafla. Name pia, nitatembea na kuruka nikimsifu Mungu.

Je, Utaamini?

Je, utaamini ripoti yake Isaya?

Sasa ni wakati wa kupokea kutoka kwa Mungu. Unaweza kupokea uponyaji wako sasa hivi!

Tumeona kutoka kwa mojawapo ya majina ya Mungu – Yehova-Rapha, kwa kuteswa kwa Yesu kwa niaba yetu, katika unabii wa Isaya, na katika shuhuda za mitume kuwa uponyaji ni sehemu muhimu katika mpango wa Mungu maishani mwetu.

➥ **Bila kujali hisia katika miili yetu, Neno la Mungu linatangaza, "kwa mapigo Yake tumeponywa!"**

Mara tu ufunuo huu unapoingia katika roho yako, imani ya kupokea uponyaji wako itafika. Kwa ujasiri tangaza "Kwa mapigo yake nimepona!" kwa matarajio anza kutazama mwili wako. Fanya kile hungefanya awali. Nenda katika hatua ya ujasiri na uanze kumsifu Mungu kwa uponyaji wako!

Kumbuka: ufunuo unaoelezwa hapa haizingatii aina ya dalili miilini mwetu – Neno la Mungu linasema tuliponywa zaidi ya miaka elf mbili iliyopita. Badala ya kuponywa sasa, au baadaye siku za usoni, ukweli ni kwamba uponyaji wetu unadhihirishwa katika mili yetu. Katika masomo haya tunatumia maneno "kuonekana kwa uponyaji wetu."

Dhihirisho inaweza kuelezwa maka "wazi machoni na akilini, au kuonekana wazi."

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, agano gani Mungu ameweka na watu Wake kuhusu uponyaji? Kwa nini ni muhimu?

2. Eleza ufunuo wa uponyaji katika Isaya 53 kwa maneno yako mwenyewe.

3. Je, ni hatua gani unaamini Mungu angependa uchukue ikiwa dalili mwilini mwako hazikubaliani na ufunuo wa kweli kama inavyoonyesha katika Neno la Mungu?

Somo la Tatu

Yesu – Mfano Wetu

Alikuja kama Mwanadamu

Ni muhimu kuelewa kuwa Yesu aliweka kando haki zake kwa muda kama Mungu alipokuja duniani. Alikuja kama Adamu wa mwisho, mwana wa Adamu. Yote aliyofanya hapa duniani, alifanya kama vile Adamu wa kwanza alivyoumbwa afanye. Yesu alitenda katika vipawa vya Roho Mtakatifu kama vile waamini wanaitajika kufanya leo.

Mtume Paulo aliandika juu kuja kwa Yesu kama mwanadamu.

Wafilipi 2:7 Lakini Yeye mwenyewe akashushwa cheo akawa mtumishi, na kuja katika umbo la mwanadamu.

MIUJIZA YA KWANZA YA YESU

Kuyageuza Maji kuwa Divai

➥ **Chochote asemacho Tenda!**

Muujiza wa kwanza aliofanya Yesu ilikuwa kugeuza maji kuwa divai katika karamu ya harusi. Baada ya Maria, mamake Yesu, kumwambia kuwa hawana divai, alinena maneno ya muhimu kwa watumishi,

Yohana 2:5b Chochote asemacho kwenu, tendeni.

Ili kuona miujiza ya Yesu maishani mwetu, ni lazima tusikie na kutii sauti ya Mungu bila kujali upumbavu unaonekana. “Chochote asemacho, tendeni!” hii huachilia Roho Mtakatifu kutenda kazi ndani yetu.

Watumishi wamtii Yesu; walijaza mitungi maji. Waliendelea kumtii, kwa kuleta maji kwa mkuu wa karamu. Mkuu wa karamu alipoionja alisema, “umeweka divai tamu hadi sasa.”

Je, ingekuwa rahisi sana wao kushuku walipoambia wachote na kupeleka maji, kwa msimamizi wa karamu. Watumishi hawakuanza tu kumtii, waliendelea kufanya hivyo ilikuwa vigumu!

Ili kuona miujiza maishani mwetu, nasi ni lazima tuseme, chochote aniambiacho, nitatenda!”

Kumponya Mwana wa Afisa wa Kifalme

➥ **Mwujiza wa Yesu wa Uponyaji ulikuwa wa pili!**

Afisa wa kifalme akasikia juu ya mwujiza Yesu alifanya harusini na kusikia kukaleta imani. Matokea ya imani hiyo, mwanawe aliyekuwa nusu hai akapona.

Yohana 4:46-51 kwa hiyo Yesu akaja tena Cana ya Galilaya mahali alipokuwa amegeuza maji divai. Na hapo palikuwa mtu mmoja afisa mkuu ambaye mwanawe alikuwa mgonjwa Kapenaumu. Aliposikia kuwa Yesu amefika kutoka Yudea hadi Galilaya, alimwendea na kumsihi aje na kumponya mwanawe, kwa kuwa alikaribia kufa.

Kisha Yesu akamwambia, "Ninyi watu msipoona ishara na miujiza, hamtaamini kamwe."

Yule mtu wa cheo akasema, "Bwana, njoo kabla mwanangu hajafa!"

Yesu akamwambia, "Nenda zako, mwanao yuwaishi."

Basi yule mtu akaamini neno Yesu alimwambia, kisha akaenda zake. Na alipokuwa anaenda, watumishi wake wakakutana naye na kumwambia, wakisema, "Mwanao yuwaishi!"

Yule mtu hakufanikiwa kumsihi Yesu amponye mwanawe jinsi alitaka. Alimwomba aje na kumponya mwanawe. Lakini, mtu huyo alipokea mwujiza wake wa uponyaji alipoamini neno ambalo Yesu alinena!

Wengi wameshindwa kupokea miujiza kwa sababu wamemsihi Yesu awafanyie jinsi wanataka. Wanaamini watapona ikiwa mtu fulani atawaombea kwa njia fulani badala ya kuweka imani yao kwa Mungu na Neno Lake.

Kama watumishi na yule mtu wa cheo, sisi pia, tunaweza kuona miujiza ikiwa tutaisikia sauti ya Yesu, kuamini neno analosema, na kutii chochote anatuambia kufanya.

YESU ALIKUJA ILI

Kuweka Huru!

Yesu alipakwa na Roho Mtakatifu kuhubiri ukombozi kwa wafungwa na kuweka huru walioteswa. Ngome zote, na pia za magonjwa na maradhi, hayawezi kamwe kuwa mapenzi ya Mungu, kwa maana upako wa Roho Mtakatifu ulikuwa kuponya na kuweka huru.

Luka 4:18 "Roho wa Mungu yu juu yangu, kwa kuwa amenipaka kuhubiri injili kwa maskini. Amenituma kuponya waliovunjika mioyo, kuhubiri ukombozi na kuondoa upofu, kuwafungua wanaoteseka."

Kuvunja kila ya Nira

Isaya alitabiri kuhusu huduma ya Yesu kuwa ataweka huru wanaoteswa.

Isaya 58:6 je, hii si ya kwanza niliyochagua:
– kufungua ngome ya unyonge,
– kuondoa mizingo mizito,
– kuwaachilia wanaoteswa kuwa huru
– na kuwa uvunje kila nira?

Kuziharibu kazi za Shetani

Kulingana ya Yohana, sababu ya kuja kwa Yesu ilikuwa,

1 Yohana 3:8b ... ili aziharibu kazi za ibilisi.

Kutoa Uhai Kamili

Kwa kuharibu kazi za ibilisi, Yesu anatoa maisha tele kwa watu Wake. Yesu alisema,

Yohana 10:10b Nimekuja ili wapate uzima, na kuwa wawe nao tele tele.

Kuwaponya Wote

Maandiko yanayotilia mkazo huduma ya Yesu ya uponyaji ni kuwa Aliwaponya wote waliokuja kwake.

Katika Biblia kuna misamiati fulani inayoeleza wokovu na uponyaji. Maneno yanayoeleza nani ataponywa ni sawa na na yale yanayo eleza nani atazaliwa mara ya pili.

Ya Wokovu:	**Ya Uponyaji:**
* Wote	* Wote
* Yeyote	* Kila

➥ **Kuna Maandiko yanayoonyesha kuwa uponyaji ni kwa wote. Unaposoma haya, tazama mkazo juu ya maneno kila na wote.**

➢ *Kila*

Matayo 9:35 Na Yesu akaenda mijini na vijijini, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri injili ya ufalme, na kuwaponya wagonjwa na wenye maradhi kati yao.

➢ *Wengi*

Matayo 14:36 Wamsihi kuwa waliguze tu pinde ya vazi Lake, na kadri wengi walipoliguza ndipo walipata uponyaji kamili.

➢ *Wote*

Matayo 12:15 Lakini Yesu alipogundua haya, akatoka pale; na umati mkubwa ulimfuata, Naye akawaponya wote.

➢ *Wote*

Matayo 8:16,17 Jioni ilipofika, walimletea watu wengi wenye pepo. Naye akawakemea pepo kwa neno, na kuponya wote waliokuwa wagonjwa ...

➢ *Wote*

Luka 6:19 Na umati wote ukatafuta kumgusa, kwa kuwa nguvu zilimtoka na kuwaponya wote.

➢ *Wote*

Matendo 10:38 ... jinsi Mungu alimpaka mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu na nguvu, aliyeenda kila mahali akifanya mema na kuponya wote walioteswa na ibilisi, kwa kuwa Mungu alikuwa Naye.

Yeye Hajabadilika!

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliandika kuwa Yesu hajabadilika; Yeye ni yule yule leo.

Waebrania 13:8 Yesu Kristo ni yule yule jana, leo, na milele.

Ikiwa aliponya alipokuwa duniani, ataponya leo! Yeyote ajaye kwake kwa imani atapokea uponyaji wao.

YESU ALITOA AGIZO KUU

Maagizo ya Mwisho

Kabla Yesu hajapaa mbinguni. Alitoa kwetu maagizo ya mwisho. Tunaita haya Agizo Kuu.

Mariko ameyaandika maneno haya ya mwisho ya muhimu kwa Waamini Wake.

Mariko 16:15-19 Naye akawaambia, "Enendeni ulimwenguni kote na kuhubiri injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokolewa; lakini yeye akataaye kuamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitawafuata wale watakaoamini: Katika jina langu watakemea pepo; watanena katika ndimi mpya; watainua nyoka; na kunywa sumu, lakini haitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapona."

Basi, baada ya Bwana kusema nao, alipokelewa juu mbinguni, na kuketi mkono wa kuume wa Mungu.

Hii sio tu pendekezo kuu – ni amri!

Yesu, Mfano Wetu

Wengi wana ugumu kuamini kuwa Yesu ni mfano wetu tunapoangazia uponyaji Wake na huduma ya miujiza. Wanawaza kuwa miujiza yake ilitokana na nguvu Zake Yeye kuwa Mwana wa Mungu. Hii si kweli.

Yesu alikuwa mfano wetu wa kipekee kwa sababu kwa muda aliweka kando haki zake kama Mwana wa Mungu na

akaja hapa duniani kuishi na kuhuduma kama mwanadamu, kama Adamu wa mwisho. Hata kama kwa kweli alikuwa Mungu, aliishi na kuhudumu hapa duniani kama Mwana wa Adamu.

Hapakuwa na miujiza iliyoandikwa maishani mwake hadi Roho Mtakatifu alipokuja juu yake alipobatizwa kwenye mto Yordani. Huduma Yake ilifanywa katika nguvu na utenda kazi wa vipawa vya Roho Mtakatifu, kama vile inatupasa kuishi na kuhudumu kama waamini waliobatizwa katika Roho.

➢ *Alitiwa Mafuta na Roho Mtakatifua*

Yesu alisema Roho Mtakatifu alimtia mafuta Yeye.

Luka 4:18,19 "Roho wa Mungu yu juu yangu, kwa kuwa amenipaka kuihubiri injili kwa maskini. Amenituma kuponya waliovunjika mioyo, kuhubiri ukombozi kwa waliofungwa na kuondoa upofu kwa vipofu, kuwafungua wanaoteseka." Kuhubiri mwaka uliokubalika wa Bwana."

➢ *Sehemu Tatu Kuu*

➥ **Huduma ya Yesu Ilijumlisha,**

- ➢ Mafundisho
- ➢ Mahubiri
- ➢ Uponyaji na Ukombozi

Matayo 9:35 Na Yesu akaenda mijini na vijijini, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri injili ya ufalme, na kuwaponya wagonjwa na wenye maradhi kati yao.

➢ *Yenye Mipaka*

Huduma ya Yesu ilibaki tu katika kijiji kimoja, au mji mmoja kwa wakati fulani. Haikuwezekana Yeye kuwafikia makundi katika kila mji. Aliwaamuru wanafunzi Wake kuomba ili wengine watumwe kama watenda kazi kwa mavuno.

Matayo 9:36-38 Naye alipowaona umati, akawahurumia, kwa kuwa walikuwa wamechoka na kutawanika, kama kondo bila mchungaji. Kisha akawaambia wanafunzi, "Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Kwa hiyo ombeni ili Bwana wa mavuno atume watenda kazi katika mavuno."

YESU ALIWAPELEKA WENGINE

Wanafunzi

Huduma ya Yesu ilizidishwa alipowapeleka wanafunzi kumi na wawili. Iliwapasa kufanya huduma hiyo aliyowaonyesha.

Matayo 10:1,7,8 Na alipowaita wale wanafunzi kumi na wawili Kwake, akawapa nguvu juu ya pepo wachafu, kuwakemea, na kuponya magonjwa na maradhi yote.

Na mnapoenda, hubiri, mkisema, 'ufalme wa Mungu uko juu yenu.' Ponya wagonjwa, wasafishe wenye ukoma, fufua wafu, kutoa pepo. Bure mmepewa, bure peaneni.

➥ **Wanafunzi waliotumwa walitakiwa:**

- ➢ Kuhubiri,
- ➢ Kuwaponya Wagonjwa,
- ➢ Kuwasafisha wenye ukoma,
- ➢ Kufufua wafu,
- ➢ Kukemea peopo.

Wangefanya haya kwa huru na kwa upendo na hruma kama vile Yesu alifanya. Huduma yao ingekuwa kama ile ya Yesu.

Wale Sabini

Baada ya wale kumina wawili kutumwa na kuendelea katika ustadi, Yesu aliwatuma sabini.

Luka 10:1,9 Baada ya hayo Bwana akawaita wengine sabini pia, kisha akawatuma wawili wawili mbele zake kwa kila mji na kote ambako mwenyewe alikuwa karibu aende.

Nanyi mkawaponye wagonjwa watakaokuepo, na mwambie, 'ufamle wa Mungu umekuja karibu nanyi.'

➥ **Agizo hilo halijabadilika. Wale sabini wangefanya:**

- ➢ Kuponya wagonjwa
- ➢ Kuhubiri Injili ya Ufalme wa Mungu.

Huduma iliendelea kupanuka. Yesu kwanza alijizidisha katika maisha ya wale wanafunzi kumi na wawili, na kisha katika maisha ya wale sabini. Hakika walikuwa na mengi ya kujifunza, lakini walikua. Zaidi sana, walimtii Yesu. Baadaye, waliona miujiza mikuu, furaha, na ushindi.

Luka 10:17a Na wale sabini wakarejea kwa furaha ...

Waamini Wote

Kwa amri ya Agizo Kuu, Yesu aliwatuma waamini wote. Wote waliozalia mara ya pili wanalo agizo hilo kuenda katika jina la Yesu Kristo.

Mariko 16:15,17,18 Naye akawaambia, "Enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Na ishara hizi zitawafuata wale waaminio: Katika jina Langu watakemea pepo; watanena katika ndimi geni; watachukua nyoka; nao wakinywa sumu, haitawadhuru; wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapona."

Mitume walipoaga, je, uponyaji ulikoma?

Hapana, Agizo Kuu lilikuwa "wale wanaoamini," sio tu kwa mitume wa awali. Waamini wakati huo na sasa, ni sharti waendelee kuleta uponyaji ulimwenguni.

Waamini leo, wanapaswa kuhubiri Yesu Kristo kama Mwokozi na Mponyaji, na wanapofundisha ukweli, imani ya kupokea na kuhudumu uponyaji itawaonekania.

➥ **Waamini walitumwa nje:**

- ➢ Kwenda kuhubiri
- ➢ Kukemea pepo
- ➢ Kunena katika ndimi
- ➢ Kuweka mikono kwa wagonjwa

Wote wanaoamini(sio tu mitume, wanafunzi, manabii, wainjilisti, wachungaji na walimu) ni sharti wanyoshe mikono yao kwa wagonjwa na watapona.

Waamini wote kila siku inawapasa watende jinsi Yesu alifanya.

Yohana 14:12 Amini, nawaambia, yeye aniaminiye, matendo ninayotenda naye atafanya; na matendo zaidi ya haya atafanya, kwa sababu naenda kwa Baya Yangu.

Waamini wote washiriki injili, wakimtarajia Bwana kutenda kazi nao, na kudhihirisha Neno Lake kwa ishara ziambatanazo nalo.

Mariko 16:20 Na walitoka nje na kuhubiri kila mahali, Bwana akitenda pamoja nao na kuthibitisha neno kwa kufuatisha ishara. Amina.

Waamini wote, wametiwa nguvu na Roho Mtakatifu, na wao ni shahidi. Inawapasa kuanzia katika mji wao wenyewe, na pia wafikie mataifa yao.

Matendo 1:8 Nanyi mtapokea nguvu atakapokuja Roho Mtakatifu juu yenu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na Yudea kote na Samaria, na hadi mwosho wa dunia.

Matthew 24:14 Na injili hii ya ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote kama ushahidi kwa mataifa, na kisha mwisho utakuja.

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alikuja duniani kuleta ukombozi kwa wanadamu wote. Ukombozi huu unajumlisha uponyaji. Yesu alianza kuponya katika huduma Yake binafsi. Kisha akaanza huduma ya kuzidisha kwa kuwafundisha na kuwatuma wanafunzi Wake. Mbinu hii inaendelea hata siku zetu. Sisi kama waamini tumetumwa kuipeleka injili kwa dunia iliyopotea na inayoangamia. Waamini wote sharti waendelee kutenda kazi hiyo Yesu alitenda.

VIONGOZI WA KANISA LA KWANZA WALIENDELEA KUPONYA

Baada ya Yesu kupaa mbinguni, je, uponyaji ulikoma? Hapana, wanafunzi waliendela kuhubiri injili na kuponya wagonjwa. Hapa tunatazama mifano ya Petro, Filipo, na Paulo.

Petro

Petro alitaja jina la Yesu kwa kilema, naye aliponywa.

Matendo 3:1-8 Sasa Petro na Yohana pamoja walienda hekaluni wakati wa saa ya maombi, saa tisa.

Na kulikuwa mtu mmoja kilema toka tumboni mwa mamake, ambaye kila siku walimweka langoni mwa hekalu liitwalo nzuri, kuomba kutoka kwa walioingia hekaluni: ambaye alipowaona Petro na Yohana wakiingia hekaluni, akawauliza msaada.

Na kwa kumkazia macho, na Yohana, Petro akasema, "Tutazame." Kisha akawaangalia, akitarajia kupokea kitu kutoka kwao. Kisha Petro akasema, "Fedha na dhahabu hatuna, bali kile tulicho nacho tutakupa: Katika jina la Yesu Kristo, inuka na utembee."

Naye akamchukua kwa mkono wa kuume na kumwinua, na ghafla miguu yake na mifupa ya visigino ikapata nguvu. Basi yeye, akiruka juu, akasimama na kutembea na kuingia hekaluni pamoja nao- akitembea, akiruka, na kumsifu Mungu.

Filipo

Filipo, kiongozi aliyefanyika mwinjilisti baadaye, alihubiri injili ya Yesu Kristo kwa wale walioko Samaria na miujiza ya uponyaji ilitendeka.

Matendo 8:5-8 Kisha Filipo akaenda mji wa Samaria na kuhubiri Kristo kwao. Nao umati kwa pamoja wakayashika maneno aliyohubiri Filipo, wakisikia na kuona miujiza aliyofanya. Kwa kuwa pepo wachafu, wakilia kwa sauti kubwa, waliwatoka wengi waliopagawa; na wengi waliokuwa wamepooza na vilema wakaponywa.

Na palikuwepo furaha tele katika mji ule.

Paulo

Paulo lihubiri injili ya Yesu Kristo kwa kilema, na mtu huyo akaponywa.

Matendo 14:8-10 Na katika mji wa Listra alikuwepo kiwete, ambaye alikuwa amelemaa tangu kuzaliwa na hakuwa ametembea kamwe. Alimsikiliza Paulo alipokuwa akihubiri. Paulo alipomtazama akaona ana imani ya kuponywa, akapaza sauti, "Simama kwa miguu yako!" Mara yule mtu akasimama upesi akaanza kutembea.

Alimpomya mtu mwenye homa na mharo.

Matendo 28:8,9 Baba yake Pablio alikuwa mgonjwa kitandani, akiwa anaumwa homa na kuhara damu. Paulo akaingia ndani ili kumwona na baada ya maombi, akaweka mikono juu yake na kumponya. Hii ilipofanyika, wote katika kisiwa waliokuwa na magonjwa pia wakaja na wakaponywa.

From the above verses, we can conclude that the early church leaders ministered healing.

UPONYAJI HUFUNGUA MILANGO YA UINJILISTI

Uponyaji hufungua nafasi ili kushiriki injili na wasiookoka. Kabla mtu hajaitikia injili, ni lazima kwanza tupate ruhusa yao. Katika ulimwengu uliojaa maumivu, uponyaji huleta usikivu wa mtu na haraka huimarisha ukweli wa Neno la Mungu.

Miujiza Kufuata Ufufuo

Mkutano wa kwanza wa kiinjili baada ya ufufuo, ulianza na uponyaji. Mwujiza wa uponyaji wa kilema katika langoNzuri, ulifungua mlango wa watu elfu tano kuokoka.

Matendo 3:8-11 Basi yeye, akiruka juu, akasimama na kutembea na kuingia hekaluni pamoja nao-akitembea, akiruka na kumsifu Mungu. Na watu wote wakamwona akitembea akimsifu Mungu. Kisha wakajua kuwa ni yule aliyekuwa langoni mwa hekalu; na wakishangaa sana kwa kile kilitendeka.

Na sasa yule kiwete aliyeponywa aliwafuata Petro na Yohana, watu wote wakakimbia pamoja kuwaendea katika pochi iitwayo ya Suleimani, wakiwa na mshangao.

Matendo 4:4 Lakini, wengi kati ya wale walisikia neno waliamini; na idadi ya wanaume ikafikia kama elfu tano hivi.

Hebu tutazame vitendo vya Petro na Yohana.

- ➢ Walikuwa wakifanya kazi ya kawaida – mwujiza ulifanyika inje ya kanisa.
- ➢ Walimwona mtu na kunena naye. Walichukua hatua na kutoa uponyaji.
- ➢ Hakupotoshwa na msaada wa awali wa pesa.

- ➢ Walipeana kile walikuwa nacho – Neno la Mungu na nguvu za jina la Yesu.
- ➢ Walinena kwa mamlaka.

Mbinu Hazijabadilika!

Mbinu za kufikia ulimwengu hazijabadilika.

Yesy alihudumu kwa:

- ➢ Kufundisha
- ➢ Kuhubiri
- ➢ Kuponya

Wale Kumi na Wawili walitumwa ili:

- ➢ Kuhubiri
- ➢ Kuponya
- ➢ Kuosha
- ➢ Kufufua wafu
- ➢ Kukemea Pepo

Wale sabini walitumwa ili:

- ➢ Waponye wafu
- ➢ Kuwambia, "Ufalme wa mbinguni umewadia."

Nasi tumetumwa ili:

- ➢ Kwenda na kuhubiri
- ➢ Kutoa mapepo
- ➢ Kunena katika ndimi
- ➢ Kuweka mikono kwa wagonjwa

➥ **Uponyaji haupatikani tu kwa wale wanaoamini, Yesu anataka sisi kuhudumu uponyaji kwa wasiookoka ili wajue Neno ni kweli na waokolewe!**

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, ni mambo gani muhimu tunayojifunza katika miujiza ya kwanza miwili ya Yesu?

2. Je, Agizo Kuu ni gani kama ilivyotolewa katika injili ya Mariko? (Tafadhali ikariri.)

3. Je, mbinu ya Yesu kufikia ulimwengu ilikuwa gani? Je, mbinu yetu inatakiwa iwe ipi? Kwa nini?

Somo la Nne

Roho Mtakatifu na nguvu Zake

Mtume Paulo aliandika,
1 Corinthians 2:4 Ikiwa hotuba na mahubiri yangu hayakuwa na maneno ya kushawishi maneno ya hekima ya mwanadamu, bali katika kuonyesha matendo ya Roho, na ya nguvu, kuwa imani yako isiwe katika hekima ya wanadamu bali katika nguvu za Mungu.

Hakika, tunaitaji nguvu ile ya Mungu ambayo alikuwa nayo, lakini ni ipi?

NGUVU YA UPONYAJI KATIKA MAISHA YA YESU

Utendaji wa wa nguvu za Roho Mtakatifu ulianza katika huduma ya Yesu punde tu Roho Mtakatifu alipokuja juu Yake alipobatizwa katika mto Yordani.

Nguvu iliyokuwa ndani ya Yesu, iliwekwa ndani ya mili ya wale walioitaji uponyaji walipomguza Yeye kwa imani, au alipowaguza. Hadidhi ya mwanamke aliyeteswa kwa ufuchaji wa damu kwa miaka kumi na miwili ni mfano wa nguvu hizi.

Nani Aliyeniguza?

Mariko 5:25-34 Sasa palikuwa na mwanamke mmoja aliyekuwa na tatizo la ufuchaji damu kwa miaka kumi na miwili, na aliteseka sana akitafuta madaktari wengi. Alitumia kila kitu alichokuwa nacho lakini hali ilizidi kuwa mbaya. Naye aliposikia kuhusu Yesu, alikuja nyuma Yake katika umati na kuyaguza mavazi Yake;kwani alisema, "Bora tu niyaguze mavazi Yake, nitaponywa." Punde ufuchaji wa damu ukaisha na kukauka, na akasikia katika mwili wake kuwa aliponywa kutokana na maradhi hayo.

Naye Yesu, mara moja akajuwa kuwa nguvu imemtoka, akageuka kwa umati na kusema " Nani aliyegusa vasi langu?"

Lakini wanafunzi Wake wakamwambia, "Unaona kuna umati mkubwa karibu Nawe, na unasema, 'Nani aliyenigusa?'"

Na akaangalia kumwona yule aliyefanya haya. Lakini mwanamke, akiogopa, na kutetemeka, akijuwa nini kilitendeka kwake, akaja na kuanguka chini mbele zake na kumwambia ukweli wote. Naye akamwambia, "Binti, imani yako imekuponya. Nenda kwa amani, na uponywe kutokana na maradhi yako."

Nguvu iliyotoka kwa Yesu ilikuwa kweli kabisa na hata akasimama na kuuliza, "Nani aliyeguza vasi langu?"

Nguvu ya Hali ya juu

Katika msitari wa thelathini, neno tafsiri "nguvu" Kigriki ni neno "dunamis," maana yake nguvu za Mungu. Dunamis ni neno la kawaida linaloeleza nguvu katika lugha ya Kigriki. Kwa kweli tunalifahamu neno hili kwa sababu maneno yetu ya Kingereza – yanaonyesha maneno ya mlipuko. Yesu alijua kuwa nguvu imemtoka.

Neno hili la Kigriki linatumika mara nyingi.

Luka 4:14 Kisha Yesu akarudi Galilaya akiwa na nguvu (dunamis) ya Roho, na habari zake zikaenea kote maeneo hayo.

Yesu alijua kuwa nguvu hii ilitoka Kwake. Ilikuwa nguvu kuu itokanayo na kuguswa. Kugusa ni sehemu ya kukutana.

Luka 6:19 Na umati wote ukatafuta kumgusa, kwa kuwa nguvu zilimtoka na kuwaponya wote.

Nguvu hii ya uponyaji ilikuja juu ya Yake alipobatizwa. Yohana alishuhudia nguvu hii.

John 1:32 Naye Yohana akawa mshahidi, akisema, "Niliona Roho akishuka kutoka mbinguni kama njiwa, na akasalia juu Yake."

Upako Tofauti Tofauti

Yesu alipohudumu katika nguvu za Roho, alitenda katika sehemu tofauti za upako. Kwa mfano, alikuwa na upako tofauti wa kuhubiri au kufundisha na ule wa kukemea ibilisi au kuponya wagonjwa.

Katika Luka, tunaona wakati ambao Yesu alifundisha, na alipokea upako kuwaponya wagonjwa.

Luka 5:17 Na ikawa siku moja, alipokuwa akifundisha, na palikuwepo Mafarisayo na walimu wa sheria walioketi, ambao walifika kutoka mjo wa Galilaya, Judea, na Yerusalemu. Nazo nguvu za Mungu zilikuwepo kuwaponya.

Nasi pia ni sharti tujifunze kuenenda katika upako wa sasa. Sisi, kama Yesu, lazima tuongozwe na Roho wa Mungu.

Yohana 5:19 Kisha Yesu akajibu akiwambia, "Amini, nawambia, Mwana wa Mungu pekee hawezi kufanya chochote, lakini kile Yeye humwona Baba Yake akifanya; kwa kuwa chochote afanyacho, Mwana pia hufanya hivyo hivyo."

NGUVU YA UPONYAJI NA MTUME PAULO

Nguvu ya Dunamis

Neno la Kigriki, dunamis, pia lilitumika kama nguvu wakati mtume Paulo aliandika kuhusu kutenda katika Roho na nguvu katika huduma yake.

1 Wakorintho 2:4 Nayo hotuba na mahubiri yangu hayakuwa ya maneno ya kuvutia ya hekima ya mwanadamu, bali huonyesha nguvu (dunami) za Roho.

Mtume Paulo alihudumu katika nguvu hiyo kama Yesu – katika nguvu ya dunamis – nguvu ya Roho Mtakatifu.

Tunapata mifano mingi katika kitabu cha Matendo ya kutenda katika nguvu ya dunamis katika huduma ya Paulo wakatika alinyosha mikono yake kwa wagonjwa na pia kuibadili nguvu hii kupitia vitambaa na mavazi.

Matendo 19:11,12 Naye Mungu alitenda miujiza ya ajabu kwa mikono ya Paulo, ili hata vitambaa na leso kutoka kwa mwili wake viliwekwa juu ya mili ya wagonjwa, na magonjwa yaliwaacha na pepo kutowatoka.

Mfano Wetu

Kutoka kwa mfano huu, tunaweza kujifunza vitu vingi.

- ➢ Nguvu ya Mungu ya uponyaji ni ya kweli kabisa na inaonekana, inaweza kupitishwa katika vitambaa.
- ➢ Mbinu hii ya kuhudumu uponyaji iliweza kutumika na Paulo wakati hangeweza kuwafikia wagonjwa na hangeweza kuletwa kwake.
- ➢ Kitambaa ilikuwa sehemu ya kukutana.
- ➢ Ilikuwa na matokeo kama vile Paulo aliwafikia binafsi na kuweka mikono yake juu yao.
- ➢ Paulo alihudumu uponyaji katika nguvu za Mungu katika huduma yake.

Kama Yesu, Paulo alikuwa na nguvu ya uponyaji katika Roho Mtakatifu maishani mwake, na kwa imani, watu walipokea uponyaji.

NGUVU YA UPONYAJI KATIKA WAAMINI-WALIOBATIZWA

Tunazo Nguvu

Wengi husema, “Ninajua nguvu hii ilikuwa mikononi mwa Yesu! Najua nguvu hii ilikuwa mikononi mwa mtume Paulo. Lakini, hiyo ina maana gani kwangu leo? Mimi ni mwamini wa kawaida tu. Je, nitawezaje kuona nguvu hii ikifanya kazi maishani mwangu na huduma?”

Kwa kuyajibu maswali haya, tuoyaone maneno ya mwisho ya Yesu katika kitabu cha Matendo.

Matendo 1:8 Nanyi mtapokea nguvu atakapokuja Roho Mtakatifu juu yenu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na Yudea kote na Samaria, na hadi mwosho wa dunia.

Hili ni neno lile kama nguvu, dunamis, iliyotumika kueleza nguvu ya uponyaji katika Yesu na Paulo. Kama waamini waliobatizwa, tunazo nguvu zile zile ndani yetu zilizokuwa ndani yao.

Nguvu ya dunamis huachiliwa tukiwa mashahidi, kuachilia nguvu kutoka na kuwafikia wengine. Mungu hudhihirisha Neno Lake ndani yetu kwa kuhudumu uponyaji kwa wagonjwa, tutakuwa mashahidi kamili kwa kupeleka injili katika Yerusamu yetu, Yuda, Samaria na ulimwenguni kote.

Nguvu Kuu

Kama ilivyokuwa katika kitabu cha Matendo, tutakuwa na nguvu kubwa na kuwa mashahidi Wake.

Matendo 4:33 Na kwa nguvu za juu (dunamis) mitume wakatoa ushahidi juu ya ufufuo wa Bwana Yesu. Na neema kubwa ilikuwa juu yao wote.

Matendo 6:8 Naye Stefano, alijawa na imani na nguvu ya (dunamis), alifanya miujiza na ishara kati ya watu.

Uwezo wa Mungu kutenda kazi kuu kwetu na ndani yetu ni kwa nguvu ya Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu.

Nguvu Kuu isiyo na Kifani

Waamini wengi waliobatizwa wamemwuliza Mungu atume nguvu zaidi. Kama Mungu angejibu ombi hilo na kutuma nguvu zaidi ya ile tumepokea, huenda tukapasuka. Tayari tunayo nguvu kuu ndani yetu. Kila mmoja wetu tayari anayo "anatembea na kipande cha nguvu kuu!"

Waefeso 3:20 Na kwa Yule awezaye kufanya zaidi ya yote tunayoweza kuuliza au kuwaza, kulingana na nguvu (dunamis) ifanyayo kazi ndani yetu ...

Mara nyingi tumeshindwa kuona uponyaji kwa kumwuliza Mungu ili atume nguvu ya uponyaji kutoka juu kuponya, badala ya kutuma, kwa imani, nguvu ya uponyaji ambayo tayari i ndani yetu katika Roho Mtakatifu.

Acha Itiririke

Yohana 7:38 Yeye aniaminiye, kama vile Maandiko yanasema, kutoka moyoni mwake itatoka mito ya maji ya uzima.

Mungu si athumani. Tunayo nguvu ile ile Yesu na mtume Paulo walikuwa nazo, na i ndani yetu tunapojazwa na Roho. Nguvu hii ya uponyaji ni nguvu ya Roho Mtakatifu.

Ufafanuzi

Baadhi ya dini za uongo yanafundisha juu ya nguvu za ndani na yanugusia roho wa mwanadamu. Tunapozungumzia juu ya nguvu za ndani, tunazungumzia juu ya Roho Mtakatifu na uponyaji wetu wenyewe au wengine katika na kupitia jina la Yesu. Ndani yetu, bila Roho Mtakatifu, au bila ya mamlaka ya jina la Yesu, hatuwezi kufanya chochote.

KUPOKEA NGUVU ZA ROHO MTAKATIFU

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ilikuwa ahadi kwa waamini wote.

Matendo 1:4,5 Na kwa kukusanyika pamoja nao, aliwaamuru wasitoke Yerusalemu, bali wasubiri ahadi ya Baba, "ambayo" alisema, "mmesikia kutoka kwangu; kwa kuwa Mtakatifu si siku nyingi kutoka sasa."

Waamini walipokea nguvu ili wafanyike mashahidi Wake, nguvu ambazo zitafanywa na kuonyesha Neno la Mungu katika ishara, miujiza na uponyaji.

Matendo 1:8 Nanyi mtapokea nguvu atakapokuja Roho Mtakatifu juu yenu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na Yudea kote na Samaria, na hadi mwosho wa dunia.

Wayahudi

Waamini Yerusalemu walikuwa wa kwanza kupokea hii nguvu walipobatizwa katika Roho Mtakatifu siku ya Pentekote

Matendo 2:1-4 Sasa siku ya Pentekote ilipowadia, wote walikuwa pamoja. Na ghafla pakaja sauti kutoka mbinguni, kama mawimbi yakipiga, na ikajaza chumba chote walikokuwa wameketi. Kisha pakatokea kwao miale iliyokawanyishwa, kama ya moto, na moja ikakaa juu ya kila mmoja. Na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena katika ndimi zingine, Roho akiwapa usemi.

Wasamaria

Kisha Wasamaria wakapokea nguvu hii.

Matendo 8:14-17 Na ikawa mitume waliokuwa Yerusalemu waliposikia kuwa Samaria wamelipokea neno la Mungu, waliwatuma Petro na Yohana kwao, ambao,basi walipofika, waliwaombea ili wapokee Roho Mtakatifu. Kwa kuwa hakuwa amekaa juu ya yeyote. Walikuwa wamebatizwa tu katika jina la Bwana Yesu. Kisha wakawawekea mikono juu yao, na wakapokea Roho Mtakatifu.

Watu Mataifa

Wale wa Siseria walikuwa wa kwanza kupokea nguvu hizi.

Matendo 10:44-46a Wakati Petro alikuwa angali akiongea maneno haya, Roho Mtakatifu akaja juu ya wote waliosikia neno. Na wale wa

tohara walioamini walishangaa, kwa kuwa wengi waliokuja na Petro, kwa kuwa karama ya Roho Mtakatifu ilikaa juu ya watu wa mataifa pia. Kwa kuwa waliwasikia wakinena katika ndimi na kumuinua Mungu.

Kisha waamini wa kiefeso wakapokea nguvu hii.

Matendo 19:2-6 Akawaambia, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?"

Nao wakamwambia, "Hatujasikia kamwe kama kuna Roho Mtakatifu."

Naye akawambia, "Je, basi mlibatizwa ubatizo upi?"

Basi wakasema, "Katika ubatizo wa Yohana."

Kisha Paulo akasema, "Yohana kwa kweli alibatiza ubatizo wa toba, akiwambia watu kuwa inawapasa kuamini katika Yeye atakayekuja nyuma, yaani, juu ya Kristo Yesu." Waliposikia haya, walibatizwa katika jina la Bwana Yesu. Na Paulo alipoweka mikono juu yao, Roho Mtakatifu alikuja juu yao, na wanena katika ndimi na kutoa unabii.

KUHUDUMU KATIKA NGUVU

Vyombo vya Udongo

Sisi, kama vyombo vya udongo (chupa ya udongo) tunayo hazina ya Roho Mtakatifu. Miujiza ya uponyaji haitokani na nguvu, bali kwa nguvu ya Mungu ndani yetu.

2 Wakorintho 4:7 Lakini tunayo hazina katika vyombo vya udongo, na kuwa ubora wa nguvu uwe wa Mungu na wala si wetu.

Mika 3:8a Lakini kwa kweli nimejazwa na Roho wa Bwana ...

Kutiwa Nguvu na Roho Mtakatifu

Ni lazima tutiwe nguvu na Roho Mtakatifu ili kuhudumu katika vipawa vya uponyaji. Katika nguvu zetu wenyewe tutashindwa.

Zakaria 4:6 Akajibu na kuniambia: "Hili ni neno la Mungu kwa Zerubabeli: 'sio kwa uwezo na nguvu, bali kwa Roho wangu,' asema BWANA wa majeshi."

Nguvu ya Ufufuo

Nguvu ya uponyaji ya Roho Mtakatifu inayopitia mikononi mwa waamini ni nguvu ile ile iliyomfufua Yesu kutokwa mautini.

Waefeso 1:19,20 Na, Je, nini ukuu unaoongezeka wa nguvu zake kwetu sisi tunaoamini, kulingana na utenda kazi wa nguvu zake kuu alizitenda katika Kristo alipomfufua kutoka kwa wafu nakuketi upande wa kuume mbinguni.

Matendo 4:33 Na kwa nguvu za juu mitume wakatoa ushahidi juu ya ufufuo wa Bwana Yesu. Na neema kubwa ilikuwa juu yao wote.

Matendo 5:12a Na katika mikono ya mitume miujiza na ishara nyingi ilifanyika miongoni mwa watu.

Kulithibitisha Neno

Kitabu cha Matendo kinaonyesha vitendo vya Roho na nguvu ya Mungu katika huduma ya Wakristo wa kwanza.

Mtume Paulo alisema:
1 Wakorintho 2:4,5 Nayo hotuba na mahubiri yangu hayakuwa ya maneno ya kuvutia ya hekima ya mwanadamu, bali huonyesha nguvu za Roho, kuwa imani yenu isiwe katika hekima ya mwanadamu bali katika nguvu za Mungu.

Matokeo bora katika huduma ya Paulo ya kufundisha na kuhubiri haikuwa kwa ajili ya uwezo wake katika ubishi na kuwavuta wengine kwa hekima ya mwanadamu. Kazi yake nzuri ilitokana na vitendo wazi vya nguvu za Mungu zilizokuwa ndani yake alipoziachilia katika mili ya wale walioitaji uponyaji na kukombolewa.

Neno la injili Paulo alihubiri ilithibitishwa katika vitendo hivi na imani ilikaa juu ya watu.

Mariko 16:20 Na walitoka nje na kuhubiri kila mahali, Bwana akitenda pamoja nao na kuthibitisha neno kwa kufuatisha ishara. Amina.

Kukataa Nguvu

Wakristo wengi leo hawana nguvu za Mungu ndani ya maisha yao kwa sababu hawajafundishwa vizuri au, wanakana nguvu ya Roho Mtakatifu.

2 Timotheo 3:5a Kuwa na mfano wa kiungu na kukana nguvu zake.

Ni Yetu

Nguvu iliyokuwa ndani ya Yesu na mitume ikuja juu yetu kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunayo mipaka katika yale tunatenda katika kukosa imani na kujitolea kwa ajili Yake.

Tumetiwa nguvu kutoka juu!

UONGOZY WA ROHO MTAKATIFU

Yesu aliongozwa na Baba

Uponyaji wa kweli hutendeka katika nguvu za Roho Mtakatifu na kwa imani katika Yesu Kristo. Lakini, mara nyingi watu hawapokei nguvu ya uponyaji kwa sababu nyingi. Tutaangalia haya katika somo linguine.

Yesu aliponya "wengi," "kila mmoja" na "kadri ya wengi," lakini Yesu alisema Yeye alifanya tu yale aliona Baba akifanya.

Yohana 5:19,20,30 Kisha Yesu akajibu akiwambia, "Amini, nawambia,Mwana wa Mungu pekee hawezi kufanya chocho, lakini kile Yeye humwona Baba Yake akifanya; kwa kuwa chochote afanyacho, Mwana pia hufanya hivyo hivyo." Kwa kuwa Baba anampenda Mwana, naye humwonyesha yote afanyayo mwenyewe; na atamwonyesha kazi kuu zaidi ya hii, ya kuwa mtashangaa.

"Mimi siwezi kufanya chochote peke yangu. Nisikiavyo, natoa hukumu; na hukumu yangu ni ya haki, kwa kuwa sitafuti mapenzi yangu Mwenyewe bali mapenzi ya Baba aliyenituma."

Katika msitari wa thelathini, Yesu anatuambia kuwa Yeye hatafuti utukufu, bali ule wa Baba.

Yesu Aliongozwa na Roho Mtakatifu

Katika Yohana, tunaona kuwa Yesu aliongozwa na Roho Mtakatifu alipohudumu uponyaji. Katika mfano unaofuata, kuna wengi waliotaka uponyaji. Lakini, kwa kuwa Yesu alitegemea Roho Mtakatifu, aliongozwa kwa mtu Fulani.

Yohana 5:1-9 Baada ya haya palikuwa karamu ya Wayahudi, Naye Yesu akaenda Yerusalemu. Na kule Yerusalemu pana karibu na Lango la Kondoo bwawa, ambalo linaitwa kwa Kiebrania, Bethesda, likiwa na nafasi tano. Hapa palilazwa umati wa watu wagonjwa, vipofu, vilema, waliopooza, wakisubiri maji yasonge. Kwa kuwa malaika aliteremka kwa wakati fulani bwawani akichafua maji, kisha yeyote angeingia kwanza, baada ya maji kuchafuliwa, alipona kwa ugonjwa wowote aliokuwa nao. Na palikuwa na mtu mmoja aliyekuwa amepooza kwa miaka thelathini na minane. Yesu alipomwona amelala hapo, na kujua kuwa alikuwa katika hali hiyo kwa muda mrefu, alimwambia, "Je, unataka kuponywa?"

Yule mtu mgonjwa akajibu, "Bwana sina mtu wa kuniweka ndani ya bwawa maji yanapochuliwa; kwa kuwa ninapokuja, mtu mwingine hunitangulia kuingia."

Yesu akamwambia, "Inuka, chukua kitanda chako na utembee." Punde mtu huyo akaponywa, akachukua kitanda chake, na kutembea. Na siku hiyo ilikuwa Sabato.

Sisi kama Yesu, ni lazima tutegemee uongozi wa Roho Mtakatifu tunapohudumu uponyaji kwa wagonjwa. Hata

Yesu alipoongozwa kwa "mtu fulani," Roho Mtakatifu atatuongozwa kwa mtu aliye tayari kupokea uponyaji katika maisha yetu ya kila siku.

NGUVU ZA UPONYAJI KUTOKA KWA IMANI

Wengi wameuliza, "Ikiwa ninazo nguvu hizi kuu ndani yangu, kwa nini nisione miujiza zaidi ndani ya maisha yangu?" Lazima tujifunze jinsi ya kuongozwa na Roho Mtakatifu. Tujifunze jinsi ya kuwasha taa ya imani ili nguvu ya Roho iweze kupita ndani yetu hadi kwa wagonjwa.

Imani

Mfano wa haya unaweza kupatikana katika mipango ya umeme katika miji na mijengo. Umeme mkubwa unaotokana na genereta unapitia nyaya nono hadi mitamboni. Kutoka hapo inagawanywa kupitia nyaya zingine ambazo huelekea katika mijengo na mwishowe kwa taa tulipo.

Hata kwa kuwa na nguvu zote zilizotuzunguka, itawezekana kuwa kwenye giza kubwa ikiwa mtu hatawasha na kuachilia nguvu ili mwanga uonekane chumbani. Imani ni kama kidude hicho cha kuwashia.

Yesu alionyesha ufunguo wa miujiza ya uponyaji ambayo mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu alipokea.

Mariko 5:34 Naye akamwambia, "Binti, imani yako imekuponya. Nenda kwa amani, na uponywe kutokana na maradhi yako."

Ilikuwa imani yake iliyoachilia nguvu katika Yesu ikaingia mwilini mwake.

Imani kila mara ni kidude kinachoachilia nguvu za Mungu kumwagika. Inaweza kuwa imani ya mtu anayeitaji uponyaji, imani ya wengine walio naye, au imani ya mtu anayehudumu uponyaji.

Imani Huja

Ili kuelewa jinsi imani hii huja na chanzo chake, tutarejea hadithi ya mwanamke.

Mariko 5:27 Naye aliposikia kuhusu Yesu, alikuja nyuma Yake katika umati na kuyaguza mavazi Yake;kwani alisema, "Bora tu niyaguze mavazi Yake, nitaponywa."

Imani ilimjia mwanamke aliyekuwa na tatizo la damu aliposikia kuhusu Yesu. Imani kila mara huja kwa kusikia.

Warumi 10:17 Basi imani huja kwa kusikia, na kulisikia Neno la Mungu.

Kwa kushikilia msimamo wake kati ya pingamizi zote, mwanamke huyu alipokea ufunuo wa kibinafsi kuhusu Yesu na nguvu Zake.

Alitembelea daktari mmoja hadi mwingine na kila wakati alirejea akiwa amevunjika moyo. Sasa pesa zake ziliisha na alidhoofika.

Lakini basi imani ikaja ndani ya roho wake, alitoka nyumbani mwake akamwendea Yesu. Labda jamaa zake walijaribu kumzuia wakitambua kuwa Yeye alikuwa mwanamke "mchafu" na kuwa angepigwa mawe angeonekana na kiongozi wa kidini.

Wakati imani ilipoingia ndani ya roho yake hangetulia. Hata katika unyonge wake, alijisukuma kupita umati karibu na Yesu alipoharakisha kumfikia. Alipomkaribisha Yesu, mmoja wa viongozi wa masinagogi alikuwa akitembea Naye, lakini hakutulia.

Imani inapoingia katika roho zetu, sisi, kama mwanamke huyu, hatutulii. Hisia zetu, kushindwa kwetu kutoka awali, na desturi za kidini haviwezi kutuzuia!

Imani Hunena

Mtume Paulo aliandika,
Warumi 10:6 Lakini haki ya imani hunena ...

Mwanamke hakusema, "Nimewajaribu madaktari wote na hawakunisaidia." Hakusema, "Mimi nina matumaini na kuomba kuwa Yesu anaweza kuniponya." Badala ya hiyo alitangaza kwa ujasiri imani yake. Alisema, "Kama ningemguza tu, nitapona!"

Sasa Imani

Kwa imani, alijua angeponywa.

Imani inapokuja, mambo husonga kutoka yale tumetarajia kwa muda wa baadaye, hadi nyakati za sasa.

Waebrania 11:1 Sasa imani ni kitu cha vitu tunavyotumainia, ushahidi wa vitu tusivyoviona.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alianza na maelezo yake ya imani kwa neno, sasa. Kama ni imani basi inakuwa sasa! Yeye alijua mwujiza wake utakuja takapomguza Yesu. Imani ilifanya mwujiza wake kuwa kweli kabisa yale aliyofunuliwa katika roho yake, hata kabla hajapokea katika mwili wake.

Imani Hutenda

Mwanamke alitumia imani yake na akaliguza vazi Lake.

- ➢ Kuguza ilikuwa sehemu ya kukutana.
- ➢ Iliachilia imani yake ili kupokea.
- ➢ Iliachilia uponyaji kuingia katika mwili wake.

Imani kila mara huambatana na imani-iliyojaa vitendo. Mtume Yakobo aliangika,

Yakobo 2:20b ... imani bila matendo (kuambatana na matendo) imekufa...

Wakati neno la ufunuo la rhema linasababisha imani kuruka ndani ya roho zetu, mambo ambayo tumetumainia huoneka katika wakati wa "sasa." Tunaanza kwa ujasiri kunena tunapoelekea katika vitendo.

Imani ni ufunguo wa kupokea au kuachilia nguvu ya dunamis ya Mungu kuanza. Kwa kuiwasha imani tunaweza kuachilia nguvu ndani yetu na kwa wale wanaoitaji uponyaji.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Andika vifungu vitatu ukijadili nguvu za Yesu za dunamis, katika Paulo na wewe mwenyewe.

2. Eleza jinsi nguvu ya dunamis ya Mungu na imani hufanya kazi pamoja kuleta miujiza.

3. Je, vipi ukweli huu unaweza kufanya kazi maishani mwako?

Somo la Tano

Uponyaji kwa Kuwekelea Mikono

Kuna mbinu nyingi za kuhudumu uponyaji, lakini kuwekelea mikono ni mbinu inayotumika sana katika Agano Jipya. Tunaposikiliza Roho Mtakatifu, Yeye atatuonyeshwa jinsi ya kuhudumu wakati wowote.

Tunapowekelea mikono mgonjwa, tunaleta sehemu ya mapatano ambapo nguvu za Mungu zinaweza kupitia kwetu hadi kwa wengine. Ni kama kuweka nyaya mbili moto pajoma ili nguvu za umeme zipite. Kuwekelea mikono, kama kupaka mafuta, kutumia vitambaa, nguo, huleta mapatano yanayoachilia imani.

Katika somo lijalo, tutajifunza maneno ya imani tunayonena tunapohudumu uponyaji. Mara nyingi, kabla ya kuwekelea mikono juu ya mgonjwa, tunaitaji muda ili kuachilia imani yake kwa kushiriki maandiko ya uponyaji, au kwa kuhuzisha shuhuda za wengine waliopokea uponyaji kama huo.

MISINGI YA BIBLIA YA KUWEKELEA MIKONO

Kuwekelea mikono kunayo mizizi katika Agano la Kale.

Ni muhimu kwetu kuelewa kuwa kuna kitu cha kweli kupitia kuwekelea mikono.

Mifano Katika Agano la Kale

➢ *Dhambi kupitishwa hadi kwenye Mbuzi*

Katika Kitabu cha Walawi, dhambi ilipitishwa hadi kwenye mbuzi.

Walawi 16:21,22 Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya mbuzi aliye hai, akiri juu yake dhambi zote za wana wa Israeli, na kuziweka juu ya kichwa cha mbuzi na atamtuma jangwani kwa mikoni ya mtu anayefaa. Mbuzi atazibeba dhambi zao zote katika nchi isiyokuwa na makaazi; na atamwachilia mbuzi jangwani.

➢ *Hekima Kupitishwa*

Kupitia kuwekelea mikono na Musa, roho wa hekima alipitishwa hadi kwa Yoshua.

Kumbukumbu 34:9 Sasa Yoshua mwana wa Nuni alijaa roho wa hekima, kwa kuwa Musa aliwekelea mikono juu yake, na kafanya kama vile BWANA alimwamuru Musa.

Kanuni Za Msingi

Tunapata katika Waebrania kuwekelea mikono ni mojawapo ya kanuni za msingi za Kristo.

Waebrania 6:1,2 Kwa hiyo, kuacha kanuni za kimsingi za Kristo, hebu na tuende katika ukamilifu, sio kwa kuweka tena msingi wa toba kutoka matendo yasiyo hai na katika imani kwa Mungu, ya ufufuo kutoka kwa wafu, na ya hukumu ya milele.

Kuwekelea mikono kila mara imetumika kupeana au kupitisha, kutoka mmoja hadi mwingi.

Kupokea Roho Mtakatifu

Paulo alipofika Efeso, aliwekelea mikono yake kwa waamini na Roho Mtakatifu akaja juu yao.

Matendo 19:6 Na wakati Paulo aliwekelea mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao, na wakanena katika ndimi na kutoa unabii.

Paulo alimwambia Timotheo kuchochea vipawa vilivyowekwa juu ya kwa kuwekelewa mikono.

2 Timotheo 1:6 Basi nakukumbisha kuchochea kipawa cha Mungu ndani yako kwa kukuwekelea mikono yangu.

As these examples illustrate, the Scripture teaches that there is a spiritual impartation through the laying on of hands.

Usipuuze

Huduma ya kuwekelea mikono isipuuzwe. Ni lazima tutambue, kujua, na kuheshimu wale wanaohudumu kati yetu.

1 Wathesalonike 5:12 Na tunakusihi, wapendwa, kutambua wale wanaotenda kazi kati yenu, na walio juu yenu na wanawaongoza...

Kuwekelea mikono ambako kuliashiria kupokea vipawa vya Roho Mtakatifu, au upako na kutambua huduma haikuwa iwe ya haraka, lakini iongozwe na Roho wa Mungu.

1 Timotheo 5:22a Usimwekelee mikono mtu yeyote haraka ...

YESU ALIHUDUMU KWA KUWEKELEA MIKONO

Wakati Yesu alihudumu uponyaji, kila mara alinyosha mikono, akigusa, kuwekelea mikono Yake juu ya watu.

Mwenye Ukoma

Ukoma ulikuwa ugonjwa wa kuambukiza sana. Lakini, mtu wa ukoma alipouliza aponywe, Yesu alihudumu kwa kuwekela mikono – alimgusa.

Mariko 1:40,41 Kisha mtu mwenye ukoma akaja kwake, akinyenyekea, akipiga magoti na kumwambia, "Ikiwa ungependa, unaweza kunifanya msafi."

Na Yesu, kwa huruma, akanyosha mkono wake na kumguza, na akamwambia, "Ningependa; na uwe safi."

Binti wa Yairo

Wakati Yesu aliitwa kitandani alikoaga binti wa Yairo, alimchukuwa kwa mkono (kuwekelea mikono) na kunena uhai ndani ya mwili wake.

Mariko 5:35-42 Alipokuwa angali akisema, wengine wakaja kutoka kwa kiongozi wa nyumba ya sinagogi aliyesema, "Binti wako ameaga. Kwa nini umsumbue mwalimu zaidi?"

Punde tu Yesu kusikia maneno yaliyosemwa, alimwambia kiongozi wa Sinagogi, "Usiwe na hofu, amini tu."

Na hakumruhusu yeyote kumfuata isipokuwa Petro, Yakobo, na Yohana nduguye Yakobo. Kisha akafika nyumbani mwa kiongozi wa Sinagogi, na kuona wale waliolia kwa sauti. Alipoingia ndani, aliwaambia, "Mbona mwafanya mtafaruku na kilio? Motto hajaaga, lakini amelala." Na wakamchekelea sana.

Lakini alipowatoa wote nje, akawachukuwa baba na mama wa mtoto, na wale waliokuwa Naye, na kuingia pale mtoto alipokuwa amelala. Kisha akamchukua mtoto kwa mkono, na kumwambia, "Talitha, Cum," tafsiri yake "Binti mdogo, nakwambia, inuka," Mara moja msichana akainuka na walked, kwa kuwa alikuwa umri wa miaka kumi na miwili. Na washindwa na mshangao mkubwa.

Mtu Kiziwi na Bubu

Katika mfano huu wa mtu kiziwi na bubu, tunaona kuwa Yesu aligusa sehemu ya mwili iliyokuwa na ulemavu. Aliweka vidole vyake katika msikio ya mtu huyo na kuugusa ulimi wake.

Mariko 7:31-35 Na tena, akiondoka kutoka Taya ya Sidoni, alipitia katikati mwa sehemu ya Dekapoli kwenye bahari ya Galilaya. Kisha wakaleta kwake mmoja liyekuwa kiziwi na haongei vizuri, na wakamsihi amwekelee mkono juu yake.

kisha akamtoa kando na umati, na kuweka vidole vyake kwenye masikio, na akatema mate na kuguza ulimi wake. Kisha, akitazama mbinguni, akamwambia, "Ufuratha," maana yake, "Funguka." Punde masikio yake yakafunguka, na kizuizi kwenye ulimi wake kikaachilia, na akaongea vizuri.

Inachangamsha sana kuona jinsi Yesu aliweka mikono juu ya watu. Mara nyingi ilikuwa kwenye sehemu iliyoitaji uponyaji. Tamaduni zetu kila mara hutuongoza kuwekelea mtu mikono kichwani, tunaweza kujifunza kutokana na mfano wa yesu.

WAAMINI WOTE NA WAHUDUMU KWA KUWEKELEA MIKONO

Mtume Paulo

Paulo pia aliwekelea mikono kwa yule mwenye maitaji.

Matendo 28:8 Baba yake Pablio alikuwa mgonjwa kitandani, akiwa anaumwa homa na kuhara damu. Paulo akaingia ndani ili kumwona na baada ya maombi, akaweka mikono juu yake na kumponya.

Waamini Leo

Yesu na Paulo waliwaponya watu wengi. Mara nyingi waliwaguza wagonjwa walipowaponya. Sisi, kama waamini pia tumagizwa kuwekelea mikono juu ya wagonjwa.

Mariko 16:17a,18b Na ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini: katika jina langu wata ... wekelea mikono wagonjwa, na watapona.

Maagizo ya mwisho aliyonena Yesu kulingana na kitabu cha Mariko inaonyesha upendo Wake mkuu na huruma kwa wagonjwa. Maneno haya ni ya waamini leo. Sisi pia, tunatakiwa kuwekelea mikono wagonjwa.

MAAGIZO YA WAZI YA KUWEKELEA MIKONO

> Kumbuka: kwa kushiriki huduma ya uponyaji kwa wagonjwa, hatusemi kuwa hii ni mbinu tu, au inayofaa utumie. Ni, hata hivyo, mbinu zilizothihirishwa kuwa za kweli katika kufaulu kwetu na maelfu ya watu duniani.

Kuna mwongozo Fulani katika kuwekelea wagonjwa mikono. Hii ina msingi yake katika Neno la Mungu, na miaka ya ustadi.

Mahali pa Kusimama

Kwa kuwa nguvu ya uponyaji ya Mungu iko ndani ya miili yetu, tunaitajika kusimama mbele ya mtu kadri inavyowezekana. Hii pia itazuia usumbufu wa aina yoyote na kumruhusu mtu huyo kufuatilia yale tunasema na kufanya. Tumia mkono au yote miwili kadri unavyoongozwa na Roho Mtakatifu.

Pata Mahitaji

Mwulize mtu kitu gani anaamini hasa uponyaji wa Mungu. Kwa mfanoi, mtu labda yuko kwenye kiti cha magurudumu na tunaamua kuwa wanataka uponyaji katika sehemu hiyo, lakini wanaweza kuwa na maumivu mabaya ya kichwa ambayo wanataka kuombewa.

Uliza swali lako vizuri ili anayetaka msaada ajibu kwa busara na kutazamia katika imani.

Usimwache akupatie orodha ya maelezo yaliyo kinyume. Kwa kusema hivyo watakuwa wakisema, “hali yangu ni

tofauti. Hii itakuwa ngumu Mungu kuniponya." Usiruhusu mawazo yaliyo kinyume. Uliza tena, "Je, unaamini nini Mungu angekufanyia sasa hivi?"

Uwe makini, lakini katika ubora na usiwaruhusu waendelee kutoka taarifa iliyo kinyume. Hii hupunguza imani na inaweza kuzuia uponyaji wao.

Hata kama watakwambia nini, kila mara jibu kwa kusema, "Hiyo ni rahisi kwa Mungu!" Ndiyo. Weka mawazo yako juu ya jinsi Mungu alivyo mwenye nguvu, na jinsi anataka waponywe!

Matayo 19:26 Lakini Yesu aliwatazama na kuwaambia, "Kwa mwanadamu hii haiwezekani, lakini kwa Mungu yote yanawezekana."

➥ **Mawazo ya kinyume huleta shaka. Maneno ya busara yenye msingi wa Neno la Mungu hujenga imani.**

Gusa sehemu Inayoitaji Uponyaji

Gusa sehemu ya mwili inayoitaji uponyaji kwa ajili ya kupitisha nguvu za uponyaji wa Roho Mtakatifu.

Matayo 9:29 Kisha akayagusa macho yao, akisema, "Kulingana na imani basi iwe hivyo kwako."

Usiwekelee mikono katika sehemu nyeti ya mtu. Ikiwa mtu wa jinsia tofauti anaitaji uponyaji katika sehemu nyeti, basi mtu wa jinsia hiyo akusaidie kuwekelea mikono juu ya yule anayetaka uponyaji.

Au, mtu anayeitaji uponyaji aweke mikono kwenye sehemu inayotaka uponyaji kisha uweke mikono juu ya mokono yao. Ikiwa hii haiwezekani, basi weka mkono wako juu ya kichwa.

Achilia Nguvu za Mungu

Unapowekelea mkono juu ya mtu, weka picha yao kimawazo wakipona kulingana na ahadi ya Neno la Mungu. Achilia nguvu ya uponyaji ya Roho Mtakatifu ipite miilini mwao unaponena kwa ujasiri, tenda, na utarajie matokeo yake.

Kuwahudumia Wengi

Kukiwa na watu wengi wa kuhudumia na upako umejaa, ni bora kutembea haraka haraka bila kuchukuwa muda kusikia maelezo ya maitaji hayo.

Watu wanaweza kukushika ili uwatazame wao tu. Wanaweza kufanya hivyo kwa sababu wanahisi hali yao ni ngumu kuliko ya wengine na itamchukuwa Mungu muda zaidi, lakini hii inadhihirisha kukosa imani na kiburi. Usiwaruhusu wamalize imani yako, au kuzima upako mkubwa wakati huo.

Nenda katika upako wa nguvu wa Roho Mtakatifu na uwekelee mikono juu ya wengi kadri iwezekanavyo kwa muda mfupi ulio nao.

Achilia Imani Yako

Unapowekelea mikono yako juu ya wagonjwa, achilia imani yako ili wapone, sio waende chini ya nguvu, au kuanguka katika Roho.

Watu wanaweza kuanguka katika Roho, na waanguke sakafuni chini ya nguvu za Mungu na wasipo. Wengine wanaweza kupona bila ya kuanguka chini ya nguvu za Mungu. Wengine wanatafuta tu ushahidi juu ya kuanguka katika Roho na hii watapokea.

Kila mara achilia imani yako ili mtu apate uponyaji.

UPONYAJI WA MGONGO, SHINGO

Watu wengi wana maumivu ya mgongo kwa sababu mishiba inachuna kwa ajili ya matatizo ya mgongo, au sehemu iliyopasuka. Mshiba unaochuna hauwezi kupeleka habari kamili kutoka kwenye ubongo hadi kwenye misuli mahali ambapo huleta matatizo mengine mwilini.

Watu wenya maumivu ya mmgongo mara nyingi hua na mguu au mkono mmoja kuwa mfupi kwa sababu ya kutokunyooka mgongoni mwao. Wakati mgongo unaponyooshwa, uponyaji wa Mungu unaweza kuthibitishwa kwa kuvitazama vidole au nyayo za mtu huyo zinaponyooka.

Kuponya Sehemu ya juu ya Mgongo

Ikiwa unahudumia sehemu ya juu ya migongo, mtu huyo asimame miguu yake ikiwa sawa, wachezeshe mikono yao kando ili kutulia, na kisha kushakanisha gumbo na kunyosha mikono yao. Kisha viganja vikiangaliana, na kwa upole walete mikono yao pamoja hadi vidole vigusane. Mara nyingi mkono mmoja utaonekana kuwa mfupi.

Mwagize mtu na wote wanaotazama wafungue macho yao. Kisha watenganishe mikono yao kama nchi moja ili isikutane. Kwa mkono wako fundua na uelekeze juu, acha mikono yao itulie juu ya mkono wako (kuwekelea mikono).

Achilia nguvu za Mungu, kwa ujasiri amuru kila mshipa, misuli, ubafu, na kila sehemu ya mgongo kuponywa na kurejea sehemu kamili. Tazama wakati haya yanatendeka. Hii inapokamilika, waulize watembee na kuangalia migongo yao. Kwa ujasiri uliza, “Je, nini kilitendeka juu ya maumivi?” Kwa haraka, mpe Mungu utukufu.

Tunapoanza kumsifu Mungu kwa yale Ametenda, imani inakua na nguvu. Uponyaji ulioanza tu mara umekamilika. Sifa ni sehemu muhimu ya uponyaji.

Uponyaji wa Sehemu ya Chini ya Mgongo

Unapohudumia mtu anayeitaji uponyaji katika sehemu ya chini ya mgongo mweke aketi juu ya kili wima. Simama, ukimtazama, inama na kuichukuwa miguu yake. Gundua jinsi mifupa ya kisigino au nyayo zao.

Achilia nguvu za Mungu, ukiamuru mifupa, misuli, mishipa iponywe na kurejea katika nafasi kamili. Inapokamilika waulize wasimame na kupima mgongo kwa kuinama au kupiga hatua, au kufanya kile hawangeweza kufanya awali. Tena, kwa ujasiri uliza, "Nini kilitendeka kwa maumivu?" Tena, hakikisha wametoa utukufu kwa Mungu.

Uponyaji wa Shingo

Kumhudumia mtu anayetaka uponyaji wa shingo, ukiweka mikono yako upande wa na shingo lao unapoweka vidole vyako juu ya mfupa wa shingo upande wa chini wa kichwa.

Achilia nguvu za Mungu, ukiamuru mfupa, misuli, na mishipa ya shingo kurejea pamoja vizuri. Kwa upole waulize wasogeze shingo katika pande zote. Achilia mkono wako na kisha wasogeze shingo. Kwa ujasiri uliza, "Nini kilifanyika kwa maumivu?" Mpe Mungu utukufu.

Uponyaji wa Mfupa wa Kiunoni

Kutokulainika kwa mifupa ya kiunoni mara nyingi husababisha kutokulainika kwa miguu, na misuli ya sehemy hiyo. Simama ukimtazama, weka mikono yako juu ya mifupa hiyo (sehemu ya ubafu wa chini) kila upande. Ikiwa mtu ni wa jinsia tofauti nawe, weka mikono juu ya mikono yao. Kwa imani, achilia nguvu za Mungu.

Mara nyingi mwili wao utaanza kugeuka upande hadi mwingine amuru mifupa hiyo, na misuli ianze kukaa sawa kwa nafasi yake. Tena, acha mtu huyo asonge na uangalie mwili wao. Uliza, "Nini kilifanyika kwa maumivu?" Na umpe Mungu utukufu!

UPONYAJI KUPITIA KUPAKA MAFUTA

Kupaka mafuta inaweza aidha kufanywa kwa kumwagia mafuta kichwani au kwa kupaka juu ya uso wa mtu kwa vidole vyako.

Wazee Kupaka Mafuta

Mbinu hii ya uponyaji inatumika na wazee wa kanisa. Hii huonekana kuwa mbinu inayofaa kwa uponyaji wakati dhambi imekuwa mlango ambapo Shetani anatumia kuleta

vita vya magonjwa. Ikiwa dhambi ndicho chanzo, kukiri dhambi hiyo inaitajika ili kupokea uponyaji.

Yakobo 5:14-16 Je, kuna yeyote mwongoni mweni aliye mgonjwa? Basi inampasa awaite wazee wa kanisa wamwombee na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana.

Kule kuomba kwa imani kutamwokoa yule mgonjwa, naye Bwana atamwinua na kama ametenda dhambi, atasamehewa.

Kwa hiyo ungamianeni makosa yenu ninyi kwa ninyi na kuombeana ili mpate kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu tena yanafaa sana.

Ahadi hii ya ya kila mtu aliye mgonjwa atakayeita, au kuwauliza wazee wa kanisa kumpaka na mafuta kwa ajili ya uponyaji.

Wanafunzi Kupakwa Mafuta

Wanafunzi kupakwa mafuta.

Mariko 6:13 Na wakakemea pepo, na kupaka mafuta wengi waliokuwa wagonjwa, na kuwaponya.

Kupaka Mafuta Leo

Katika Biblia nzima, mafuta huonyesha mfano wa Roho Mtakatifu. Wakati mtu amepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, yeye amepata uponyaji wa Mungu ndani na ishara hiyo si lazima tena; lakini inaweza kutumika kama sehemu ya kupatana ili kuachilia imani!

Kupaka mafuta ni lazima iambatane na maombi katika imani ili kuwafanya mgonjwa apone.

Yakobo 5:15a Kule kuomba kwa imani kutamwokoa yule mgonjwa, naye Bwana atamwinua.

Kupaka mafuta kamwe isiwe tupu. Ni sharti ifanywe katika imani, ikiachilia nguvu za Mungu kupita.

UPONYAJI KUPITIA VITAMBAA NA NGUO

Mfano Mmoja

Kutumia vitambaa vilivyopakwa imetajwa mara moja tu katika Agano Jipya.

Matendo 19:11,12 Sasa Mungu alifanya miujiza isiyo kawaida kwa mkono wa Paulo, hata kwamba leso au vitambaa vilivyokuwa vimegusa mwili wa Paulo viliwekwa juu ya wagonjwa, nao wakaponywa magonjwa yao pepo wachafu wakawaacha.

Nguvu ya uponyaji ya Roho Mtakatifu ilipitishwa kutoka mwili wa Paulo hadi leso au vitambaa. Magonjwa yaliponywa na pepo wachafu kuwaacha.

Inafaa Leo?

➥ **Je, leso na vitambaa vinafaa Leo?**

Mungu atatumia mbinu nyingi tofauti ili kumleta mtu katika sehemu ya imani. Usimpe kipimo! Nguvu ya uponyaji wa Mungu inaonekana wazi na inaweza kupitishwa hata kwa kitambaa.

Nguvu hii ya uponyaji huachiliwa na mtu mmoja aliye na imani kamili katika nguvu za Mungu kuponya. Wakati mtu analeta kitambaa kwa mtu mwingine na kuuliza upako juu ya kitambaa hicho, watu wawili au zaidi wamekubaliana kimaombi kwa ajili ya uponyaji wa mtu fulani. Pia, katika imani mtu yule achukue kitambaa na kumwekea mgonjwa.

Kitambaa kilipakwa huwa sehemu ya mapatano, na imani tena inaachiliwa kwa ajili ya kuonyesha nguvu za Mungu. Ni kutenda imani ndiko kutamheshimu Mungu.

Je, Vinatumika Vipi?

➥ **Je, vitambaa vilivyopakwa vitatumika vipi leo?**

Mwamini yeyote aliyebatiswa katika Roho anayeamini katika nguvu za uponyaji ya Roho Mtakatifu anaweza kuwekelea mikono vitambaa, na kuachilia nguvu za Mungu kwa imani.

Imependekezwa kuwa vitambaa vya kawaida vitumike, (wala sio karatasi au vitu vingine).

Mbinu hii inaweza kutumika pia wakati roho mchafu, au roho wa ulemavu anahusika.

Wakati mwingi mtu huwa mgonjwa sana hata asiweze kumfikia mwamini aliyejazwa Roho. Kutumika vitambaa vilivyopakwa ni njia moja ya kuhudumu ikiwa haiwezekani kukutana na mtu huyo.

Uponyaji kupitia mafuta na kupaka vitambaa ni ya kimaandiko na inatumika hata sasa.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kwa nini kugusa ni muhimu unapowahudumia wagonjwa?

2. Kwa nini wakati mwingine ni bora kuwekelea mikono yetu juu ya sehemu ya mwili inayoitaji uponyaji?

3. Ni kupitia hali gani ambapo kupaka mafuta kunaweza kutumika kimaandiko ili kuhudumu uponyaji?

4. Ni kupitia hali gani ambapo ni bora kutumia kitambaa ili kuhudumia uponyaji kwa mgonjwa?

Somo la Sita

Maneno Tunayonena

Imani imepimwa au huachiliwa kwa maneno tunayonena. Katika Somo la Nne, tulijifunza kuwa imani ni kidude kinachoachilia nguvu ya uponyaji ya dunamis ya Roho Mtakatifu kupita. Pia tulijifunza kuwa imani kila mara hunena maneno yaliyojaa imani. Tuliona mfano wa mwanamke mwenye hali ya damu, akinena imani yake aliposema, "Nitaponywa."

Kuna sehemu nne za maneno yaliyojaa imani ambayo tunaitaji kunena kuongezea matarajio ya imani. Nguvu za Mungu za uponyaji huachiliwa kwa,

- ➢ kulitaja jina la Yesu,
- ➢ kukemea roho wa ulemavu,
- ➢ kunena miujiza ya kujitengenezea
- ➢ na kulinena Neno la Mungu

KULITAJA JINA LA YESU

Je, kuna umuhimu wowote kwa kulitaja jina la Yesu? Je, kunazo nguvu katika kulitaja jina hilo?

Maana ya jina "Yesu" kwa kweli ni ombi, "Mungu tuokoe," au maneno "Yehova ndiye Wokovu." Kwa kweli kunazo nguvu katika kulitaja jina la Yesu.

Mamlaka katika Jina

Je, kuna mamlaka gani katika jina la Yesu?

Mamlaka yote katika mbingu na dunaiani.

Matayo 28:18 Kisha Yesu akaja na kuwaambia, akisema, "Nimepewa mamlaka yote katika mbingu na duniani."

Juu ya Majina mengine Yote

Jina la Yesu ni juu ya majina mengine yote

Wafilipi 2:5-11 Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu. Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya si kitu, akajifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu. Naye akiwa katika umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza hadi mauti, naam, mauti ya msalaba!

Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana na kumpa jina lililo kuu kuliko kila jina, ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, vya duniani na vya chini ya nchi, na kila ulimi ukiri ya kwamba YESU Kristo ni BWANA. Kwa utukufu wa Mungu Baba.

Kila ugonjwa na maradhi ina jina lake. Saratani, mafua na homa ni baadhi ya majina. Jina la Yesu liko juu ya majina ya magonjwa haya, na ni lazima yainame wakati imani inapotajwa, "Yesu!"

Uponyaji kupitia Jina

Wakristo wa kwanza walinena uponyaji katika jina la Yesu. Zingatia tena mfano wa Petro na Yohana walipomponya yule mtu, kilema toka tumboni mwa mamaye. Walifanya hivyo katika jina la Yesu.

Matendo 3:4 Kisha Petro akasema, "Fedha na dhahabu hatuna, lakini nilicho nacho nakupa wewe: katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti, inuka na utembee."

➢ *Imani Katika Jina Lake*

Petro, chini ya upako wa Roho Mtakatifu, anatwambia ni katika imani katika Yesu mtu huyo aliponywa.

Matendo 3:16 Na jina Lake, kwa imani katika jina Lake, imemtia nguvu mtu huyu, ambayo mnamwona na kumfahamu. Ndiyo, imani inayokuja kupitia Yeye imempa msimamo huu mbele yenu ninyi wote.

➢ *Kutishwa Kulitumia Jina*

Matokeo ya uponyaji huu, Petro na Yohana walishikwa, kuwekwa korokoroni usiku kucha, na kutishwa na viongozi wa Wayahudi wakiwaambia wasinene tena katika jina la Yesu. Viongozi wa kidini waliitambua nguvu iliyopo katika jina la Yesu.

Petro kwa ujasiri aliwajibu kuhusu uponyaji wa yule kilema kwa kusema,

Matendo 4:10 Hebu na ijulikane kwenu wote, na kwa watu wote katika Israeli, kuwa katika jina la Yesu wa Nazareti, ambaye mlisulubisha, ambaye Mungu alimfufua kutoka wafu, kwa ajili Yake mtu huyu amesimama mbele yenu akiwa amepona.

➢ *Ishara na Miujiza Katika Jina Lake*

Wakati Petro na Yohana walirejea kwa watu wao na kutoa taarifa yaliyotokea, waliinua sauti zao kwa Mungu wakiomba. Walimaliza maombi haya kwa kuuliza ishara na miujiza zaidi.

Matendo 4:29-31 Sasa, Bwana, tazama vitisho vyao, na tupe sisi watumishi wako ujasiri wote ili wanene Neno Lako, kwa kunyosha mkono na kuponya, na kuwa ishara na miujiza itendeke katika jina Lako Mtumishi mtakatifu Yesu.

Na baada ya kuomba, mahali walipokusanyika palitetemeka; na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.

➢ *Kufanya Kila Kitu katika Jina Lake*

Katika Wakolosai tunaamuriwa kufanya kila kitu katika jina la Yesu.

Wakolosai 3:17 Na chochote unachofanya katika maneno au vitendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, kutoa shukrani kwa Mungu Baba katika Yeye.

➢ *Amini Katika Jina Lake*

Mariko 16:17,18 Na ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini: Katika jina langu watakemea pepo; watanena na katika ndimi; watashika nyoka; na wanapokunywa sumu, haitawadhuru kamwe; wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapona.

Hapakuwa na mpangilio maalum katika lugha ya Kigiriki. Tunaweza kwa uangalifu soma kifungu kifuatacho,

Ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini katika jina Langu:

- ➢ Watakemea pepo.
- ➢ Watanena katika ndimi mpya.
- ➢ Watachukua nyoka (ibilisi).
- ➢ Wakinywa sumu, haitawadhuru.
- ➢ Watawekelea mikono wagonjwa na watapona.

Kunayo mamlaka katika jina la Yesu, jina juu ya majina yote. Wakristo wa kwanza walinena uponyaji katika jina la Yesu kwa imani. Hata kati ya vitisho vya mauti, Petro alitilia mkazo kuwa uponyaji ulikuwa katika jina la Yesu.

KUKEMEA MAPEPO CHAFU

Huduma ya Yesu

Katika huduma ya uponyaji ya Yesu uliambatana na kukemea mapepo. Hata leo, wengi wanakombolewa katika magonjwa na maradhi wanapochukua mamlaka juu ya roho hao ambayo yameletwa na adui ili kuiba, kuua, na kuharibu.

Katika Luka, tunasoma kuhusu mwanamke aliyeshikwa na Shetani na roho mchafu.

Luka 13:11-13,16 Wakati huo huo akaja mwanamke mmoja aliyekuwa na pepo mchafu, naye alikuwa amepinda mgongo kwa muda wa miaka kumi na minane, wala hawezi kunyoka wima. Yesu alipomwona, akamwita akamwambia, "Mwanamke, uwe huru, umeponywa ugonjwa wako."

Yesu alipomwekea mikono yake, mara akasimama wima akaanza kumtukuza Mungu.

Yesu anatambua pepo hawa wa ugonjwa kama utumwa wa Shetani.

"Je huyu mwanamke ambaye ni binti wa Abrahamu, aliyeteswa na Shetani akiwa amemfunga kwa miaka hii yote, hakustahili kufunduliwa kutoka katika kifungo hicho siku ya sabato?"

Neno "chafu" maana yake magonjwa au maradhi. Roho mchafu ni roho wa magonjwa au udhaifu. Inaweza kuwa ugonjwa wa aina yoyote.

Magonjwa Yasiyotibika

Kwa Mungu, hakuna magonjwa yasiyoweza kutibiwa. Karibu magonjwa yote ambayo madaktari huyataja kama yasiyotibiwa, yanasababishwa na roho wa pepo. Kwa kuhudumu haya, tunaweza kunena dhidi ya pepo chafu, au kuwaita kwa jina la ugonjwa. Kwa mfano, tunanena dhidi ya pepo wa saratani, homa na mengine.

Kujumlishwa katika orodha ya magonjwa ambayo husemekana kuwa ya mapepo ni kama yafuatayo:
Ukimwi
Unywaji pombe, madawa za kulevya
Arthritis (Kingereza)
Asthma (Kingereza)
Upofu
Saratani
Kupooza
Bubu
Depression (Kingereza)
Ugonjwa wa Kisukari
Kifafa
Kuambukiza
Wazimu
Ukoma
Leukemia (Kingereza)
Lupus (Kingereza)
Multiple Sclerosis (Kingereza)
Ugonjwa unaohusika na Misuli
Parkinson's disease (Kingereza)
Maumivu makali
Palsy (Kingereza)
Sclerosis (Kingereza)
Tumors (Kingereza)

Mifano ya Kiblia

➢ *Bubu*

Matayo 9:32,33a Walipotoka nje, tazama, aliletwa kwake mtu mmoja, bubu na mwenye pepo mchafu. Na pepo alipotoka, yule bubu akaongea.

➢ *Kisiwi na Bubu*

Mariko 9:25 Yesu alipowaona watu wakija kwake, alimkemea pepo mchafu, akisema, "Wewe roho wa bubu na kisiwi, nakuamuru, toka, na umwache kabisa!"

➢ *Kifafa*

Matayo 17:15,18 Bwana, mhurumie mwanangu, kwa kuwa ana kifafa na anateseka; kwa kuwa yeye huanguka motoni na majini.

Na Yesu akakemea pepo, na ikamtoka; na mtoto akaponywa kutoka wakati huo.

➢ *Kipofu na Bubu*

Matayo 12:22 Kisha mmoja akaletwa kwake akiwa na pepo, kipofu na bubu; Naye akamponya, na kisha mtu yule akaongea na kuona.

➢ *Kifua Kikuu*

Luka 13:11,12 Na tazama, kulikuwa na mwanamke aliyekuwa na pepo mchafu miaka kumi na minane, aliyepinda na kamwe hangesimama wima. Lakini Yesu alimwona akamwita aje kwake na kumwambia, "Mwanamke, umefunguliwa kutoka kwa pepo chafu."

Kufunga na Kufungua

Kwa kushughulikia pepo wachafu, tumepewa mamlaka na maagizo kwa ajili ya kufaulu katika huduma.

Matayo 16:19 Nami nitawapa funguo za ufalme wa mbinguni, na chochote mtakachofunga duniani kitafungwa mbinguni, na chochote mtafungua duniani kitafunguliwa mbinguni.

➢ *Kufunga*

Kufunga maana yake kuzuia, kufunga pamoja, kuzuia uwezo wa kutenda. Kwa mfano:

- ➢ "Nakufunga Shetani juu ya mwili wa mtu huyu ..."
- ➢ "Nakufunga wewe pepo wa saratani ..."

➢ *Kufungua*

Kufungua maana yake kumwachilia mtu kutoka ngome ya ungonjwa.

Luka 13:12b "Mwanamke, umefunguliwa kutokana na pepo mchafu."

Kutoa Mapepo

Mojawapo ya agizo tulilopewa, ni kukemea mapepo.

Mariko 16:17a Ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini: katika jina Langu watakemea mapepo ...

Matayo 9:33 Na pepo alipotoka, bubu akaongea. Na umati ukishangaa, ukisema, "haijawahi tokea hivi katika Israeli!"

➢ *Saratani – Kwa Mfano*

Mtu akiwa na saratani, imepandwa kama mbegu mwilini mwake na pepo wa saratani. Hebu tutazame mapendekezo ya kuponya saratani.

- ➢ Kwanza, funga shetani katika jina la Yesu.
- ➢ Funga pepo wa saratani kumwamuru atoke katika jina la Yesu.
- ➢ Laani mbegu ya saratani, na kuiamuru ife.

Ni lazima tuweke shoka la Neno la Mungu kwenye mzizi wa saratani.

Matayo 3:10 Na hata sasa shoka limewekwa kwenye mizizi ya miti. Kwa hiyo kila mti usiozaa matunda mema utakatwa na kutupwa motoni.

Saratani hakika si matunda mema. Tunaweza kuamuru ife na kuharibiwa kutoka mizizini hadi juu.

Weka mikono sehemu inayougua, achilia nguvu za uponyaji kwa imani, nena mwujiza wa kujenga, kisha amuru sehemu iliyoharibika, iliokufa kuwa hai tena, au kurejeshwa katika jina la Yesu.

KUNENA JUU YA MLIMA WA UGONJWA

Mara nyingi, sehemu za mwili hukosekana kupitia ajali, upasuaji, kuzaliwa na ulemavu, au magonjwa. Tunaweza kuhudumu miujiza kwa "kunena juu ya milima" ya magonjwa na kuamuru sehemu mpya kujengeka kwa kulinena Neno la Mungu lenye kujenga.

Mariko 11:23 Kwa hakika, nakwambia, yeyote atakayeambia mlima huu, 'ondoka hadi baharini,' na asiwe na shaka moyoni mwake, lakini aamini kuwa mambo yale asemayo yatatimika, atapokea chochote atakachouliza.

Siku iliyopita, Yesu alikemea mzabibu. Wanafunzi walishangaa walipoupita baadaye na kuona umeakufa. Msitari wa ishirini na tatu ni sehemu ya maelezo ya Yesu kwao. Alikuwa akisema, "Mizabibu ni midogo, unaweza kuamuru mlima uondoke!"

Milima maishani mwetu inaweza kuwa kiroho, kimawazo, au kimwili. Milima hunena juu ya nguvu na uwezo, lakini Mungu na Neno Lake wako imara zaidi na uwezo kuliko mlima.

Amri!

Yesu alisema, "Yeyote anayesema." Hakusema "Yeyote aombaye na kumwuliza Mungu afanye." Kusema ina maana kuamuru.

Katika Biblia hakuna mahali ambapo wanafunzi wanaombea wagonjwa baada ya kuja kwa Roho Mtakatifu. Walihudumu uponyaji kwa wagonjwa kupitia nguvu Zake – nguvu hiyo ya uponyaji ilioko ndani yetu sasa.

Kuponya Wagonjwa!

Wengi wetu tunawaombea wagonjwa kama vile tunamwomba Mungu asiyetaka kuponya na tunapata matokeo machache. Tusimwulize Mungu afanye kitu ambacho tayari ametuambia tufanye katika nguvu Zake.

Matayo 10:8 Kuponya wagonjwa, kuosha wenye ukoma, kufufua wafu, kukemea pepo. Kwa kuwa mmepokea bure mpeane bure.

Mariko 16:18b Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapona.

Kuchukua Utawala

Mungu alimpa mwanadamu utawala na mamlaka.

Mwanzo 1:26a Kisha Mungu akasema, "Hebu na tuumbe mwanadamu kwa mfano Wetu, kwa sura yetu; na wawe na utawala."

Tunaitajika kunena katika mamlaka na nguvu kama vile Yesu alifanya kwa sababu ametupatia mamlaka hayo.

Luka 4:32 Nao wakishangaa kwa mafundisho Yake, kwa kuwa Neno Lake lilikuwa na mamlaka.

Luka 10:19 "Tazama, nawapa mamlaka kuwakanyaga nyoka na nge, na juu ya mamlaka ya adui, na hakuna kitakachowadhuru."

Ujumbe na mamlaka ya Yesu iko ndani yetu na bado inayo nguvu!

Nena Neno

Tunaweza kunena juu ya mti wa ugonjwa.

Luka 17:6 Basi Bwana akasema, "Ikiwa una imani kama mbegu ya haradali, unaweza kuuambia mti huu, 'ngika kwa mizizi na upandwe baharini,' na utatii."

Yesu alikemea homa kuu ya mama mkwe wa Simoni. Alichukua mamlaka juu yake.

Luka 4:39 Basi akasimama juu yake na kukemea homa, na ikamwacha. Na punde akaamka na kuwahudumia.

Kwa mfano, tunaamuru mwili uwe kawaida.

- ➢ "Shinikizo la damu – rudi kawaida!"
- ➢ "Ninaamuru figo hizi kufanya kazi sawa katika jina la Yesu!"

Tunanena miujiza ya kujenga.

- ➢ "Nina nena moyo mpya ndani ya mwili huu!"
- ➢ "Ninaamuru vidole hivi kukua kawaida!"

Mariko 3:1,3,5b Na akaingia sinagogi tena, na mtu alikuwa pale akiwa na mkono uliodhoofika.

Kisha akamwambi mtu huyo aliyekuwa na mkono uliopooza, "Njoo mbele."

Akamwambia, "Nyosha mkono wako." Na akaunyosha, na mkono wake ukapona na kuwa sawa kama ule mwingine.

Nena kwa Ujasiri na Nguvu

Tunaposoma maelezo juu ya uponyaji katika Agano Jipya, mara tunasoma misamiati na mshangao kama ifuatavyo:

Yohana 11:43 Na basialiposema haya, alipaasa sauti, "Lazaro, toka!"

Matendo 3:6b "Katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti, inuka na utembee."

Paulo alimhudumia kilema Lystra.

Matendo 14:9,10 Paulo, kwa kumchunguza na kuona kuwa alikuwa na imani ya uponyaji, alisema kwa sauti, "Simama wima kwa miguu!" na akainuka na kutembea.

Tunayo mifano na maagizo kunena maneno ya uponyaji kwa ujasiri. Hata kama hii ni tofauti na tamaduni zetu, hebu na tufuate Neno la Mungu.

KUNENA NENO LA MUNGU

Kile tunasema ni muhimu katika kuleta uponyaji kwa watu wa Mungu. Maneno yetu yanaweza kuleta uhai au mauti, ugonjwa au afya. Tunatakiwa kunena Neno la Mungu. Maneno ya Mungu huleta uponyaji.

Aidha Uhai au Kifo

Mfalme Suleimani aliweka wazi kuwa uhai na kifo vipo katika nguvu ya ulimi.

Mithali 18:21 Mauti na uhai vipo katika nguvu ya ulimi, na wale wanaoupenda watakula matunda yake.

Watu wengi wanajiua na wengine kwa ajili ya yale wanasema. Wengine wamejufunza kuishi kwa Neno la Mungu kwa imani.

Kiri Wokovu

Moyo huamini, na kinywa hukiri wokovu.

Warumi 10:8-10 Lakini inasema nini? "Neno liko karibu nawe, hata mdomoni na moyoni mwako" (ambayo, neno la imani tunalohubiri): kuwa unapokiri kwa kinywa Bwana Yesu na kuamini moyoni kuwa Mungu amemfufua kutoka wafu, utaokoka. Kwa kuwa kwa moyo mtu huamini haki, na kwa kinywa hukiri wokovu.

Wokovu kamili hujumlisha uponyaji na ukombozi. Kama vile tunaamini moyoni na hukiri kwa kinywa kwa wokovu, kwa hivyo tuamini kwa mioyo yetu na kukiri kwa vinywa vyetu kwa ajili ya uponyaji.

Tangaza Neno

Jemadari mmoja akamjia Yesu na kumwuliza ili mtumishi wake aponywe, alitambua nguvu ya mamlaka na maneno. Alimwambia Yesu, "Sema tu neno, na mtumishi wangu atapona."

Matayo 8:5-10,13 Yesu alipoingia Kapernaumu, jemadari mmoja alimjia, kumwomba msaada akisema, "Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani amepooza, tena ana maumivu makali ya kutisha."

Yesu akamwambia nitakuja kumponya."

Lakini yule Jemadari akamwambia, "Bwana mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu. Lakini sema neno tu, naye mtumishi wangu atapona. Kwa kuwa mimi name niko chini ya mamlaka, nikkiwa na askari chini yangu. Nikimwambia huyu nenda naye huenda, na mwingine nikimwambia 'njoo,' huja. nami nikimwambia mtumishi wangu, 'fanya hivi,' hufanya."

Yesu aliposikia maneno haya, akishangaa, akawaambia wale waliomfuata, "amini amini nawaambia, hata katika Israeli sijaona imani kubwa namna hii!"

Kisha Yesu akamwambia jemadari, "Nenda; na kama vile umeamini, na itendeke kwako." Na mtumishi wake aliponywa wakati huo.

Yesu alimsifu jemadari huyu kwa imani yake kwa kutambua kuwa kile Yesu angefanya ni kunena neno tu na mtumishi wake angepona. Yeye hakuelewa tu mamlaka, bali alijuwa umuhimu wa kunena Neno. Ikiwa tutanena Neno tu, hatuneni hisia zetu, au shaka, au kutokuamini.

Sikia Neno

Tumeamuriwa kuyasikia Maneno Yake.

Mitahli 4:20-22 Mwanangu, yasikie maneno yangu; yatege masikio yako kwa usemi wangu. Usiyaache yatoke machoni mwako; yaweke moyoni mwako; kwa kuwa ni maisha kwa wale wayapatayo na afya kwa mili yao.

Tuma Neno Lake

Katika Zaburi, tunapata kuwa Mungu alituma Neno Lake na kuwaponya.

Zaburi 107:20 Alituma Neno Lake na kuwaponya, na kuwakomboa kutoka maangamizi yao.

Tunayatuma maneno kwa kuyanena. Tunayo mamlaka ya Yesu. Tunaweza kulituma Neno la Mungu, kwa kulinena kwa imani na mamlaka.

Halitarejea Likiwa Tupu

Mungu ameahidi Neno Lake halitarudi bila matokea. Halitarudi likiwa tupu.

Isaya 55:10,11 kwa kuwa kama vile mvua ijapo, na theluji toka mbinguni, na havirudi kule, bali huleta maji ardhini, na kuleta mimea na maua, ili itoe mbegu kwa mpanzi na mkate kwa mlaji, vivyo hivo Neno Langu litokapo kinywani Mwangu; halitarudi kwangu likiwa tupu, litatimiza mapenzi yangu, na litadumu katika yale nimekusudia.

Tunaona kwa wazi kuwa Neno la Mungu lilipeanwa kwa kusudi na halitashindwa. Sehemu mojawapo ya Mungu ni kuleta uponyaji kwa mataifa. Sisi ni mikono na vinywa vya Mungu leo. Hebu na tuisikie sauti Yake, Tuyanene maneno Yake ya wokovu, na kuleta uponyaji kwa watu wake.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, nini unatarajia kutendeka unapolitumia jina la Yesu ukihudumu uponyaji kwa wagonjwa? Eleza kwa nini.

2. Kama ungeitwa kumwombea mtu ambaye daktari wamesema atakufa saratani, au akiwa na ugonjwa mwingine “usiotibika”, ungewahudumia vipi uponyaji?

3. Orodhesha mifano ya kibiblia ya kunena kwa nguvu katika huduma ya uponyaji.

Somo la Saba

Uponyaji Kupitia Vitendo na Maombi

Tumejifunza katika masomo yaliyopita kuwa ni muhimu kuelewa Neno la Mungu kama inavyohusika na kuwaponya wagonjwa. Lakini haijalishi kiasi gani tunajua, bila hatua kwa upande wetu, uponyaji hautafanyika. Ni lazima tunene imani yetu. Ni lazima tuchukue hatua. Lazima tuwafikie wagonjwa.

SEHEMU YA MUNGU – SEHEMU YETU

Ili miujiza ifanyike, ni lazima tuchukue hatua yetu na tumtarajie Mungu afanye Yake.

Nuu alijenga safina – Mungu alileta gharika.

Musa alinyosha fimbo – Mungu aligawanyisha maji.

Yoshua alitembea nje ya Kuta za Yeriko – Mungu alizivunja.

Elisha alitupa kijiti mtoni – Mungu alifanya shoka lielee.

Sehemu ya Mungu

Kwa kuhudumia uponyaji kwa wagonjwa, kuna hatua tunaitaji kuchukuwa, na kuna hatua ambayo Mungu atachukuwa. Ni muhimu kuelewa utaratibu huu wa pande mbili. Tunapoyaamini maneno ya Yesu na kuchukuwa hatua katika imani, Mungu atafanya sehemu yake na kuleta uponyaji.

➢ *Yote Yawezekana*

Ni rahisi kusema na Yesu, "Yote yanawezekana na Mungu!"

Luka 18:27 Lakini akasema, "Yasiyowezekana na kwa mwanadamu yanawezekana na mungu."

Mariko 10:27 Yesu aliwatazama na kusema, "Kwa mwanadamu haya haiwezekani, lakini kwa Mungu; yote yanawezekana."

Ni vigumu kukubaliana na Yesu aliposema, "Yote yanawezekana kwa yeyote anayeamini."

Mariko 9:23 Yesu alisema, "Ikiwa unaweza kuamini, yote yanawezekana kwa yeyote aaminiye."

Kwa kawaida, huenda haiwezekani. Lakini ikiwa Mungu amesema, inawezekana kutenda, sio kwa nguvu zetu, bali

kwa nguvu za Mungu. Mungu hawezi kamwe kutuambia kufanya kitu tusichoweza.

Matayo 17:20 ... amini, nawaambia, ukiwa na imani kama mbegu ya haradali, utasema kwa mlima huu, 'ngoka kutoka hapa hadi pale,' na itasonga; na hakuna kisichowezekana kwenu.

Sehemu Yetu

➢ *Kuwa Mtiifu*

Yesu alituamuru kuwekelea mikono juu ya wagonjwa. Tusiruhusu hofu itufanye tukose kutii amri hii!

1 Samueli 15:22 Kisha Samueli akasema: "Je, Bwana anafurahia dhabihu ya kuchomwa moto na sadaka, kuliko kuitii sauti ya BWANA? Tazama, kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia bora kuliko kondoo aliyenona."

Ikiwa tutaona miujiza ya uponyaji maishani mwetu, ni lazima tuwe watiifu kwa maagizo na amri ya Neno la Mungu. Lazima tuwe wepesi katika kutii chochote Roho Mtakatifu anatuamuru kutenda, hata kama ni ovyo.

➢ *Kuendeleza Tabia ya "Ninaweza Fanya"*

Tunaweza kufanya chochote Mungu anatuamuru kuendeleza imani yetu; ikiwa tutakoma kusema, "siwezi!" na kuanza kukubaliana na Neno la Mungu kusema, "Naweza!"

Wafilipi 4:13 Ninaweza kufanya kila kitu kupitia Kristo anipaye nguvu.

➢ *Kuipinga Hofu*

Hofu au woga haitoki kwa Mungu. Itatuzuia kufanya yote ambayo Mungu ametupangia maishani. Hofu isiyo ya kawaida inatoka kwa Shetani kutuzuia katika kumtii Mungu.

2 Timotheo 1:7 Kwa kuwa Mungu hakutupa roho wa hofu, bali wa nguvu na upendo na akili timamu.

Kutimiza Neno la Mungu, lazima tuishinde roho wa kushindwa, na kuwa na hofu juu ya heshima yetu iwapo mwujiza hautafanyika. Ikiwa Yesu aliacha heshima Yake kwa ajili yetu, kwa nini tushughulikie hali zetu?

Wafilipi 2:7 Lakini Yeye mwenyewe akashushwa cheo na kuwa mtumishi, na kuja katika umbo la mwanadamu.

Usijiulize, "Je, pasipofanyika kitu?" Uliza badala yake, "Je, nikitii na wapokee uponyaji?"

TEMBEA KATIKA IMANI SIO HISIA

Hisia za hofu, uwoga, kutokutosheleza vimewazuia wengi kupokea uponyaji wao wenyewe, au kutembea katika imani na kuwahudumia wengine uponyaji. Hatuwezi kutenda katika hofu na imani wakati mmoja.

Kama waamini, tunaitajika kuishi katika roho. Fikira zetu sharti zifanywe upya kwa ufunuo wa Neno la Mungu. Matendo yetu sharti yawe yenye kumtii kile Mungu ametufunulia katika Neno Lake na kunena katika roho zetu.

Nafsi zetu zinaporejeshwa, hisia na fikira vitaitikia kwa kutii roho wetu na wala sio kwa ustadi kinyume wa awali. Shetani kamwe hatatuzuia kumtii Mungu.

Imani Katika Neno

Ikiwa tutamwamini Mungu kwa miujiza ya uponyaji, ni lazima kwanza tufahamu kutoka kwa Neno la Mungu kile alisema atafanya.

➥ **Imani:**

- ➢ kamwe sio hisia na hisia kamwe si imani
- ➢ haina uhusiano wowote na hisia – hupuuza hisia
- ➢ huja kupitia Neno la Mungu
- ➢ hufahamu, kuamini, na hupokea yote ambayo Mungu amewyafunua katika Neno Lake

Hisia, “Nimechoka sana.” “Sijui njia ipi ... Labda nitashindwa.” “Nimejaribu kufanya hivyo awali lakini ...” “Nitafanya, lakini unaelewa sina ujasiri ....”

Imani husema, “Nitaamini na kutenda katika Neno la Mungu” “Nitaamini na kupokea” “Sitashuku na kutenda bila!”

Mtu anawweza kupokea uponyaji wao kwa nguvu za Mungu na asihisi kitu. Mwingine anaweza kuhisi msisimko wa nguvu za uponyaji wa Mungu, joto, ubaridi, au mshituko kama wa umeme.

Kwa ajili ya uponyaji, mtu asitafute hisia, lakini tafuta, amini, na utarajie matokeo ya ahadi.

LITENDE NENO LA MUNGU

Yesu alihudumu kwa Ujasiri

Yesu mara nyingi aliponya akitumia ujasiri fulani.

➢ *"Nyosha Mkono"*

Yesu alimponya mtu mwenye mkono uliopinda kwa kumwamuru afanye kitu ambacho hangefanya.

Matayo 12:10a,13 Tazama, palikuwa mtu mmoja aliyekuwa na mkono uliopinda ...

Kisha akamwambi, "Nyosha mkono wako." Naye akaunyosha, nao ukawa sawa kama ule mwingine.

Hadithi hii pia imeelezwa katika Mariko 3:1-5, na Luka 6:6-10. Maandiko haya yanazungumzia vitendo. Yesu alimwamuru yule mtu afanye kitu. Mtu huyo akafanya kile Yesu alisema, akanyosha mkono wake. Kwa kufanya kile Yesu alisema, aliponywa.

➢ *"Nenda Ukaoshe"*

Yesu alimponya mtu kipofu kwa kumwambia aoshe kwenye bwawa fulani.

Yohana 9:6,7 Baada ya kusema haya, akatema mate ardhini, akatengeneza tope kwa mate na kumpaka yule mtu kipofu machoni. Kisha akamwambia, "Nenda ukanawe katika bwawa la Siloamu (maana yake aliyetumwa). Basi akaenda akaosha, na akarudi huku akiona.

Je, mtu huyo alipata kuona Yesu alipotengeneza tope na kumpaka macho, au aliponawa katika bwawa?

Mtu huyo alipata kuona alipoamini, akamtii Mungu na kutekeleza imani.

➢ *"Chukua Kitanda Chako"*

Yesu amlimwamuru mtu aliyepooza, "Inuka, chukua kitanda na uende."

Mariko 2:11,12 "Nakwambia, inuka, chukua kitanda chako na uende nyumbani kwako."

Yule mtu aliyekuwa amepooza akainuka, akachukua kitanda chake akatembea machoni pao wote, jambo hili likawashangaza, wakamtukuza Mungu, wakisema,, "Hatujapata kuona jambo kama hili kamwe!"

Kwa kawaida, haikuwezekana kwa mtu huyo kusimama, kuchukua kitanda chake, na kuenda popote! Lakini alijua kile Mungu alisema. Aliifuata na kisha akapona.

Wanafunzi Walifuata Mfano

Petro na Yohana and John followed the example of healing that Jesus had given. They commanded the crippled man to rise and walk.

Matendo 3:6,7 Kisha Petro akasema, "Fedha na dhahabu sina, lakini kile nilicho nacho nakupa: katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti, inuka na utembee."

Akamchukua kwa mkono wa kuume na kumwinua, na punde miguu na mifupa ikapata nguvu.

Imani Ukiongeza Matendo

Yakobo anatwambia kuwa imani bila matendo imekufa.

Yakobo 2:14,17,18,20 Ndugu zangu, yafaa nini ikiwa mtu atadai kuwa na imani lakini hana matendo? Je, imani kama hiyo yaweza kumwokoa?

Vivyo hivyo, imani peke yake bila ya kuambatana na matendo imekufa.

Lakini mtu mwingine atasema, "Wewe unayo imani, mimi ninayo matendo." Nionyeshe imani yako pasipo matendo nami nitakuonyesha imani yangu kwa matendo.

Je, wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani bila matenda haifai kitu?

Inatupasa kufuata Neno la Mungu, kwa kuwa imani bila matendo imekufa. Imani yetu inapoingia katika matendo, tunaachilia nguvu ya Mungu ya uponyaji. Nguvu ya Mungu inapoachiliwa kupita katika matendo, ugonjwa lazima uondoke.

Imani-matendo ni muhimu katika kuwahudumia wagonjwa. Wakati mwingine itakuwa kwa yule anayehudumu uponyaji. Wakati mwingine, kitendo kitakuwa juu ya mtarajiwa wa imani na kutii maagizo.

Mapendekezo ya Hatua

Punde uonapohudumu uponyaji kwa mtu, wambie wafanye kitu hawangeweza awali. Kwa mfano:

- ➢ "Songesha mkono huo" – "Inama" – "Iangalie"
- ➢ Kwa ujasiri uliza, "Nini kilifanyika kwa maumivu?"

➥ **Unaamini Neno la Mungu ni kweli! Tenda hivyo! Fuata Neno la Mungu. Fuata kiwango cha imani yako.**

- ➢ Imani huingia katika matendo.
- ➢ Nguvu ya Mungu ya uponyaji huachiliwa.
- ➢ Uponyaji huja!

➢ *Tahadhari!*

Tusiwai mwambia mtu atoe kifaa cha daktari, au aache kutumia dawa, hata kwa kushawishi. Hatujui mahali imani ya mtu huyo ipo, hata kama wanazo pingamizi maishani mwao ambazo huenda ziwazuie kupokea uponyaji.

Tunaitajika kunena kwa sifa ili imani yao iinuke ndani yao. Ikiwa wanayo imani kutoa kifaa cha daktari hiyo itakuwa bora!

Kumbuka: Unaweza kuhukumiwa kisheria kwa ajili ya matokeo ya sasa, au baadaye, matokeo ya kinyume kutokana na hatua na maagizo yako ambayo ni kinyume na maagizo ya madaktari.

KUELEWA MAOMBI NA UPONYAJI

Mawazo Potovu

Kuna mawazo potovu kuhusu maombi, na sehemu yake katika kuhudumu uponyaji kwa wagonjwa. Wengine husema tunatakiwa kuomba na kuuliza, au hata kumsihi Mungu kana kwamba hataki kuponya. Wanajikuta wakimpa Mungu sababu za kumponya mtu. Kwa mfano, "Yeye ni kiongozi katika jamii ya Wakristo … Yeye ni mtu mzuri, ni lazima umponye."

Mungu hasiti kuponya! Yeye alifanya sehemu Yake miaka elfu mbili iliyopita, wakati Yesu alibeba mateso yetu na magonjwa kwa mapigo mwilini Mwake. Sasa, ametwambia tufanye yale alifanya; kuwaponya wagonjwa na kufufua wafu; kuweka mikono yetu kwa wagonjwa nao watapona!

Tamaduni zetu huenda zinataka tuwe na mistari ya maombi ili kuombea wagonjwa, lakini Mungu aliwambia waponywe.

Mbali na Yakobo 5:14 na 15, ambapo wagonjwa wanaweza kuwaita wazee wa kanisa ili kuwapaka mafuta na maombi na maombi yatolewe kwa imani yataponya mgonjwa, hatuna mifano yoyote ya uponyaji baada ya siku ya Pentekote na waamini "wakiwaombea wagonjwa."

Maana ya Maombi

Maombi isiwe mbinu ya kumsihi Mungu atufanyie kitu.

➥ **Maombi huonyesha imani katika Neno la Mungu, uwezo wa kutenda Neno Lake, na kukubali kuwa kile Mungu ameahidi, atafanya.**

Tunapoomba Neno la Mungu, matumaini yetu huwa imani, na imani yetu hutuelekeza kumtii Mungu kwa imani-iliyojaa matendo. Tunapoomba kwa imani, tunaanza kupokea yale Mungu amesema ni yetu. Tunaanza kutenda kazi ya Yesu. Maombi huachilia imani katika matokeo bora.

Maombi, kama ishara ya imani katika Neno la Mungu, ni wakati wa kusikia kutoka kwa Mungu na hutuandaa kwa nyakati za huduma tunapowaponya wagonjwa katika kulitii Neno la Mungu.

MAOMBI YA MAKUBALIANO

Wawili Wanakubaliana

wazo la maandiko kuhusu makubaliano katika maombi ni kanuni muhimu kwetu kuelewa na kufanya uponyaji.

Matayo 18:19,20 Tena nawambia ikiwa wawili kati yenu watakubaliana duniani kuhusu chochote watakachouliza, kitafanyika na Baba yangu wa mbunguni. Kwa kuwa palipo wawili au watatu katika jina Langu, niko kati yao.

Makubaliano

Unapokubali, umeunganika na mtu mwingine. Mahali wawili wameungana, na wanaamini katika jina la Yesu kwa uponyaji, maombi hujibiwa kwa sababu Mungu yuko pale!

Pia kuna nguvu zaidi tunapoomba tukikubaliana na mtu mwingine.

Yoshua 23:10 Mmoja wenu atapigana na maelfu, kwa kuwa BWANA Mungu wenu ndiye huwapigania, kama alivyowaahidi.

Kumbukumbu 32:30a Je, vipi mmoja anaweza kupigana na elfu, nao wawili hushida elfu kumi ...

Tunaitaji wengine. Kumbuka, mmoja anaweza kufukuza elfu, lakini wawili wanaweza kushinda elfu kumi. Maombi ya makubaliano inaweza kuongeza manufaa mara kumi.

Ikiwezekana, tunatakiwa kuijenga imani ya mgonjwa kwa kuwafundisha Neno la Mungu kwa ajili ya uponyaji ili kufikia katika makubaliano nasi.

Kuna hali zingine ambapo mtu ni mgonjwa sana asiweze kupata kweli katika Biblia kuhusu uponyaji, au hata kulisikia Neno la Mungu, na ni katika hali kama hizi ambapo waamini wawili wanaweza kukubaliana kimaombi ya mtu huyo.

Tunapokubaliana pamoja, imani yetu huzidisha na matokea yetu katika huduma huongezeka.

MAOMBI YA IMANI

Imani Katika Neno la Mungu

Maombi ni nguzo muhimu katika huduma. Maombi yetu ni sharti iwe na manufaa na wala sio kushawishi. Kuomba maombi ya imani mara nyingi ni ufunguo wa nguvu kwa matokeo makubwa.

➥ **Maombi ya imani ni kuomba kwa makubaliano na kweli, amri, na ahadi za Mungu. Maombi ya imani hutazama katika ulimwengu usioonekana na huesabia kuwa imetikika. Maombi ya imani huleta matokeo.**

Yakobo 5:14,15 Je, kuna yeyote miongoni mwenu aliye mgonjwa? Basi inampasa awaite wazee wa kanisa wamwombee na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana.

Kule kuomba kwa imani kutamwokoa huyo mgonjwa, naye Bwana atamwinua, na kama ametenda dhambi atasamehewa.

Mariko 11:22-24 Yesu akajibu akiwambia, "Kuwa na imani katika Mungu. Kwa hakika, nawambia, yeyote atakayeambia mlima huu, 'ondoka hadi baharini,' na asiwe na shaka moyoni mwake, lakini aamini kuwa mambo yale asemayo yatatimika, atapokea. Basi nawambia, chochote utakachouliza ukiomba, amini kuwa umepokea, na utapokea."

Adui wa Imani

Adui wa imani hupatikana katika fikira zetu ambazo hazijaumbwa upya. Hatuwezi kutenda katika roho na kwa maarifa yetukwa wakati mmoja.

➢ *Kutokusamehe*

Hapatakuwa na maombi ya kufana ikiwa tunakosa kusamehe maishani mwetu. Kutokusamehe ni kisuizi kati yetu na Mungu. Hatuwezi kosa kusamehe na kutenda imani wakati mmoja.

Mariko 11:25 Chochote mnaomba, ikiwa una kitu dhidi ya mtu yeyote, msamehe, ili Baba yako wa mbinguni atakusamehe makosa yako.

➢ *Kutokuamini*

Kutokuamini ni kinyume na imani. Maombi ya imani "huamini kuwa umepokea." Kutokuamini hutuzuia kupokea kile Mungu ametufanyia.

Imani ya haitegemei ushuhuda wa mtu ingawa shuhuda hakika ni mojawapo ya tunaweza kujenga imani yetu. Imani ya kweli huegemea Neno la Mungu.

➢ *Shaka*

Shaka pia ni kinyume cha imani. Maombi ya imani hayawezi kutolewa kwa uponyaji ikiwa utakuwa na shaka kuwa ni mapenzi ya Mungu kuponya. Mafundisho yali kinyume na Neno la Mungu huleta kutokuamini na mashaka.

Ikiwa ni mapenzi ya Mungu tuwe wagonjwa, basi si itakuwa makosa kuomba maombi ya uponyaji? Pia si itakuwa makosa kutafuta msaada kutoka kwa wataalamu wa matibabu, au kupata dawa?

Ikiwa Mungu anataka tuwe wagonjwa maka adhabu, au kutufunza kitu, au kujipa utukufu Mwenyewe, basi si tukubali kuwa wagonjwa na tusifanye chochote kuzuia mapenzi ya Mungu?

Msifu Mungu! Yeye hakusema alitaka tuteseke ugonjwa kwa ajili Yake, Yeye alisema aliteswa katika magonjwa, maumivu, na mateso kwa ajili yetu!

Matokeo ya Mara Moja?

Je, maombi ya imani kila mara huleta matokeo ya ghafla, yanayoonekana?

Ikiwa hatuoni matokeo ya ghafla tunapoomba kwa imani, bado tunaamini kuwa tumepata. Neno la Mungu ni la kweli. Ni juu yetu kuamini bila kutilia shaka, kumtii Yeye atoe dalili zote za magonjwa. Mara nyingi, tunaona uponyaji kwa muda fulani badala ya mwujiza wa ghafla.

Maombi ya imani ni sehemu muhimu katika mpango wa uponyaji. Tunapokubaliana na Neno la Mungu na kulifuata kama la kweli, milima mikuu itahama.

Badala ya kuangalia dalili za kinyume zinazobakia, anza kusifu Mungu ukijua kuwa Neno Lake ni la kweli. Anza kumsifu Yeye kwa matokeo yoyote mazuri katika dalili, hata yakiwa madogo. Usitupe ujasiri wako. Endelea kuamini na kupokea hadi matokeo kamili yatakapofika.

KULIOMBA NENO

Ufafanuzu

➥ **Kuliomba Neno maana yake kuchukua Maandiko yenyewe na kuomba ukimrudishia Mungu, lakini yabadili Maandiko na kuyafanya binafsi. Hii huachilia imani yetu kwa Mungu atende yale amesema. Kwa mfano,**

Baba, uliandika katika Isaya 53:5 kuwa Yesu alijeruhiwa kwa ajili ya dhambi zangu, aliteswa ajili yangu: kwa ajili ya

amani yangu; na kwa mapigo Yake nimepona. Sasa ninaamini kuwa unamaanisha kile uliandika. Nimepona!

Take God's Words with you as you go to Him in prayer.

Waefeso 6:17,18a Vaeni chepeo ya wokovu, na upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. Mkiomba kila mara kwa maombi yote na kuuliza katika Roho ...

Upanga wa Roho ni Neno la Mungu. Hebu na tuchukue silaha ambazo tumepewa na tumshinde Shetani. Tunapoomba Neno, tutakuwa na uhakika kuwa tunaomba na kukubaliana na Mungu.

Maombi ya Kufana

Kuomba Neno la Mungu na kukubaliana ni sehemu muhimu katika kufanya kazi ya Yesu na kuwahudumia wagonjwa uponyaji.

Mariko 1:35 Sasa alfajiri, baada ya kuamka mapema, Yeye akaenda mahali pa kutengwa; na hapo akaomba.

Yakobo 5:16 Kwa hiyo ungamianeni makosa yenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu tena yanafaa sana.

KUOMBA KWA MAAGIZO

Tutafaulu zaidi kuombeana, iwapo tutachukua muda kwanza kumwuliza Mungu kwa maagizo Yake jinsi tunaweza kuomba au kuhudumu uponyaji. Tunao mfano wakati Paulo alihudumu katika kiziwa cha Malta.

Matendo 28:8 Baba yake Pablio alikuwa mgonjwa kitandani, akiwa anaumwa homa na kuhara damu. Paulo akaingia ndani ili kumwona na baada ya maombi, akaweka mikono juu yake na kumponya.

Kwa nini Biblia inaweka wazi kuwa Paulo alihudumu uponyaji kwa mtu huyu baada ya maombi? Inaonekana kuwa maombi hayo yalikuwa kusikia kutoka kwa Mungu – kupata maagizo maalum kuhusu jinsi ya fulani ya kuhudumu. Katika kutii, Paulo alimwekelea mikono na kumponya.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza sehemu yetu na ya Mungu katika kuwaponya wagonjwa.

2. Eleza jinsi unaweza kulihuzisha Neno la Mungu katika maombi.

3. Eleza ombi la makubaliano na ombi la imani, na utaje jinsi maombi mazuri yanaweza kukufanya ufaulu katika huduma kwa wagonjwa.

Somo la Nane

Uponyaji Kutoka Ndani Nje

Neno la Mungu linaonyesha kweli – afya na uponyaji wa mili yetu hutegemea afya na uponyaji wa nafsi zetu. Utafiti wa wataalamu wa kiafya umeonyesha kuwa kutokusamehe, kukataliwa, hasira, na chuki vinaweza kusababisha magonjwa kama vile kifua kikuu, na saratani.

Funga Mlango!

Tabia ya kinyume akilini au hisia, husababisha mlango wazi, kwa ibilisi kuweza kupiga mili yetu.

Waefeso 4:26,27 "Kasirikeni, na wala usitende dhambi": usiache jua litue ukiwa na hasira yako, au kutoa nafasi kwa ibilisi.

Mara nyingi ugonjwa unaoonekana ni dalili ya mateso yaliyo ndani, katika nafsi ya mtu. Kwa kuwasamehe wale waliokataa, kusaliti, au kutujeruhi, kwa kuwa na fikira zetu zikifanywa upya kwa Neno la Mungu, na nyoyo zetu kurejeshwa kwa nguvu ya Mungu ya uponyaji, tunaweza kufunga milango hii na kutoa haki ya Shetani ya kupiga mili yetu.

Kutokusamehewa na mawazo mengine kinyume ni pingamizi kwa mtu kuweza kupokea uponyaji katika mwili wao. Hata wale wanaopata uponyaji wa kimwili wanaweza kupoteza uponyaji wao ikiwa watakataa kuwasamehe waliowakosea.

Mara mtu anapomtii Mungu na kuwasamehe waliomkosea, wanakuta inakuwa rahisi kupokea na kulinda uponyaji huo. Tunaita hii kuponywa kutoka ndani nje!

Mtume Yohana aliandika,
3 Yohana 2 Wapendwa, omba kuwa mfaulu katika mambo yote na muwe na afya, kama vile nafsi zenu hufaulu.

KUELEWA NAFSI

Kwa kuwa afya ya mwili na maendeleo vinategemea afya ya nafsi, ni muhimu kuelewa zaidi kuhusu nafsi.

➥ **Nafsi ni sehemu yetu ambayo inagusia fikira za kuzaliwa na jinsi ya kuitikia katika mtazamo wa kiakili na hisia. Inajumlisha:**

- ➢ Fahamu zetu – sehemu inayowaza na kufikiria
- ➢ Hisia zetu – hisia ambazo huitikia fahamu setu
- ➢ Uamuzi wetu – uwezo wa kuchagua kufanya uamuzi

Roho, Nafsi na Mwili

Ili kuelewa nafsi zetu, ni lazima tuitofautishe na mili yetu. Tuliumbwa katika utatu, na inachukua kila moja ya sehemu hizi kuikamilisha kuwepo kwetu.

Kabla ya kuzaliwa kwetu, tulkuwa tumekufa kiroho. Roho zetu hazikutenda kwa ajili ya dhambi. Wakati wa wokovu, tulifanyika hai kiroho kama viumbe wapya katika Yesu Kristo. Mili yetu inaweza kutajwa kama nyumba ya nafsi zetu na roho zetu. Kwa maneno mepesi tunaweza kusema:

- ➢ Sisi tu roho.
- ➢ Tunayo nafsi.
- ➢ Tunaishi katika mwili.

Roho zetu zilizozaliwa upya, zina uhai wa Mungu ndani yake. Roho zetu ni sehemu yetu ambayo inamjali Mungu na inaweza kushiriki Naye na kumwabudu Yeye. Kama viumbe wapya, roho zetu ni takatifu, zenye haki, bila lawama na kamili kama zinavyotakiwa.

Wokovu wa Nafsi Zetu

Kwa sababu ya mateso yanayotokana na maisha ya awali, nafsi zetu, kama mili yetu, inaitaji uponyaji. Fikira zetu zinaitaji kufanywa upya kwa Neno la Mungu. Hisia zetu zinaitaji kuponywa kwa kuwasamehe wale waliotutesa na kwa kupokea nguvu za uponyaji wa Mungu. Uamuzi wetu lazima utii Bwana Yesu.

Petro aliita mpango huu wa uanafunzi wa imani, wokovu wa nafsi zetu.

1 Petro 1:9 Kupokea mwisho wa imani yetu – wokovu wa nafsi zetu.

Ni mpango wa ustadi wa kufanywa safi, wa kutengwa kwa ajili ya Mungu, ambayo ni kuleta nafsi zetu na mili zaidi katika mahali pa kuwa kamili kama roho zetu.

1 Wathesalonike 5:23 Sasa na Mungu wa amani Mwenyewe awaoshe kabisa; na roho yako yote, nafsi, na mwili view bila lawama ajapo Bwana Yesu Kristo.

MATESO YA NAFSI

Chanzo Cha Mateso

Kuna njia nyingi ya mateso ambayo yanapiga vita nafsi zetu. Kwa sababu wazazi wetu, dada, ndugu, au majamaa hakuwa wakamilifu, sote tuliteswa kifikira, kimwili, au kijinsia tulipkua. Mateso mengine mengi yametokana na kukataliwa, au hisia za kukataliwa. Wengine hawakupendwa, au kusalitiwa na na jamaa au marafiki.

Daudi aliandika,
Zaburi 34:19 Mateso ni mengi kwa mwenye haki, lakini BWANA humkomboa kutoka yote.

Yakobo 5:13 Je, kuna yeyote miongoni mwenu mwenye mateso? Basi na aombe. Je, mwenye furaha? Naye aimbe zaburi.

➢ *Tabia za Wazazi Mbaya*

Tabia mbaya za wazazi zinaweza kuiharibu nafsi na kumletea mtoto taabu wakati huo na siku za usoni.

Waefeso 6:4 Nanyi, msiwachochee watoto wenu kwa hasira, lakini walee kwa kuwa funza na kuwaonya katika Bwana.

➢ *Usinzi*

Usinzi huaribu nafsi na huleta matatizo sio tu kwa wahusika bali wengine walio karibu nao.

Mithali 6:32-34 Lakini mwanaume aziniye na mwanamke hana akili kabisa; yeyote afanyaye hivyo hujiangamiza mwenyewe. Mapigo na aibu ni fungu lake na aibu yake haitafutika. Kwa maana wivu huamsha ghadhabu ya mume, naye hataonyesha huruma alipizapo kisasi.

➢ *Fikira za Dhambi*

Fikira za dhambi, kama vile tamaa, kupenda utajiri, ni adu wa nafsi.

1 Petro 2:11 Wapendwa, nawasihi kama wasafiri na wapitaji, jizuieni kutokana na tamaa iletayo vita dhidi ya nafsi.

➢ *Matendo Kidhambi*

Matendo ya kidhambi hufanya nafsi kuwa dhaifu.

Wagalatia 5:19-21 Basi matendo ya mwili ni dhahiri nayo ni haya: Uasherati, uchafu, ufisadi, kuabudu sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mambo mengine yanayofanana na hayo; nawaonya, kama nilivyokwisha kuwaonya kabla, kwamba watu watendao mambo kama hayo, hawataurithi ufalme wa mungu.

YEYE KUIREJESHA NAFSI YANGU

Tumekuwa tukifundisha juu ya uponyaji katika mwili, lakini je, kuna uponyaji wa nafsi zetu?

Maombi ya Mfalme Daudi

Daudi aliomba kwa ajili ya uponyaji wa nafsi.

Zaburi 41:4 Nikasema, "BWANA, nihurumie; iponye nafsi yangu, kwa kuwa nimetenda dhambi kinyume chako."

Nafsi ya Daudi iliharibiwa na dhambi yake mwenyewe.

Zaburi 6:1-4a Ewe BWANA, usinikemee katika hasira yako, au kuniadhibu kwa hasira yako kali, nionee huruma, ewe BWANA, kwa kuwa mimi ni mdhaifu; ewe BWANA niponye, kwa kuwa mifupa yangu inasumbuka. Nafsi yangu pia inateseka; lakini wewe ewe BWANA – kwa muda gani? Nirudie, ewe BWANA, ikomboe nafsi yangu...

Zaburi ishirini na tatu ni sura nzuri ya amani ambayo Mungu anataka katika kila hali. Tunaweza kufurahi na Daudi kwa kurejeshwa kwa nafsi.

Zaburi 23:1-3 BWANA ni mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu. Yeye hunilaza katika majani mabichi; ananiongoza kando ya maji matulivu. Yeye huirejesha nafsi yangu.

Nafsi Iliyotosheka

Kunayo ahadi maalum ya kuitosheleza nafsi.

Isaya 58:10,11 Nanyi kama mkimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi zenu na kutosheleza mahitaji ya walioonewa, ndipo nuru yenu itakapong'aa gizani, nao usiku wenu utakuwa kama adhuhuri. BWANA atakuongoza siku zote, atayatosheleza mahitaji yako katika nchi kame, naye ataitia nguvu mifupa yako; utakuwa kama bustani iliyonyweshwa vizuri, kama chemchemi ambayo maji yake hayakauki kamwe.

Isaya aliandika kuwa ikiwa tutajitolea kabisa kuwasaidia wengine, giza letu litafanyika mwanga. Bwana atatuongoza, kututia nguvu, na kutosheleza mahitaji ya nafsi zetu.

Yesu Huponya Waliovunjika Moyo

Yesu aliponya waliovunjika mioyo. Alisema,

Luka 4:18 "Roho wa Mungu yu juu yangu, kwa kuwa amenipaka kuihubiri injili kwa maskini. Amenituma kuponya waliovunjika mioyo, kuhubiri ukombozi kwa waliofungwa na kuondoa upofu kwa vipofu, kuwafungua wanaoteseka."

VITA VYA NDANI

Roho

Kabla ya wokovu, tulikuwa wafu kiroho. Nafsi na mili yetu ilitawala maisha yetu. Tulipozaliwa mara ya pili, tulizaliwa kwa Roho. Tulifanywa viumbe wapya – roho aishie.

Hadi nafsi zetu zeweze kuponywa na uamuzi wetu kufikia kumtii Yesu kama Bwana wa maisha yetu, bado kutakuwepo vita ndani yetu.

Mungu ni roho. Njia ya pekee ya kuwa na ushirika pamoja Naye ni kuishi na kutembea katika Roho.

Yohana 4:24 Mungu ni roho, na wale wanaomwabudu lazima wamwabudu katika roho na kweli.

Yohana 3:5,6 Yesu akajibu, "Hakika, nawaambia mtu asipozaliwa kwa maji na roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kile kzaliwacho kwa mwili ni mwili, na kile kizaliwacho kwa Roho ni roho."

2 Wakorintho 5:17 kwa hiyo, ikiwa yeyote aliye ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya: Ya kale yamepita; tazama, mambo yote yamekuwa mapya.

Mwili

Hata kama tumezaliwa upya na sasa tuko hai kiroho kama viumbe wapya, tunakuta kuwa miili yetu na nafsi bado zinataka kuyaongoza maisha yetu. Ni lazima tuchague kuishi na kutembea katika Roho.

Wagalatia 5:16,17,24,25 Basi nasema: Tembea katika Roho, na hautatimiza tamaa ya mwili. Kwa kuwa mwili hutamani dhidi ya Roho, na Roho dhidi ya mwili; na hawa hupingana, ili usifanye mambo usiyotaka.

Na wale walio wa Kristo wamesaliti mwili na tamaa na matakwa yake. Ikiwa tutaishi katika Roho, nasi tutembee katika Roho pia.

Tunapoweka uamuzi wetu kwa Yesu Kristo, tunaanza mpango wa kufa kwa dhambi. Hakika, tunasaliti mwili pamoja na tamaa na matakwa yake ili tuweze kuishi na kutembea katika Roho.

Ufahamu wa Kichwani

Ufahamu (sehemu ya nafsi) ya wale ambao hawajabadilishwa kwa kufanywa upya fikira na hawaelewi mambo ya Roho. Ni ujinga kwa akili ya kawaida.

1 Wakorintho 2:13,14 Mambo haya tunasema pia, sio kwa maneno hekima ya mwanadamu hufundisha bali kile Roho Mtakatifu hufundisha, kwa kulinganisha mambo ya kiroho na kiroho. Lakini mtu wa kawaida hawezi kupokea mambo ya Roho wa Mungu, kwa kuwa ni ujinga kwake; wala hawezi kuyajua, kwa kuwa yanakaguliwa kiroho.

Mambo ya kiroho, huchunguzwa kiroho si kwa ufahamu.

➢ *Kubadilishwa na Kufanywa Upya*

Ili tuwe chini ya roho zetu, fikira lazima zibadilishwe.

Warumi 12:1,2 Kwa hiyo, ndugu zangu nawasihi kwa rehema zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana. Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na ukamilifu.

Kando na nguvu ibadilishayo ya Roho Mtakatifu, saikolojia na ushawishi kila mara vitashindwa katika kufanya upya akili yao. Akili zetu haziwezi kufanywa upya kwa bidii yetu wenyewe katika kuangazia mateso ya awali kupitia mawazo ya mwanadamu. Mawazo kufanywa upya huafikiwa tu katika kazi iliyobadilishwa ya Roho Mtakatifu.

➥ **Fikira zetu zinaweza tu kufanywa upya kwa Neno la Mungu.**

➢ Kwa kusoma, kujifunza, na kutafakari juu ya Neno la Mungu kila siku.

- ➢ Kwa kuwasikia walimu waliojaa Neno la Mungu, na wanaofundisha kwa nguvu na ufunuo wa Roho Mtakatifu.
- ➢ Kwa kutafakari juju ya Neno hadi Neno lifanyike kweli kwetu kuliko shida.

Mfano wetu, ikiwa tuna uwoga, tunaweza kunukulu 2 Timotheo 1:7 na kulifanya binafsi.

Mungu hajanipa roho wa uwoga, bali wa nguvu, wa upendo na akili timamu.

Tunaposoma, kujifunza na kutafakari juu ya Neno la Mungu, Roho Mtakatifu atayadhihirisha mawazo yake kwetu katika roho zetu.

Isaya 55:8,9 "Kwa maana mawazo yangu si mawazo yako, wala njia zako njia Zangu," asema BWANA. "Kwa kuwa kama vile mbingu zilivyo juu zaidi ya dunia, basi pia njia zangu zilivyo juu ya njia zako, na fikira Zangu zilivyo juu ya fikira zako."

UPONYAJI WA NAFSI

Imani kwa Ajili ya Uponyaji

Mungu anapotufunulia fikira zake, imani huingia ndani ya roho zetu. Imani hii huachilia nguvu za Mungu kuponya na kurejesha nafsi zetu.

Imani hunena hivi:

- ➢ "Mimi siko tena chini ya hukumu wala makosa. Katika Yesu, ninayo haki ya Mungu ndani yangu!"
- ➢ "Sitazamii kuponywa baadaye. Neno la Mungu linasema, 'Kwa mapigo Yake tayari nimepona.' Ninaamini uponyaji kamili utaonekana sasa."
- ➢ "Mwili nna nafsi huingiana na Neno la Mungu! Mapenzi ya Mungu ni kuwa nitafaulu katika mambo yote na kuwa katika afya kama vile nafsi yangu inavyofaulu."

Kwa ajili ya kufaulu katika huduma kwetu na wengine, ni lazima ifanywe kwa imani, katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Msamaha wa Mungu Huleta Uponyaji

- ➢ *Wakati wa Wokovu*

Tulipozaliwa mara ya pili kupitia toba ya binafsi na imani katika Yesu Kristo, tulisamehewa dhambi zetu zote. Tulipokea haki Yake Mungu Mwenyewe. Kwa kutojua, wengi wameteswa na hisia za kutosamehewa na hukumu, bila kujua kuwa tayari wamesamehewa.

2 Wakorintho 5:21 Kwa kuwa alimfanya Yeye asiyejua dhambi awe dhambi kwetu, ili tufanyike haki ya Mungu ndani Yake.

Warumi 8:1 Basi sasa hakuna hukumu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu, wale hawatembei katika mwili, bali kulingana na Roho.

➢ *Baada ya Wokovu*

Baada ya kufanyika waamini, tukifanya dhambi, lazima tuwe wepesi kutupu, kuiacha dhambi hiyo, na kukiri kwa Mungu.

1 Yohana 1:9 Ikiwa tutakiri dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na mwenye haki kutusamehe dhambi zetu na kutuosha kutokana na makosa yote.

Huu ni msitari bora sana. Tukitenda dhambi, tunaitajika tu kuikiri dhambi hiyo Naye Mungu atatusamehe. Hii muhimu sana leo ambapo kuna watu wengi sana wanaokana dhambi kwa kusema,

"Mimi sikusababisha."

- ➢ "Ni jinsi nilivyo tendewa nikiwa mtoto."
- ➢ "Ni makosa ya mume/mke wangu."
- ➢ "Ni ujirani wangu."
- ➢ "Ni hali yangu ya kiuchumi."

Katika jamii zetu, tumejifunza kuona matendo yetu kama makosa ya mtu mwingine. Tumefundishwa kuwa tumetokana na mazingira yasiyo na msaada. Lakini hii haiambatani na Neno la Mungu.

Ni lazima tukubali yale tunafanya na kukubali kuyakiri kwa Mungu kama dhambi. Kwa imani, tunaweza kupokea hakikisho kamili kuwa tumesamehewa.

Kupitia Kuwasamehe Wengine

Kunazo sehemu tatu katika kutokusamehe:

- ➢ Wengine
- ➢ Sisi Wenyewe
- ➢ Mungu

Matayo 6:14,15 Kwa kuwa ukiwasamehe wanadamu makosa yao, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe. Lakini usipowasamehe watu makosa yao, nawe pia hautasamehewa makosa yako na Baba yako.

Tunapata uponyaji wa nafsi tunapowasamehe wengine. Kusamehe ni njia ya pekee ya kukamilisha hali fulani.

Mara nyingi tunawasikia watu wakisema vitu kama vile, "hawastahili kusamehewa," au "Hawajawai hata kukubali walifanya makosa!" Mungu hakuweka hii iwe kielelezo kabla ya kusamehe. Huenda wasione walifanya makosa. Labda hawataki kusamehewa. Yote haya yasilete tofauti yoyote kwetu.

➢ *Tunastahili Uhuru*

➥ **Hata kama wahusika hawastahili msamaha, tunaitajika kuwa huru na mateso hayo, na njia ya pekee kuwa huru ni kusamehe.**

Kwa mfano, ikiwa ulibakwa ukiwa mtoto aliyefanya huenda asikubali. Usishikile kuwa wanatakiwa kuadhibiwa, au kulipiza kisasi. Wala usishikilie haki yako ya kuteseka hisia.

Ikiwa hatutasamehe, tunaruhusu mtu huyo kutuumiza mara kwa mara, kila mwaka, kwa kumbukumbu inayoendelea kututesa. Tunajishikilia katika ngome mbaya sana jinsi tulivyoteseka mara ya kwanza.

➥ **Tunayo haki ya juu zaidi! Tunaitajika kuwa huru kwa matokeo ya kuteswa huko.**

Kwa hiyo wasamehe! Acha yote mikononi mwa Mungu, na kisha uende mbele katika maisha tele na kamili.

➢ *Ni Utiifu*

Yesu alituamuru kuwasamehe wengine.

Matayo 18:21,22 Kisha Petro akaja kwake na kumwambia, "Bwana, je, ni mara ngapi ndugu yangu atanikosea, nikimsamehe? Hadi mara saba?"

Yesu alimwambia, "Sikwambii, hadi mara saba, bali hadi sabini mara saba."

Waefeso 4:32 Na kuweni wakarimu mmoja kwa mwingine, wenye mioyo mikunjufu, mkisameheana, kama vile Mungu katika Kristo aliwasamehe.

Mariko 11:25 Na unaposimama kuomba, ikiwa umemkosea yeyote, wasamehe, na kuwa Baba yenu wa mbinguni aweze kukusamehe makosa yako pia. Lakini usiposamehewa, hata Baba yako wa mbinguni hatawasamehe makosa yenu.

Ni lazima tuwasamehe wengine katika kutuii amri ya Yesu. Tunaweza kusamehe kwa kuwa Yesu anayeishi ndani yetu alisamehe. Kusamehe si kitu ambacho tunaweza kufanya tukijisikia. Kusamehe ni uamuzi. Ni kitendo ambacho tunafanya katika kutii amri ya Mungu.

Kupitia Kusahau

Tunaweza kupata uponyaji wa nafsi zetu kwa kutokuwa na kulipiza kisasi.

Waefeso 4:26,27 "Kasirika, na wala usitende dhambi": usiache jua litue ukiwa na hasira yako, au kutoa nafasi kwa ibilisi.

Wafilipi 3:13 Ndugu zangu, sijihesabu kuwa nimekwisha kushika; lakini ninafanya jambo moja: ninasahau mambo yale yaliyopita, nakaza mwendo kufikia yale yaliyo mbele ...

Tunashikilia kutosamehe na hasira, tunatoa nafasi, au kufungua mlango kwa Shetani kutupiga kimwili, kifahamu, na ngome za hisia.

Baada ya msamaha, tunaweza kutoa nguvu ya uponyaji wa Yesu katika mioyo yetu iliyovunjika. Mioyo yetu iliyoteseka inaweza kuwekwa kukombolewa na kuwekwa huru.

Luka 4:18 Roho wa Mungu yu juu Yangu, kwa kuwa amenipaka ili nihubiri injili kwa maskini. Amenituma kuwaponya waliovunjika mioyo, kuhubiri ukombozi kwa wafungwa na kuwezesha vipofu kuona, kuwapa matumaini walioteseka ...

Tukiendelea kuongea juu ya mambo yaliyo kinyume na mateso yote yaliyopita, hali wasiwasi, na hatari bado vipo, huenda tuwe hatujamsamehe kila mtu aliyehusika, au tunamruhusu adui wa nafsi zetu kuweka "taka" yote juu yetu.

Baada ya kusamehe, tutaitaji kupigana na ukumbusho wetu kwa muda, lakini mwishowe, tutakuta hatukusamehe tu, bali tumesahau na kuyaacha mateso yote.

Pumziko na Marejesho

Tunaweza kupata uponyaji wa nafsi katika utulivu wa Mungu na marejesho. Mara nyingi nafsi huteswa na shughuli za kawaida kila siku. Tumekuwa na shughuli sana hatukupata muda na Mungu au kufanya yale tungependa kufanya.

Ingawa ni ngumu, tunaitaji kuangalia tena mambo tunayoipa uzito. Jifunze kusema hapana wakati umesukumwa kuchukua majukum mengi. Jifunze kumsikia Mungu na kufanya kile Anasema.

Yesu alisema,
Matayo 11:28,29 Njooni kwangu, enyi mlio na mizigo mikubwa, na nitawapumzisha. Chukueni nira yangu na kujifunza kutoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtulivu moyoni, na mtapata kupumzishwa nafsi zenu.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anazungumzia juu ya kuingia katika pumziko Lake.
Waebrania 4:1-3a Kwa hiyo, kwa kuwa ahadi inbakia kuingia katika pumziko Lake, na tuwe na hofu ili pasiwe mmoja wenu aliyepungukiwa na hiyo. Kwa kweli injili ilihubiriwa kwetu na pia kwao; lakini neno walilosikia halikuwafaidi, sio kwa kuchanganya na imani ya wale waliolisikia. Kwa kuwa sisi tulioamini tunaingia katika pumziko hiyo, kama alivyosema: "Niliapa kwa hasira Yangu, hawataingia katika pumziko langu."

Kwa imani na nidhamu-binafsi, tunaingia na kupokea wakati kwa wakati pumziko na amani kwa nafsi zetu.

Msifu Mungu kwa Uponyaji Wako

Nafsi zetu zinapoponywa, ni muhimu kuwa tunaanza kumbariki Bwana kwa sifa.

Zaburi 103:1-5 Mbariki BWANA, ewe nafsi yangu; na yote ndani yangu, libariki jina Lake takatifu! Mbariki BWANA ewe nafsi yangu, na usisahau matokeo yake mema: Nani anayetusamehe makosa yetu yote, nani aponyaye magonjwa yetu yote, nani akukomboaye kutokana na maangamizi, nani hukuvalisha upendo na huruma, anayetosheleza kinywa chako na mambo mazuri, ili ujana wako ufanywe upya kama tiwi.

Sifa huonyesha imani. Baada ya kumtii Mungu katika kila sehemu tuliyojifunza, kwa imani, tunauliza Mungu kwa uponyaji wa nafsi zetu, kuamini kuwa tumepokea uzima, nafsi na mwili.

Mariko 11:24 Kwa hiyo nawaambia, chochote unachouliza unapoomba, amini kuwa utavipokea, na utavipata.

➥ **Tunamsifu Mungu kuwa alileta uponyaji wa nafsi na mili yetu, ili kurejeshwa na kuwa jinsi alivyotuumba tuwe katika sura Yake – nafsi na mwili.**

Ni furaha ilioje kuwa tumeponywa kutoka ndani nje! Kwa kuwa nafsi yetu imepona, Shetani hana nafasi tena, hakuna mlango uliofunguliwa, au unaoweza kuweka magonjwa na maradhi juu ya mili yetu.

Tunaweza kuendelea kutembea katika afya. Tunaweza kuendelea kuwahudumia wengine uponyaji kwa ujasiri. Haya ni mapenzi ya Mungu! Hii ni haki yetu ya agano! Kweli, Yeye amejidhihirishwa kwetu kama Yehova Rafa, Bwana mponyaji wetu!

Kumbuka: Kwa mafundisho zaidi kwa somo hili soma Sura ya Kuumbwa Upya chake A.L. na Joyce Gill.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza kwa kina zile sehemu tatu za nafsi.

2. Kwa maneno yako mwenyewe, eleza vita kati ya nafsi na roho.

3. Eleza kwa kina jinsi ya kupokea uponyaji wa nafsi.

Somo la Tisa

Roho Mtakatifu na Vipawa Vyake

UTENDA KAZI WA ROHO MTAKATIFU

Mojawapo ya vipawa tisa vya Roho Mtakatifu katika 1 Wakorintho 12, ni kipawa cha uponyaji. Vinajulikana kama vipawa (wingi) kwa kuwa nyingi ya vipawa hutoka na kushirikiana tunapohudumu uponyaji.

Vipawa vya uponyaji huonekana wakati Roho Mtakatifu anapohudumu nguvu Yake ya uponyaji katika waamini-waliojazwa na Roho. Ni vipawa vyake, sio sisi. Sisi ni vyombo atumiavyo kutoa vipawa kwa wanaoitaji.

Tunapoingia katika uhusiano wa ndani, wa binafsi na Roho Mtakatifu, vipawa hivi vitatenda kazi kupitia sisi wakati tofauti panapotokea maitaji.

Mtu wa Utatu wa Mungu

➥ **Mungu ni mmoja, lakini anatambulika katika utatu. Kila mtu wa utatu wa Mungu yu sawa na anashiriki katika sifa za Mungu. Kila mmoja anadhihirishwa kando na wengine, na ana kazi yake tu na utu.**

Roho Mtakatifu, hata kama Baba na Mwana, hukazia uhusiano wa karibu na kila mwamini.

2 Wakorintho 13:14 Neema ya Bwana Yesu Kristo, na upendo Wake Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu uwe nanyi. Amina.

Paulo alitaja "Uhusiano wa karibu wa Roho Mtakatifu." Neno Uhusiano Kigiriki maana yake "Koinonia" na ina maana mapatano, au kuhusika. Sisi ni lazima tuwe wahusika na Roho Mtakatifu. Ni sharti tushiriki na kuhusika Naye.

Msaidizi na Mfariji

Katika injili ya Yohana, Roho Mtakatifu anajulikana kama msaidizi katika vifungu vine tofauti. Neno la awali la Kigiriki "Parakletos" maana yake kuitwa kwa upande wa mtu fulani. Inapendekeza kuingilia ili kutoa msaada kama mwombezi au mshauri.

Roho Mtakatifu ameitwa upande wetu kama msaidizi, kutembea nasi, kushirikiana nasi katika uhusiano wa karibu. Yeye hutuombea, kutufariji, na kututia moyo.

Yesu aliwashangaza wanafunzi wake aliposema ilikuwa kwa uzuri wao aende. Kwa maneno haya, aliweka wazi kuwa tunaitajika kujali, na kufurahia uhusiano wa karibu wa

uwepo wa Roho Mtakatifu kwa upande wetu kama vile Yesu ndiye anatembea kando yetu katika mwili.

Yohana 16:7 Lakini nawaambia ukweli. Ni kwa wema wenu niende; Kwa kuwa nisipoenda, Msaidizi hatakuja kwenu; lakini nikienda, nitamtuma kwenu.

Kulingana na maneno ya Yesu katika Yohana 14:15, Yohana 14:26, na Yohana 15:26 Roho Mtakatifu atatoa ushahidi kuhusu Yeye, atatufunza mambo yote, kuleta yote katika ukumbusho wetu, na kukaa nasi milele.

KUWEZA KUMFAHAMU YEYE

Hata tunapolinda kwa makini nyakati za uhusiano na Baba na Mwana katika kuabudu na maombi, inatupasa kulinda na kueshimu uwepo unaoendelea wa Roho Mtakatifu kwa kuwa Yeye yuko upande wetu akiwa msaidizi, mfariji, mshauri, mwalimu na mwelekezi.

Nguvu za Roho Mtakatifu ni mlipuko, ya ajabu, na inazidi kipimo. Lakini, Yeye pia ni mnyenyekevu sana, mlinzi, anayependa anayeweza kukasirishwa kwa utofauti, kutotii, na dhambi.

➢ *Anakaa Ndani Yetu*

Kwa kuwa Yesu likuwa hapa duniani kama mwanadamu, Yeye angekuwa sehemu moja tu kwa wakati mmoja. Je, inazidi kiasi kipi kwetu leo kwa kuwa Roho Mtakatifu na Yesu wanakaa ndani yetu wakati wote.

Yohana 14:16,17 Nami nitamwomba Baba, Naye atawapa ninyi msaidizi mwingine, kuwa Yeye aweze kukaa nanyi milele-Roho wa kweli, ambaye dunia haiwezi kumpokea, kwa kuwa hawamwoni Yeye au kumfahamu; lakini ninyi mwamjua, kwa kuwa anakaa nanyi naye atakuwa ndani yenu.

➢ *Hutufundisha Sisi*

Roho Mtakatifu ni Mwalimu wetu.

1 Wakorintho 2:13a mambo haya pia tunasema, sio tu kwa maneno ambayo hekima ya mwanadamu hufundisha lakini yale Roho Mtakatifu hufundisha, kulinganisha mambo ya kiroho na kiroho.

Ni Roho Mtakatifu ndiye atupaye maneno ya kusema nyakati za shida.

Luka 12:11,12 Sasa watakapowaleta kwa masinagogi na majaji na mbele ya mamlaka, usiwe na hofu juu ya jinsi au nini mtajibu, au kile mtasema. Kwa kuwa Roho Mtakatifu atawafundisha wakati huo huo kile mtasema.

➢ *Huleta Nguvu*

Nguvu tunayostahili kuwa nayo ni ile ya Roho Mtakatifu.

Matendo 1:8a Lakini mtapokea nguvu Roho Mtakatifu ajapo juu yenu ...

➢ *Huleta Ujasiri*

Roho Mtakatifu hutupa ujasiri.

Matendo 4:31b ... na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri.

➢ *Huleta Mwelekeo*

Hutupa mwelekeo.

Luka 2:26a Na ilidhihirishwa kwake na Roho Mtakatifu ...

Luka 4:1a Kisha Yesu, kwa kujazwa na Roho Mtakatifu, akatoka Yordani na akaongozwa na Roho Mtakatifu ...

Matendo 13:4a Kwa kutumwa na Roho Mtakatifu ...

Matendo 16:6b Walikanywa na Roho Mtakatifu ...

➢ *Huleta Upendo*

Roho Mtakatifu ndiye hufanya upendo wa Mungu wazi kwetu.

Warumi 5:5 Na sasa tumaini halitavunja moyo, kwa kuwa upendo wa Mungu umemwagwa kutoka mioyo yetu na Roho Mtakatifu ambaye tuliyepewa.

➢ *Haki, Amani na Furaha*

Kupitia Roho Mtakatifu, tunayo haki, amani na furaha.

Warumi 14:17 ... kwa kuwa ufalme wa Mungu sio kula na kunywa, bali haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu.

Hakikisho la Ukombozi

Roho Mtakatifu ni hakikisho la urithi wetu.

Waefeso 1:13,14 Katika Yeye pia mliamini, baada ya kulisikia neno la kweli, injili ya wokovu wako; katika yeye pia, baada ya kuamini, mlizibwa na Roho Mtakatifu wa ahadi, ambaye ni hakikisho la urithi wetu hadi ukombozi wa mali tuliyonunua, kwa sifa na utukufu Wake.

Waefeso 4:30 Na msimuhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, kwake mlizibwa naye kwa siku ya ukombozi.

Kuonekana Vipawa

Roho Mtakatifu ametupatia vipawa tofauti vya kiroho tisa. Nyingi ya vipawa hivi vinausika na kuponya wagonjwa. Sote tunaweza kujifunza kuhudumu katika vipawa hivi ili tufaulu katika huduma.

1 Wakorintho 12:1,7-10 Sasa kuhusu karama za rohoni, sitaki mkose kufahamu: Basi kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa faida ya

wote:
– kwa kuwa mtu mmoja kwa Roho hupewa neno la hekima,
– kwa mwingine neno la maarifa kwa Roho huyo huyo,
– mwingine imani na Roho huyo huyo,
– kwa mwingine karama za kuponya,
– kwa mwingine matendo ya miujiza,
– kwa mwingine unabii,
– kwa mwingine kupambanua roho,
–kwa mwingine aina mbalimbali ya lugha,
– kwa mwingine tafsiri za lugha.

Utenda kazi wa karama za Roho Mtakatifu maishani mwetu ni ishara ya uwepo Wake nasi. Tusizitumie kujijengea heshima na kiburi. Na ziweze kuonekana kwa kawaida, bila kuonyesha vituko, ili kuonyesha upendo wa Mungu kwa dunia itesekayo.

Katika sehemu za ushirika, tutajifunza karama sita za Roho Mtakatifu na kuonyesha jinsi inahusiana hasa na uponyaji.

KUTOFAUTISHA KATI YA ROHO

Ufafanuzi

➥ **Kutofautisha roho ni ufahamu usio wa kawaida katika ngome ya ulimwengu wa roho. Hii huonyesha aina ya roho, ndani ya mtu, hali, kitendo, au ujumbe. Ni ufahamu katika roho yetu unaokuja kwa ufunuo wa njia isiyokawaida kuhusu chanzo, asili, na kazi ya roho yoyote.**

Kuna sehemu tatu katika ulimwengu wa roho ambazo zinaweza kutofautishwa kupitia karama hii.
➢ Roho wa Mungu, au malaika
➢ Roho wa mwanadamu
➢ Shetani au roho wa pepo

Roho wa Maradhi

Mara nyingi, roho za pepo za maradhi huleta magonjwa au maradhi. Kwa mfano kuna roho za saratani, kifua kikuu, kukataliwa na hasira. Katika karama ya kiroho ya kubainisha roho, Roho Mtakatifu atadhihirisha, au kuonyesha chanzo cha shida, ili mtu akombolewe na kuponywa.

Luka 11:20 Lakini nikiwakemea pepo kwa kidole cha Mungu, hakika ufalme wa Mungu umekuja juu yenu.

Jinsi Karama Hufanya Kazi

Mtu anapoongozwa na Roho wa Mungu, karama ya kubaini roho itaonekana kwa dalili, au wazo, ambayo hutambua au jina la roho kama chanzo cha shida hiyo.

Matayo 9:32,33 Walipoenda nje, tazama, wakamleta mtu, bubu na mwenye pepo. Na baada ya pepo kutolewa, yule bubu akaongea. Na umati ukashangaa, wakisema, "Hii haijawaionekana Israeli!"

Ili kuenda katika ulimwengu wa roho na kupigana vita bora, tunaitaji kuelewa na kukubali kuongozwa na karama ya kubaini roho. Kwa karama hii, Roho Mtakatifu atatuongoza na kututia nguvu.

NENO LA MAARIFA

Definition

➥ **Neno la maarifa ni ufunuo wa Roho Mtakatifu kuhusu kweli fulani, za sasa au awali, kuhusu mtu au hali, ambazo hazipatikani kwa ufahamu wa fikira. Karama hii hutoa habari kutoka kwa Mungu ambayo haijulikani kiasili.**

Yesu na Mwanamke Msamaria

Katika hadithi ya mwanamke Msamaria, Yesu alijua kwa neno la maarifa kuwa yeye alikuwa na waume watano, na kuwa mumewe wa sasa hakuwa wake kindoa.

Yohana 4:18 ... kwa kuwa unao waume watano, na yule uliye naye sasa si mumeo; kwa hiyo ulisema kweli.

Maarifa kuhusu mwanamke huyu ilimjia Yesu si kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu, bali, alitembea kama Mwana wa Adamu kupitia karama ya Roho.

Neno la Maarifa kwa Uponyaji

Mara nyingi katika kuhudumu uponyaji, Mungu atakufunulia neno la maarifa kuhusu ugonjwa fulani. Wakati mwingine ni la mtu mmoja fulani, wakati mwingine kwa watu kadha.

Inaweza kutambulika kwa jina la ugonjwa, kwa sehemu ya maumivu, au kwa jina la sehemu ya mwili ambapo Mungu ataonyesha uponyaji Wake wakati huo.

Jinsi Inavyokuja

Neno la maarifa huja kwa njia aina nyingi unapohudumu.

- ➢ Kwa kuhisi hali isiyositarehe kama msukumo, mwamsho, au hisia fulani.
- ➢ Wakati mwingine unaweza kuhisi maumivu madogo.

Neno la maarifa linaweza kuwa neno, wazo, ambayo hueleza ugonjwa, maradhi, au maumivu.

- ➢ Jina la ugonjwa
- ➢ Jina la sehemu ya mwili iliyoadhirika

Neno la maarifa linaweza pia kuja kwa maono ya sehemu ya mwili inayoitaji uponyaji.

➢ *Mgonjwa Kujulikana*

Wakati mwingine, Mungu ataonyesha mahali fulani aliko mgonjwa, au mtu huyo ambayo uponyaji utamfikia. Hii wakati mwingine inatambulika kama mvuto (kama mnaso wa spaki) kuelekea sehemu ya chumba, kwa nafasi fulani, au pahali alipo mtu huyo.

Nyakati zingine hii inaweza kuja kama mwanga, au nuru, au hisia zingine zinazovuta usikivu wa mtu fulani.

Pia, Bwana atafunulia majina ya watu, au kutoa mbinu nyingine ya kutambua, itakayowahakikishia kuwa Roho Mtakatifu amewaona kwa ajili ya uponyaji.

➢ *Imani Huachiliwa*

Roho Mtakatifu anapofunua uponyaji fulani kwa neno la maarifa, na mtu huyo mara moja akakubali kuwa yeye, ndiye anayeelezwa, imani itaachiliwa, na uponyaji utaonekana.

➢ *Onyo Dhidi ya Roho Zijulikanazo*

Mtu aliye katika karama hii awe mwangalifu kuwa yeye anapokea kweli anapokea neno la Mungu la maarifa, na kuwa hasikilizi roho bandia. Njia moja rahisi ya kutofautisha uwepo wa roho zingine, ni kuchunguza anayepokea utukufu.

- ➢ Je, yule anayehudumu anaonyesha kujigamba na uwezo wake?
- ➢ Je, watu wanamtazama na kufrahia “sinema”?
- ➢ Je, utenda kazi wa neno la maarifa unawainua watazamaji kwa hali ya juu ya imani katika Mungu, au imani ya mtu anayewahudumia?

Roho Mtakatifu kamwe hataleta utukufu kwa kwa mtu, kila mara kwa Mungu!

➢ *Uwe Tayari Kuchukuwa Hatua*

Wakati mtu anayejifunza kuhudumu katika sehemu hii ya neno la maarifa anapokea ufunuo fulani kutoka kwa Mungu, anatakiwa kutoka kwa imani, na kunena neno.

- ➢ Tuwe tayari kuonekana wenye ujinga tukikosea.
- ➢ Tusirudi nyuma kwa hofu ya kushindwa.
- ➢ Tujifunze kuwa makini kwa Roho Mtakatifu.
- ➢ Tunatakiwa kumtii Mungu, kuchukua hatua ya imani, na mwache Mungu atukuzwe katika uponyaji.

NENO LA HEKIMA

Ufafanuzi

➥ **Neno la hekima, ni ufunuo wa ndani unaotolewa kwa mwamini. Ni hekima ya Mungu kuchukua hatua ya kutekeleza kulingana na maarifa ya asili. Inaonyesha mpango wa Mungu na kusudi Lake:**

- ➢ kwa maisha yetu na huduma
- ➢ kufanyika mara moja au wakati fulani baadaye
- ➢ juu ya jinsi tunaweza kumhudumia mtu maitaji fulani

neno la hekima huja kwatika njia nyingi, katika maono ukiwa macho, katika ndoto unapolala, kupitia karama za unenaji.

Katika Uponyaji

Neno la hekima hufanya kazi kwa karibu na karama ya kupambanua roho na neno la maarifa. Ni ufunuo wa jinsi ya kuhudumu kwa maitaji fulani.

Neno la hekima hutolewa kwa kulinda na kuagiza na kila mara huonyesha jinsi ya kutumia maarifa uliyopata katika neno la maarifa na kupambanua roho. Inaweza kutoa ufahamu kuhusu huduma kwa njia fulani.

Neno la hekima linaweza kutuagiza:

- ➢ kuwekelea mikono juu ya mtu
- ➢ nena neno
- ➢ utende mwujiza fulani
- ➢ kemea pepo

Neno la hekima hutupatia hekima ya kuhudumu katia karama za uponyaji. Inaleta imani ya kuhudumu kwa ujasiri.

KIPAWA CHA IMANI

Ufafanuzi

➥ **Kipawa cha imani asili yake sio kawaida na ni ya muda na kusudi maalum. Ni kipawa cha nguvu kutimiza kazi fulani katika hali yoyote uliyo ndani wakati huo.**

Si Ya Kawaida

Kipawa cha imani huja kwa isiyo kawaida na bila bidii yoyote kwa yule anayehudumu.

- ➢ Ni kipimo cha imani kwa kila mwamini.
- ➢ Ni imani inayokuja kwa kujifunza Neno la Mungu.
- ➢ Huja kwa njia isiyo kawaida kwa Roho Mtakatifu inapoitajika kwa mwujiza fulani.

➢ *Na Miujiza*

Kipawa cha imani mara nyingine hupewa wakati mwujiza unatakikana. Ghafla anayehudumu ataona katika Roho, sehemu ya mwili inayokosekana kirejea. Huu ni utenda kazi wa karama ya roho ya neno la hekima.

Mfano

Petro anaonekana alipewa karama ya imani alipomwambia kilema kwa ujasiri,

Fedha na dhahabu sina, lakini nilicho nacho nakupa wewe: Katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti, inuka na utembee (Matendo 3:6).

KUTENDA MIUJIZA

Ufafanuzi

➥ **Kutenda miujiza ni kazi isiyo kawaida katika hali ya kiasili. Hii huonyesha nguvu za Mungu ambazo sharia za asili zimeundwa, kuegemea au kuongozwa.**

Inapotumika kuleta urejesho katika njia ya miujiza kwa mwili, utenda kazi kama mojawapo ya karama za uponyaji.

Miujiza ya Kuundwa

Mara nyingi, viungo mwilini vinakosa kutokana na ajali, upasuaji, kuzaliwa na dosari, au ugonjwa. Labda, imani yetu haijakua kufikia mahali tunaweza kumwamini Mungu kwa ajili ya miujiza ya kuundwa maishani mwetu.

Imani tunayoitaji lazima itegemee maarifa yetu katika Neno la Mungu.

Neno Lililofunuliwa

Lazima tulisoma, kujifunza, na kutafakari kile Neno la Mungu linasema kuhusu miujiza. Lazima tufahamu kuwa yote yanawezekana na Mungu.

Matayo 19:26 Lakini Yesu akawatazama na kuwambia, "Kwa wanadamu haiwezekani, lakini kwa Mungu yote yanawezekana."

Yesu alihudumu kwa kutumia miujiza ya kuundwa.

Mariko 3:3,5b Kisha akamwambia mtu huyo mwenye mkono uliopooza, "Njoo mbele." Akamwambia, "Nyosha mkono wako." Kisha akaunyosha, nao mkono wake ukarejeshwa na kuwa sawa kama ule mwingine.

Tunajua kuwa Yesu alisema tutafanya matendo hayo aliyofanya. Tunaijua ahadi ya Yesu.

Mariko 9:23 Yesu akamwambia, "Ukiamini, yote yanawezekana kwa yule anayeamini."

Neno la Hekima – Kipawa cha Imani

Ghafla, neno la hekima kwa njia ya maono pendekezo huruka ndani ya roho zetu. Tunajiona tukihudumu mwujisa ya kubuni kwa mtu kwa njia fulani. Katika Roho tunaona mwujiza ukitendeka kabla tushuhudie ukifanyika.

Hapatakuwa tena na tatizo katika kuamini. Karama ya imani imekuja katika roho zetu. Imani yetu imepata nguvu na ujasiri kuwa mwujiza utatendeka.

Kutenda Miujiza

Tunaanza kutenda yale tayari tumejiona tukifanya katika Roho. Huu ni utendaji wa miujiza.

Tunaanza kunena na kuamuru mshipa mpya, au misuli ianze kurejea. Tunaumba kwa kutazamia mema imani yetu hadi mwujiza ukamilike.

Yesu Akitenda Kazi Nasi

Tunajua kuwa Yesu yu pale akitenda kazi nasi kama alivyokuwa na waamini wa awali.

Mariko 16:20 Na wakaenda nje kuhubiri kila mahali, Bwana akitenda pamoja nao na kuhakikisha neno kupitia ishara zilizowafuata.

KIPAWA CHA UPONYAJI

Ufafanuzi

➥ **Vipawa vya uponyaji nguvu za Mungu za hali ya juu za uponyaji kwa wale wanaoitaji uponyaji. Zinaelezwa kama vipawa (wingi) kwa kuwa baadhi ya vipawa hutokakana na kutenda pamoja kama vipawa vya uponyaji. Mtu anayepokea uponyaji amepokea vipawa vya uponyaji.**

Ni vya Hali ya juu

Vipawa vya uponyaji si sawa na sayansi ya kimatibabu. Luka, mwandishi wa vitabu vya Luka na Matendo, ni mfano bora. Akiwaandikia Wakolosai, Paulo alimtambua kama daktari.

Wakolosai 4:14 Luka daktari mpenzi ...

Luka alikuwa katika kisiwa cha Malta pamoja na Paulo, lakini hakuna palipotajwa kuwa wagonjwa walikuja kwake na wakaponywa.

Matendo 28:8,9 Baba yake Pablio alikuwa mgonjwa kitandani, akiwa anaumwa homa na kuhara damu. Paulo akaingia ndani ili kumwona na baada ya maombi, akaweka mikono juu yake na kumponya. Hii ilipofanyika, wote katika kisiwa waliokuwa na magonjwa pia wakaja na wakaponywa.

Hata kama daktari alikuwepo, alikuwa mtume Paulo ndiye aliwaponya watu kimiujiza.

> Kumbuka: tunapohudumu, tunataka kupima na kushirikiana na madaktari na sayansi ya kimatibabu. Wengi wetu tuko hai leo kwa sababu madaktari walituweka hai hadi imani yetu iweze kukua na nguvu ili tupokee uponyaji wetu. Lakini tofautisha kati ya sayansi ya matibabu na karama ya uponyaji.
>
> Usimwambie yeyote asiende kwa daktari wake au kuacha dawa. Wanapoponywa, hawataitaji dawa tena. Kwa kuwa daktari wao aliwaandikia dawa hizo, yeye tu lazima awambie wasichukue dawa tena!

Kusudi la Vipawa vya Uponyaji

Kuna kusudi tatu ya vipawa vya uponyaji:

- ➢ Kuwakomboa wagonjwa,
- ➢ Ili kuziharibu kazi za ibilisi katika miili ya wanadamu,
- ➢ Ili kutimiza ujumbe wa wokovu kwa ishara na miujiza.

Tunapokaribia uhusiano wa katibu na Roho Mtakatifu, karama za uponyaji na karama zingine za Roho Mtakatifu zitafanya kazi ndani yetu.

Kwa neno la maarifa, tunaweza kupokea maarifa yanayodhihirisha kuwa Mungu anataka kuponya mtu fulani

au ugonjwa. Karama ya kupambanua roho inaweza kudhihirisha chanzo cha pepo wa ugonjwa anayetakiwa kukemewa.

Kwa neno la hekima, tunapokea ufunuo wa ajabu kuhusu jinsi ya kumhudumia mtu huyo vizuri. Tunajiona sisi wenyewe tukifanya. Tunaona uponyaji au miujiza ikitendeka. Hii huachilia kipawa cha imani na tunaanza kwa ujasiri kuhudumu utendaji miujiza.

Tunapojifunza kuhudumu katika vipawa vyote vya Roho Mtakatifu na katika imani kutarajia kuonekana katika maisha yetu, tutagundua kuwa ni rahisi kufanya mwujiza kama vile kutoa ujumbe katika ndimi, au kutenda katika vipawa vingine vya Roho Mtakatifu.

Kumbuka: Kuishi Kusio kwa Kawaida katika Vipawa vya Roho Mtakatifu na A.L. Na Joyce Gill ni mafunzo ya undani zaidi ya vipawa vya Roho Mtakatifu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza kwa kina Roho Mtakatifu ni nani na hufanya nini maishani mwetu.

2. Je, kupambanua roho huwa na msaada gani unapowaombea wagonjwa?

3. Eleza utendaji wa neno la hekima na kipawa cha imani tunapohudumu uponyaji na miujiza.

Somo la Kumi

Kupokea na Kuifadhi Uponyaji Wako

Katika somo hili, tutajifunza vizuizi kwa uponyaji na jinsi ya kuifadhi uponyaji wako. Mara nyingi vitu ambavyo vitatuzuia kupata uponyaji ni vitu ambavyo, kama vingerejea vingewafanya watu kupoteza uponyaji wao.

Sehemu ya kwanza ya somo hili ni kutaja tena mambo ambayo tumejifunza. Ni wakati kuleta kweli hizi katika kipimo maishani mwetu.

VIZUIZI KWA UPONYAJI

Mtu asipopokea uponyaji, kunayo sababu. Mtu huyo achukue muda na Bwana akitafuta chanzo. Ni lazima awe makini asipokee lawama anapokuwa katika wakati huu wa kutafuta. Mungu hatoi lawama. Yeye hukosoa na kuagiza katika haki Yake anapotubadilisha katika sura ya Mwana Wake.

Ikiwa unamwamini Mungu kwa uponyaji sasa hivi, tia kikomo na umwulize Roho Mtakatifu akufunulie kwa nini hujapokea uponyaji. Chukua hatua haraka juu ya chochote Mungu anakufunulia unapoendelea na masomo haya.

Maswali ya Kujiuliza Wenyewe

➢ *Dhambi Isiyosamehewa*

➥ **Je, kunayo dhambi ambayo hujasamehewa iletayo kizuizi kati yangu na Mungu?**

Dhambi hujeruhi nafsi na hufungua mlango kwa roho wa maradhi kuleta magonjwa mwilini mwetu. Kukiri dhambi zijulikanazo kwa Mungu na kupokea msamaha ni muhimu ili kupata uponyaji.

Yakobo 5:15,16 Na maombi ya imani itamwokoa mgonjwa, naye Bwana atamwinua. Na ikiwa ametenda dhambi, atasamehewa. Kwa hiyo ungamianeni makosa yenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu tena yanafaa sana.

Dhambi isiyosamewa hufanya ugonjwa usalie. Shetani anaweza kujaribu kuficha dhambi hizi kwetu. Tunaweza kuwaza na kupuuza, lakini ugonjwa husalia. Ni lazima tukiri dhambi hii kwa Mungu na kupokea msamaha Wake.

Matayo 9:2,5-7 Na tazama, wakaleta kwake mtu aliyepooza akiwa kitandani. Naye Yesu, kuona imani yao, akamwambia aliyepooza, "Mwana, kuwa na furaha; dhambi zako zimesamehewa."

"Je, nini rahisi kusema, Dhambi zako zimesamehewa,' au kusema, 'Inuka na utembee?' Lakini mjue Mwana wa Adamu ana nguvu duniani kusamehe dhambi"-kisha akamwambia mtu aliyepooza, "Inuka, chukua kitanda chako, na uende nyumbani kwako."

Naye akaamka na kuenda zake nyumbani. Nao umati walipoona haya, walishangaa na kumtukuza Mungu aliyetoa nguvu kama hizo kwa wanadamu.

Ikiwa kuna dhambi yoyote maishani mwetu, tunatakiwa kukiri kwa Mungu na kupokea msamaha.

1 Yohana 1:9 Ikiwa tutakiri dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na mwenye haki kutusamehe dhambi zetu na kutuosha kutokana na makosa yote.

➢ *Kukosa Kuwasamehe Wengine*

➥ **Je, nimemsamehe kila mtu aliyenikosea? Je, nimejisamehe? Je, nimemsamehe Mungu?**

Kwa kuwahudumia watu kwa miaka, na kwa kuongea na wahudumu wengine, tumegundua kuwa kutosamehe ni chanzo cha msingi kwa mtu kukosa uponyaji.

Ni rahisi kuwasamehe wengine, kuliko kujisamehe. Tunawasikia watu wakisema vitu kama vile, "Nilikuwaje mjinga kiasi hicho. Kwa nini nilijiingiza katika hali hii?" mara nyingi tunawaruhusu wengine na kutarajia ukamilifu.

Jisamehe!

Mamabo mabaya yakifanyika, watu mara nyingi humlaumu Mungu. "kwa nini Mungu aliachilia hii ikanifanyikia? Yeye ni Mungu! angeikomesha!"

Ikiwa hii ni kweli katika hali yako, kiri hisia zako kwa Mungu bila kuficha. Tayari anajua jinsi unahisi.

Sema, "Mungu, nimeelewa vibaya. Ninajua wewe ni Mungu wa upendo. Najua unanipenda zaidi ya vile ninadhani. Sasa, natambua kuwa ni Shetani, na wala si wewe aliyeleta madhara haya maishani mwangu. Nimeshikilia haya dhidi Yako. Lakini sasa nakusamehe na kuachilia hisia za kinyume kwako."

Mariko 11:24,25 kwa hiyo nawaamabia, chochote mtakachouliza mkiomba, amini kuwa mmepokea, na mtapokea. Chochote mnaomba, ikiwa una kitu dhidi ya mtu yeyote, msamehe, ili Baba yako wa mbinguni atakusamehe makosa yako.

➢ *Kutokuwa wa Maana, Lawama na Hukumu*

➥ **Je, ninaruhusu hisia za kutokuwa wa maana, lawama na kuhukumiwa vinizuie kupokea kutoka kwa Mungu?**

Baadhi ya silaha za kichini na hatari za ibilisi ni mawazo ya kutokuwa wa maana, lawama na kuhukumika. Lawama hushughulikiwa katika kukiri dhambi na kwa imani kupokea msamaha. Ikiwa hisia za lawama zitaendelea, hizo, pamoja na hisia za kutokuwa wa maana na hukumu, vinatoka kwa Shetani.

Umuhimu wetu uko katika Yesu. Sisi ni haki Yake Mungu katika Yeye. Tuko katika msimamo sawa na Mungu Baba kwa ajili ya Yesu.

Ili tujisikie hivyo ni kujinyima kazi ya ukombozi ya Yesu, haki Yake, na nafasi yetu ndani Yake.

Warumi 8:1 Basi sasa hakuna hukumu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu, wasiotembea katika mwili, bali katika Roho.

2 Wakorintho 5:21 Kwa kuwa Alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu ili tuwe haki Yake Mungu katika Yeye.

Kata hisia hizo. Anza kutangaza Neno la Mungu na uwe na nguvu katika sehemu hizi.

➢ *Matumaini ya Uongo*

➥ **Je, ninaruhusu matumaini ya uongo, ndoto ambayo wakati mwingine baadaye nitaponywa, kuchukua pahali pa imani?**

Kuna matumaini ya kweli ambayo hutangulia imani. Ni kuamini kuwa baadaye tutapokea kile ambacho tunatamani.

Tunaposikia au kusoma Neno la Mungu, tutasonga kutoka mahangaiko hadi matumaini. Lakini, tusipoendelea kutoka matumaini hadi imani, inaweza kuwa matumaini ya uongo.

Waebrania 11:1 Sasa imani huleta matumaini juu ya kitu, ushahidi wa yale hatujayaona.

Tunapotumainia uponyaji, ina maana hatujapata imani ya uponyaji, bali kuwa tunatarajia kupokea siku za usoni

Wakati mwingine mtu huamini kuwa atapona wakati tukio au wakati wa usoni huja. mara nyingi wanajiwekea matarajio yasiyo kweli na kuingia katika kujihukumu.

Matumaini ya uongo iliyoingia katika imani huwa ni ndoto. Ni pingamizi kwa uponyaji ambayo Shetani anataka ukubali – ikatae!

➢ *Mafundisho ya Uongo*

➥ **Je, kuna mbegu za mafundisho ya uongo ambayo nimepokea hapo awali yananizuia kupona?**

Mafundisho ambayo ni kinyume na Neno la Mungu, au kukosa mafundisho mazuri imemruhusu Shetani kuwaibia Wakristo kile kilicho chetu. Mafundisho ya uongo husema:

- ➢ Magonjwa ni mapenzi ya Mungu.
- ➢ Maumivu hukufunza subira.
- ➢ Maradhi yatakuleta karibu na Mungu.
- ➢ Mateso yataleta utukufu kwa Mungu.

Chukua mafundisho ya uongo uliyopokea na useme, "Ninakataa …. leo. Ninaamuru kila wazo lililo kinyume na Neno la Mungu kujionyesha litoke katika fikira zangu."

➢ *Shaka na Kutokuamini*

➥ **Je, nimekosa kuamini moyoni mwangu?**

Kutokuamini inaweza ktuoka kwa mafundisho ya zamani, kutokana na dhambi isiyosamehewa maishani mwetu, au hata kutokana na nyakati za mahangaiko unapojaribu kumwamini Mungu kwa ajili ya uponyaji wa awali. Kutokuamini ni kinyume na imani.

Ikiwa tunapigana na kutokuamini tunaomba, "Bwana nisaidie kutokuamini kwangu!" Na kisha tafakari juu ya kile Neno la Mungu linasema kuhusu uponyaji.

Mariko 9:24 Mara baba ya yule mvulana akapiga kelele akisema, "Bwana, ninaamini; nisaidie katika kutokuamini kwangu!"

➢ *Kuzitegemea Fikira za Kawaida*

➥ **Je, ninaamini fikira zangu badala ya kuacha roho yangu iamini Neno la Mungu?**

Kwa fikira zetu, tunaamini kile tunaona, kusikia, kunusia au kuonja. Tunatakiwa kujua kuwa ufunuo wa Neno la Mungu na wazi sana na kweli kuliko fikira zetu. Hebu tuangazie Thomasi mwenye shaka.

Yohana 20:24-28 Lakini Thomasi aliyeitwa Didimasi, yaani, Pacha, mmoja wa wale kumi na wawili, hakuwa pamoja nao Yesu alipokuja. Hivyo wanafunzi wengine wakamwambia, "Tumemwona Bwana."

Lakini yeye akawaambia, Nisipoona zile alama za misumari mikononi mwake na kuweka kidole change kwenye hizo alama za misumari na mkono wangu ubavuni Mwake, sitaamini."

Baada ya siku nane, wanafunzi Wake walikuwa tena pamoja ndani ya nyumba, naye Thomasi alikuwa pamoja nao. Ndipo Yesu akaja milango ikiwa imefungwa na kusimama katikati yao akasema "Amani iwe nanyi."

Kisha akamwambia Thomasi, "Weka kidole chako hapa na uone mikono Yangu, nyosha mkono wako uguse ubavuni Mwangu. Usiwe na shaka bali uamini tu."

Thomasi akamwambia "Bwana wangu na Mungu wangu!"

Jibu la Yesu kwa Thomasi bado ni jibu bora kwetu leo!

Mst. 29 Yesu akamwambia, "Thomasi kwa kuwa umeniona, umeamini. Wabarikiwe wale hajaniona na bado wameamini."

Omba, "Bwana, na kile Neno Lako linafundisha kiwe wazi na kweli kwangu kuliko chochote naona, kusikia, kugusa, kunusa, au kuonja. Na niingie zaidi ndani ya ulimwengu wa Roho na kuamini Neno Lako!"

ENDELEA KUPONYA KWA KUJIHAMI KWA VITA

Mtambue Adui

Ibilisi ni mnyang'anyi na mwizi. Yeye ni adui wa afya yetu.

Yohana 10:10 Mwizi haji ila kuiba, na kuua, na kuharibu. Nimekuja ili wawe na uzima, na wawe nao tele.

Ibilisi huja kama samba angurumaye akitafuta kuharibu.

1 Petro 5:8,9 Kuweni macho, kwa kuwa dui wenu ibilisi anatembea kama samba angurumaye, akitafuta atakayemla. Mpinge, mkiwa imara katika imani, mkijuwa kuwa mateso hayo hayo wanagumbana nayo ndugu zenu ulimwenguni.

Shetani ni adui wa mwili, nafsi, na roho. Ni lazima tugundue mbinu zake na kumshinda maishani mwetu.

Kuweni na Nguvu katika Bwana

Lazima tujifunze kuwa na nguvu katika Bwana, kuvaa chepeo letu, kuwa macho, tayari kushinda kila vita. Shujaa mkuu, mtume Paulo, alituandikia kuhusu haya.

Waefeso 6:10-13 Mwisho, ndugu zangu, kuweni na nguvu katika Bwana na kwa nguvu za ukuu Wake. Vaeni silaha kamili ya Mungu, kuwa mweze kumshinda ibilisi.

Kwa kuwa hatupigani dhidi ya mwili na damu, bali dhidi ya ngome, ya nguvu, uongozi wa gizani wa nyakati hizi, dhidi ya roho za uovu juu mginguni. Kwa hiyo vaeni silaha nzima ya Mungu, ili mweze kushinda nyakati za uovu, na baada ya kufanya yote, msimame.

Pambanua Mishale ya Shetani

Ibilisi hujaribu kuiba afya yetu kwa kutumia mishale ya moto ya maumivu, dalili za ugonjwa, mawazo ya kinyume, na mashaka.

Waefeso 6:16 Juu ya yote, mkichukua ngao ya imani ambayo mtatumia kuzima mishale ya yule adui.

Tumepewa silaha ya imani ili kupinga vita vya Shetani. Maumivu, dalili, na mawazo ya kinyume ya kutokuamini hayatatushinda ikiwa tutaendelea kutumia ngao ya imani.

➢ *Mawazo Yaliyo Kinyume*

Ni lazima tuchunguze mawazo yetu na tusiruhusu kutokuamini. Njia nzuri ya kufanya haya ni kwa kuweka macho yetu juu ya Yesu.

Matayo 14:27-31 Mara Yesu akanena, akiwaambia, "Muwe na furaha! Ni mimi; msiwe na hofu."

Naye Petro akamjibu na kusema, "Bwana, ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji."

Basi akasema, "Njoo." Na alipokuja Petro kutoka kwa chombo, akatembea juu ya maji akienda kwa Yesu. Lakini alipoona mawimbi yamezidi, akaogopa; na akianza kuzama akaita, akisema, "Bwana, niokoe!"

Na mara moja Yesu akanyosha mkono Wake na kumshika, na kumwambia, "Ewe mwenye imani ndogo, kwa nini ulishuku?"

Tunapoanza kufuata hisia zetu, hofu, mtazamo ulio kinyume, au maneo ya wengine, tutazama.

➢ *Mashaka*

Mashaka, kama kukosa imani, ni kinyume na imani. Mtu hawezi kutembea katika imani na mashaka wakati mmoja! Shaka ni dhambi. Na ni kuamini Neno la Mungu kuwa si la kweli.

Luka 12:22,29 Na akawaambia wanafunzi Wake, "Kwa hiyo nawaambia, msihofu juu ya maisha yenu, mtakachokula; au juu ya mwili, mtakachovaa. Na wala msitafute kile mtakula au kunywa, au kuwa na mahangaiko akilini."

➢ *Zikatae*

Lazima tujifunza kukataa mawazo ya kinyume haraka. Lazima tukatae mawazo ya ugonjwa na maradhi punde yaingiapo akilini mwetu. Paulo aliandika kuwa lazima tulete kila wazo kwa kuyafunga kwa Yesu.

2 Wakorintho 10:3-5 Kwa kuwa hata kama tunatembea katika mwili, vita vyetu si vya mwili. Kwa kuwa sila za vita vyetu si vya hapa bali ni kubwa katika Mungu kwa kuvuta ngome, kuzusha ubishi na chochote kilichojiinua dhidi ufahamu wa Mungu, kuleta kila wazo na kufunga katika utiifu wa Kristo ...

Lazima kila mara tulinde mawazo yetu kuyaweka katika makubaliano na utiifu kwa mawazo ya Kristo kama yanavyodhihirishwa katika Neno Lake kuhusu uponyaji na afya.

Mawazo yetu lazima yawe na nidhamu ili kukataa mawazo au dalili ambazo hazikubaliani na Neno la Mungu.

Tunaitajika kukataa mawazo yaletayo magonjwa kama vile "Nafikiri nashikwa na homa." Hii hufungua mlango ili Shetani atushinde. Tunapokaa macho kwa ujanja wa Shetani, tunaweza kulinda afya yetu.

SIMAMA DHIDI YA MAWIMBI MAISHANI

Katika msemo wa mpanzi, tunaonywa kuwa tukipokea mbegu ya Neno moyoni mwetu, Shetani, inayoonyeshwa na ndege wa shambani, huja na kuiba mbegu hiyo.

Mariko 4:3,4,14-17 Sikilizeni! Tazama, mpanzi alienda kupanda. Na ikawa, baadhi ya mbegu ilianguka kando ya njia; nao ndege wa angani wakaja na kuila.

Kwa kufafanua msemo huu Yesu alisema,
Mpanzi hupanda neno. Ni hawa ndio kando ya njia ambapo neno lilipandwa. Na wanaposikia, Shetani huja haraka na kulichukuwa neno lililopandwa mioyoni mwao. Pia haya hupandwa juu ya shamba lenye mawe, ambao walisikiapo neno, wanalipokea kwa busara; na hawana mzizi ndani yao, na kwa hiyo wao huvumilia tu kwa muda. Baadaye, majaribu na mateso yajapo dhidi ya neno wanatingika au hukasirika.

Yesu alionya kuwa punde tunapopokea kweli fulani kutoka kwa Neno Lake, Shetani atakuja haraka kuliiba. Yesu aliweka wazi kuwa hila za Shetani za kuiba ni kwa kutumia mateso na majaribu.

Mateso na Majaribu

Je, mateso na majaribu ni nini?

Kamusi hutumia maneno kama vile mahangaiko, taabu, mateso, maumivu, kuteswa, na majaribu katika kueleza majaribu. Inasema kuwa mateso ni hali inayozidi, isiyokaribishwa, kuweka maumivu, nidhamu, au mauti hasa kwa sababu ya kidini.

Shenai anajua kuwa ikiwa Neno la Mungu litadumu maishani mwa mtu, yeye hataweza kuwashinda. Kwa hivyo atajaribu kila kitu ili washuku Neno hili.

Ikiwa mtu amepokea Neno la Mungu kuhusu uponyaji na kupokea uponyaji katika mwili wake, Shetani mara nyingi hurusha mishale yake ya dalili na maumivu. Hujaribu kuweka mishale ya mawazo kinyume akilini mwao na kusema ugonjwa umerejea tena.

Mawimbi Makali

Yesu alikuwa ndani ya chombo alipokuwa akifundisha watu waliokusanyika kando ya bahari msemo wa mpanzi. Aliwaonya watu kuwa Shetani atakuja haraka kuiba mbegu ya Neno.

Baadaye siku hiyo, walipokuwa wakivuka kwenda upande wa pili, alienda kulala nyuma ya chombo hicho.

Mariko 4:37-39 Na pakaja wimbi kubwa, na mawimbi yakapiga chombo, kuwa likaanza kujaa maji, lakini Yeye alikuwa ngamani, amelala. Nao wakamwamsha na kumwambia "Mwalimu, je, hujali kuwa tunaangamia?" Kisha akaamka na kukemea mawimbi, na kuiambia bahari, " Amani, tulieni!" nayo mawimbi yakatulia na kuka utulivu mkubwa.

➢ *Huja Ajili ya Neno*

Majaribu na mateso huja kwa ajili Neno kwa mfano wa mawimbi makali. Kama vile Yesu alisema, shetani alikuja haraka kuiba mbegu ya Neno kutoka mioyoni mwao. Badala ya kusimama katika imani nakuyaambia mawimbi yenyewe, walikasirika.

Wavuvi hawa, waliokuwa na ustadi katika kushughulikia mawimbi bahari, walibabaika na kuhofu kuwa watazama. Walikasirika kuwa Yesu alikuwa amelala na kuonekana hajali kuhusu hali yao. Walimwamsha Yesu na kumlaumu, "Mwalimu, je, hujali kuwa tunaangamia?"

Labda, tumejibu mateso na majaribu ya ugonjwa, maradhi na maumivu kwa kulia kwa Mungu "Je, hujali kuwa naangamia? Je, hujali kuwa dalili hii imekuja juu yangu?" labda, sisi kama wanafunzi wa kwanza, tumekasirika na kumlaumu Mungu kwa kuruhusu haya yafanyike kwetu. Kwa kufanya hivyo, sisi pia tumemruhusu Shetani kuiba mbegu ya Neno kutoka mioyo yetu.

➢ *"AmaniTulia"*

Mariko 4:39-41 Naye akaamka na kuyakemea mawimbi, na kuiambia bahari "Amani, tulia!" Nayo mawimbi yakatulia na kuwa na utulivu wa ajabu. Lakini akawambia, "Kwa nini mkawa na hofu? Kwa nini hamna imani?"

Nao wakaogopa sana, na kuambiana, "Ni nani huyu, kuwa hata mawimbi na bahari vinamtii Yeye!"

Ikiwa Shetani anaweza kuiba Neno tulilopokea, anaweza pia kuleta tena dalili za magonjwa na maradhi.

Shetani anapoleta mawimbi dhidi yetu, sisi, kama Yesu, lazima tusimame katika chombo chetu na kwa ujasiri, kunena Neno la Mungu. Tunapofanya hivyo, imani yetu

itakuwa. Tutaonyesha Neno la Mungu maishani mwetu na kuwa na nguvu na katika imani!

Uamuzi Wetu

Wakati mishale mikali ya majaribu na mateso ijapo, lazima tufanye uamuzi.

- ➢ Je, tuamini Neno la Mungu, au imani ya tamaduni zetu?
- ➢ Je, tuamini Neno la Mungu, au tuamini dalili zetu?
- ➢ Je, tuamini Neno la Mungu, au tuamini maneno ya marafiki wasioamini?
- ➢ Je, tuamini Neno la Mungu, au taarifa ya daktari?

Lazima tuamue wenyewe kusimama juu ya Neno la Mungu bila kujali madaktari, marafiki, au dalili zinavyosema. Hatuwezi wakati huu, kusimama juu ya imani ya mwingine, mafundisho, au ushuhuda. Lazima tusimame katika imani yetu wenyewe juu ya Neno la Mungu.

Shughuli za Ulimwengu Huu

Yesu pia alionya kuwa Neno tunalopokea linaweza kutolewa ndani ya maisha yetu, ikiwa tutaruhusu shughuli za ulimwengu huu, mawazo ya kidunia na tabia kuingia akilini mwetu.

Mariko 4:19 ... na shughuli za ulimwengu huu, udanganyifu wa mali, na kutaka mambo mengine yaiongiayo huharibu neno na kuwa halina matokeo.

Tunapoweka udongo wa mioyo yetu sawa, na kuipa maji kwa kuendelea kutafakari juu ya Neno la Mungu, mioyo yetu itasalia katika shamba nzuri. Tutaishi katika ushindi na Baraka tele.

Mariko 4:20 Lakini hii ni ile iliyopandwa kwenye udongo mzuri, wale wanalisikia neno, kulikubali, na kuzaa matunda: Wengine thelathini, wengine sitini, na wengine mia.

USITOE NAFASI KWA SHETANI

Tusitoe nafasi kwa ibilisi kwa kuweka dhambi nje ya maisha yetu.

"Usitende Dhambi Tena"

Baada ya Yesu kumponya mwanamume tasa katika bwawa la Bethsaida aliyekuwa na roho wa kupooza kwa miaka thelathini na nane, Yesu alienda kumtafuta ili ampe ujumbe maalum.

Yohana 5:14 Baadaye Yesu alimkuta hekaluni, na akamwambia, "Tazama, umeponywa. Usitende dhambi tena, au kitu kibaya kitendeke maishani mwako."

Tukishikilia dhambi tusiokiri, au dhambi ambayo hatujatubu maishani mwetu, tunatoa nafasi kwa ibilisi kuleta magonjwa juu yetu, na kutuibia uponyaji wetu.

Waefeso 4:27 ... wala kutoa nafasi kwa ibilisi.

Usitoe Nafasi kwa Roho

Roho za kupooza hutafuta nafasi ili kurudi na kuingia nyumba yao.

Matayo 12:43-45 Wakati roho mchafu anatoka nje ya mtu, anapitia mahali jangwa, akitafuta kutulia, naye hukosa. Kisha husema, 'nitarejea kwa nyumba yangu nilikotoka.' Na anaporudi, anaikuta wazi, imefagiliwa na kupangwa sawa. Naye huondoka na kuwaleta roho zingine saba ovu zaidi kuliko yeye, nao huingia na kukaa hapo; na hali ya mwisho ya mtu huyo ni mbaya zaidi ya ile ya kwanza. Ndivyo itakuwa na kizazi hiki kiovu.

Weka Nyumba Ijae

Lazima tuweke nyumba zet, miili zetu, imejaa.

➢ *Na Yesu*

Ufunuo 3:20 Tazama, nasimama mlangoni nabisha. Ikiwa yeyote ataisikia sauti Yangu na kuufungua mlango, Nitaingia kwake na kula naye, naye pamoja Nami.

➢ *Na Roho Mtakatifu*

1 Wakorintho 3:16 Je, hamjui kuwa ninyi ni hekalu la Mungu na kuwa Roho wa Mungu hukaa ndani yenu?

➢ *Na Neno la Mungu*

Yohana 15:7 Mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, mtauliza mnachotaka, na mtapewa.

➢ *Na Imani*

1 Yohana 5:4 Kwa kuwa chochote kinachozaliwa na Mungu hushinda ulimwengu. Na huu ndio ushindi ulioshinda ulimwengu – imani yetu.

Hali kamili Yake Mungu haistahimili dhambi. Tukiruhusu dhambi iendelee maishani mwetu, tunajitoa katika ulinzi wa Mungu na kufungua milango Shetani atuibie afya na amani ya mawazo.

PIGANA ILI KUIFADHI UPONYAJI WAKO!

Vaa Silaha

Weka chepeo yako ya imani vizuri na kila mara uwe tayari kuzima mishale ya Shetani yenye moto ya shaka na kutoamini.

Afya ni Mapenzi ya Mungu

Unaweza kutembea katika afya ya Mungu ukijua mapenzi ya Mungu upate uponyaji.

Matendo 10:38 ... jinsi Mungu alimpaka mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu na nguvu, aliyeenda kila mahali akifanya mema na kuponya wote walioteswa na ibilisi, kwa kuwa Mungu alikuwa Naye.

3 Yohana 2 Wapendwa, naomba kuwa mweze kuendelea katika mambo yote na kuwa katika afya nzuri, kama vile nafsi yenu inavyoendelea.

Shikilia Imani kwa Nguvu

Lazima tushikilie sana imani tunayokiri. Kile tunakiri ndivyo tutaishi, kile tufanyacho, na kile tusemacho.

Waebrania 4:14 Basi kuona kuwa tunaye Kuhani Mkuu ambaye amepita mbingu, Yesu Mwanawa Mungu, basi na tushikilie sana kukiri kwetu.

Warumi 10:6-10 Lakini haki ya imani hunena hivi, "Usiseme moyoni mwako, 'Nani atapaa mbinguni?' "(yaani, kumleta Kristo kutoka juu) au," 'Nani atashuka kutoka jehanamu?' "yaani, kumtoa Kristo kutoka kwa wafu).

Lakini inasema nini? "Neno liko karibu nanyi, hata kinywani mwako na moyoni mwako" (yaani, neno la imani tunalohubiri): Kuwa ukikiri kwa kinywa chako Bwana Yesu na kuamini moyoni mwako kuwa Mungu amemfufua kutoka wafu, utaokolewa. Kwa kuwa kwa moyo mtu huamini kwa haki, na kwa kinywa hukiri wokovu.

Lazima tuwe waangalifu tusiruhusu vinywa vyetu kuharibu ushuhuda wetu kwa maneno potovu. Tunashikilia sana imani na Neno la Mungu kwa kusema kila wakati kile Neno la Mungu linasema.

Nena Neno la Mungu

Bila kujali dalili kinyume, endelea kuamini na kunena Neno la Mungu.

Yoeli 3:10b ... naye mnyonge aseme, `Ninazo nguvu.'

2 Wakorintho 4:13 Lakini kwa kuwa tunaye roho sawa wa imani, kulingana na kile kimeandikwa, "Niliamini na kwa hiyo nilisema," nasi pia tunaamini na kunena.

Kwanza huonekana ngeni na ngumu, lakini ikiwa tutajikaza kunena Neno na tusiwe na shaka, tutaishi katika ushindi ambao ni wetu katika Kristo!

Kuweni Zaidi ya Washindi

Lazima tujue kuwa sisi tu zaidi ya washindi!

Warumi 8:37-39 Na katika mambo haya yote sisi tu zaidi ya washindi katika Yeye aliyetupenda. Kwa kuwa nimekubali kuwa si mauti wala uhai, wala malaika wala ngome wala nguvu, wala vitu vya sasa au baadaye, wala juu au chini, au chochote kilichoumbwa, haitatutenganisha na upendo wa Mungu ambao uko katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Hali, mapepo, au watu wengine hawatatutenganisha na ulinzi wa Mungu. Ni sisi tu tunaoweza kujitenga. Kwa kulijua Neno na kuwa sisi ni nani katika Kristo, tunaweza kulinda imani na kusalia katika afya.

Ni mapenzi ya Mungu watu kuponywa, kuweka uponyaji wao, na kuishi katika afya nzuri. Lazima tuelewe na kufuata mpango wa Mungu wa vita vya kiroho na imani. Lazima tupinge shaka na dhambi. Kwa kujua, kuamini, kunena, na kutenda Neno la Mungu, tutaendelea kuishi katika afya ya mwili na nafsi!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, mambo gani matatu yanayoweza kumzuia mtu uponyaji na unawezaje kuyashinda?

2. Je, nini kiunganishi kati ya msemo ya Mpanzi na Mawimbi Makali na hii inahusiana vipi nawe?

3. Je, vipi tuweza kumpiga Shetani na kulinda uponyaji wetu?